SIRI PART 2

MAISHA NA KIFO CHA MELANIE CHUMA

SEASON 9

MTUNZI: PATRICK.CK



HADITHI HII NI MALI YA MWANDISHI NA HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA KWA HIYO HAIRUHUSIWI KUCHAPISHA, AU KUITUMIA KWA NAMNA NYINGINE HADITHI HII BILA RUHUSA YA MWANDISHI.HATUA KALI ITACHUKULIWA KWA YEYOTE ATAKAYEKIUKA MASHARTI HAYA..

SIMULIZI NYINGINE ZA MTUNZI PATRICK.CK

1.MISS TANZANIA
2.I WAS WRONG
3.TEN CHAPTERS
4.I DO
5.SERENA
6.BEFORE I DIE
7.BEYOND PAIN
8.PENIELA
9.QUEEN MONICA
10.THE FOOTBALL
11.I DIED TO SAVE PRESIDENT
12.KIAPO CHA JASUSI
13.KIKOSI CHA SIRI
14.SIRI

MAWASILIANO
0764294499

ILIPOISHIA SEHEMU ILIYOPITA

“Mathew unaweza ukasimamisha gari?Kuna kitu nataka uone” akasema Ruby na Mathew akatafuta sehemu nzuri akasimamisha gari .

“Kuna nini Ruby?akauliza Mathew

“Nimepata taarifa za Melanie Davis” akasema Ruby na kumpa Mathew kompyuta ili asome

“It’s her ! akasema Mathew baada ya kuiona picha ya Melanie Davis

“Huyu ndiye Yule mwanamke niliyekuwa ninamzungumzia.Huyu ndiye ambaye nilimshuhudia Dubai akisaini makubaliano ya kupokea fedha kwa niaba ya James Kasai. Hata ukitazama sura yake haina kovu lolote ni kama ile picha niliyoichora” akasema Mathew

“Taarifa inaonyesha anaitwa Melanie Davis.Ni raia wa Ufaransa mwenye asili ya jamhuri ya kidemokrasia ya Congo”

“Melanie Davis ana asili ya Congo ! Mathew akashangaa

na kuendelea kusoma ile taarifa na kuimaliza

“Taarifa inaonyesha Melanie Davis ana utajiri mkubwa aliorithi kutoka kwa wazazi wake waliofariki katika ajali.Anatajwa kuwa miongoni mwa mabilionea wenye umri mdogo lakini haijaonyesha anamiliki miradi au biashara zipi nchini Ufaransa na hata wazazi wake hawajatajwa kwa majina ili tujue walikuwa wanamiliki miradi ipi.Bado kuna ukakasi kuhusu huyu Melanie Davis”akasema Mathew

“Ninajiuliza kama anatajwa kuwa miongoni mwa mabilionea wakubwa nchini Ufaransa amekuja kutafuta nini Tanzania? Akauliza Ruby

“Yawezekana amewekeza hapa Tanzania na ndiyo maana IS wanapitisha fedha kwake.Ninadhani hata vyombo vya fedha havijaweza kuwa na mashaka naye kwa vile ni mtu mwenye utajiri mkubwa.Ruby tutaendelea baadae kuwachimba hawa watu wawili Melanie Davis na Melanie Chuma.Kwa sasa tuwahi nyumbani kwa Dr

Sebastian” akasema Mathew na kuingia barabarani wakaendelea na safari

“Melanie Davis ambaye ninaamini ndiye aliyesaini makubaliano ya fedha na IS na ndiye tunayeamini ni mchumba wa Gosu Gosu anatokea Ufaransa.Gosu Gosu naye alikwenda Ufaransa na baada ya kurejea ndipo akaanza kuonekana na huyo mwanamke.Ni vipi mahusiano yao yalianza? Je walikutana Ufaransa? Nini anakifanya huyu mwanamke hapa nchini ? Melanie Chuma amefanana

naye kwa kila kitu je wana undugu au imetokea tu wakafanana? Au ni mtu mmoja? Haya yote baadae kwa sasa ngoja tumsake kwanza huyu daktari aliyetaka kumuua Gosu Gosu" akawaza Mathew

Walifika katika nyumba anakoishi Dr Sebastian kwa mujibu wa maelekezo waliyopewa kule hospitali.Ni nyumba ambayo ilikuwa na uzio wa maua na geti la bati.Mathew na Ruby wakashuka garini na kuliendea geti kwa tahadhari kubwa.Akajaribu kulisukuma

geti halikuwa limefungwa wakaingia ndani.Taratibu wakaelekea hadi katika mlango mkubwa wa kuingilia ndani ulikuwa umefungwa.Mathew akazunguka nyuma ya ile nyuma ambako kulikuwa na mlango mwingine akajaribu kuufungua nao ulikuwa umefungwa.Akatoa vifaa Fulani vidogo na kuvichomeka katika kitasa akaufungua mlango wakaingia ndani wakaanza kukagua vyumbani.Katika chumba kikubwa cha kulala wakakuta vitu vimepanguliwa

hovyo..Kabati la nguo lilikuwa tupu

“Tumechelewa.He’s gone.Inaonekana baada ya kufanya kitendo kile alikuja hapa na kuchukua vitu akaondoka haraka.Unaweza ukajua mara ya mwisho alizungumza na nani?akauliza Mathew wakatoka na kurejea katika gari Ruby akachukua kompyuta yake na kuziingiza namba za Dr Sebastian katika program maalum na baada ya dakika mbili akasema

“Aliwasiliana na mtu anaitwa Salome Mtete”

akasema Ruby na kuufungua ujumbe huo

“Unaweza ukafuatilia na kujua mahala alipo?akauliza Mathew na Ruby akafungua program nyingine akamtafuta huyo mtu aliyewasiliana naye mara ya mwisho akaweza kujua mahala alipo.

“Samawati tower” akasema Mathew kisha akaondoa gari wakaondoka.

ENDELEA.....

Baada ya kutoka katika geti la hospitali ya Mtodora Dr Sebastian alichukua simu na kumpigia mpenzi wake Salome Mtete

“Hallo Darling” akasema Salome baada ya kupokea simu

“Salome ninakuja hapo kazini kwako muda si mrefu naomba usitoke nisubiri tafadhali” akasema Dr Sebastian.

“Sawa nakusubiri mpenzi” akajibu Salome na Dr Sebastian akakata simu kisha akaizima kabisa.

Kutoka hospitali anakofanya kazi hadi nyumbani kwake ilimchukua dakika ishirini na tano.Alipofika nyumbani kwake akashuka garini huku akikimbia na kufungua mlango akaelekea chumbani kwake akachukua sanduku lake kubwa akafungua kabati na kuanza kupakia nguo haraka haraka halafu akafungua ndoo za kabati akachukua nyaraka zake za muhimu.Akaangalia mle chumbani kama kuna kitu cha muhimu amekisahau na aliporidhika kwamba kila kitu kiko sawa akatoka akafunga

nyumba yake na kuondoka.Moja kwa moja akaelekea katika jengo la kibiashaa lililojulikana kama Samawati tower anakofanya kazi mchumba wake Salome.Alipofika akaegesha gari na kushuka garini akatembea haraka haraka kuelekea katika katika duka la kuuza vifaa vya electroniki anakofanya kazi Salome ambaye alipomuona akatoka akamfuata.

“Seba kuna nini leo?Mbona unaonekana una haraka sana? akauliza Salome

wakati wakishuka ngazi kwa haraka kuelekea chini

“Nimepata safari ya dharura ya kikazi ndiyo maana unaniona nikiwa na haraka namna hii” akasema Sebastian

“Unasafiri kwenda wapi?akauliza Salome lakini Seba hakumjibu akampatia funguo za nyumba yake

“Funguo hizi za nyumba yangu utazitunza.Gari pia ninakuachia utaendelea kulitumia hadi pale nitakaporejea” akasema Dr Sebastian

“Seba mbona hutaki kunieleza unakwenda wapi?akauliza Salome

“Nitakupigia simu nikifika” akasema Sebastian huku akifungua buti ya gari na kutoa sanduku lake akaita taksi halafu akambusu Salome

“Baki salama Salome.Nakupenda sana” akasema Dr Sebastian na kuingia katika taksi akaondoka akimuacha Salome akiwa ameduwaa.Hakuwahi kumuona mchumba wake akiwa katika hali ile.

“Seba amepatwa na nini?Mbona ghafla namna hii?Halafu mbona anaonekana kuwa na wasiwasi mwingi?akajiuliza Salome wakati taksi aliyopanda mpenzi wake ikitoka katika geti la kuingilia Samawati tower.

Dr Sebastin alimuelekeza dereva wa ile taksi aliyopanda ampeleke sehemu Fulani na alipomfikisha mahala hapo akamlipa fedha akashuka halafu akaifuata gari moja nyeusi iliyokuwa imeegeshwa pembeni ya kibanda cha

kuuzia magazeti akaufungua mlango na kuingia kisha lile gari likaondoka.Kulikuwa na mtu mmoja tu mle garini ambaye hakumuuliza chochote Dr Sebastian.Gari lile alilopanda Seba lilikwenda hadi katika nyumba iliyozungushwa ukuta wa rangi nyeupe na juu kukawekwa seng'enge.Akapiga honi geti likafunguliwa wakaingia ndani.Yule dereva akashuka akamfungulia mlango Dr Sebastian na kulishusha sanduku lake.Toka ndani ya ile nyumba wakatoka watu watatu

na mmoja wao akiwa ni Edwin Mbeko mkurugenzi msaidizi wa SNSA.

“Dr Sebastian karibu sana.Umefika kwa wakati muafaka” akasema Edwin Mbeko huku akiitazama saa yake

“Ahsante sana Edwin” akasema Dr Sebastian

“Dr Sebastain naiomba simu yako” akasema Edwin na kuichukua simu ya Sebastian akaikanyaga ikasambaratika halafu akamtazama DrSebastian na kusema

“Dr Sebastian taarifa niliyoipata kutoka kwa watu wangu ni kwamba yule jamaa yuko hai” akasema Edwin na Dr Sebastina akastuka sana

“Yuko hai?akauliza

“Ndiyo yuko hai.Madaktari wamefanikiwa kuokoa maisha yake na hii inaashiria kwamba hukuifanya vyema kazi yako”

“That’s impossible.Sumu niliyomchoma ni kali sana na inayoua baada ya muda mfupi.Niliichoma sumu ile katika chupa ya maji aliyokuwa ametundikiwa na niliamini ndani ya muda mfupi

angepoteza maisha kutokana na ukali wa sumu ile na……..” akasema Dr Sebastian na Edwin akamkatisha

“Dr Seba makubaliano yetu yalikuwa ni kumuua Yule jamaa Gosu Gosu lakini hukufanya hivyo na Yule jamaa ni mzima.Kibaya zaidi ni kwamba tayari umefahamika kuwa ni wewe uliyetaka kumuua na tayari suala hilo limefika katika vyombo vya uchunguzi.Tumeua watu wawili muuguzi mkuu na muuguzi aliyepangiwa chumba

cha Gosu Gosu lakini hakuna manufaa yoyote tuliyoyapata hivyo basi wewe ni mzigo ambao hatuwezi kuubeba” akasema Edwin Mbeko na kwa kasi ya ajabu akachomoa bastora iliyofungwa kiwambo cha kuzuia sauti na kumpiga Dr Sebastian risasi katika paji lake la uso akaanguka katika majani.Hakuwa na uhai tena

“Get rid of the body ! Edwin akawaamuru vijana wake wawili halafu akaelekea katika gari lake akaliwasha na kabla ya kuondoka akampigia simu Devotha

“Hello Edwin naamini kila kitu kimekwenda vizuri” akasema Devotha baada ya kupokea simu

“Madam Devotha mambo hayajaenda vyema.Kuna makosa yamefanyika katika lile zoezi la kumuua Gosu Gosu na kwa taarifa niliyoipata ni kwamba bado yuko hai” akasema Edwin

“Nini kimetokea Edwin? Suala lile lilikuwa la muhimu sana kwani Yule jamaa endapo akipona anaweza akawaeleza wenzake mambo anayoyafanya Melanie hivyo kumuweka

katika hatari kubwa na Melanie akiingia katika hatari sisi sote tunakuwa hatarini” akasema Devotha

“Daktari niliyemtumia alifanya makosa kidogo na kusababisha hayo yakatokea lakini tayari nimekwisha mshughulikia.Nimemuua ili kuondoa matatizo kwani suala hili limekwisha fika katika vyombo vya dola lakini nitalimaliza endapo litataka kuleta shida upande wetu” akasema Edwin

“Edwin jitahidi sana kusitokee tena makosa ya aina

yoyote ile.We’re so close.Tumekaribia sana kumaliza misheni yetu”akasema Devotha

“Nitajitahidi madam Devotha” akasema Edwin

“Vipi kuhusu huyo mkurugenzi mpya unamuonaje? Anaweza akawa kikwazo katika mipango yeu?akauliza Devotha

“Kama nilivyokwambia asubuhi kwamba huyu bado ni mgeni na hajui mambo mengi hivyo hadi pale atakapoanza kuielewa idara hii atakuta tayari tumekwisha kamilisha

kila kitu.Kwa muonekano wake haonyeshi kama atakuwa kikwazo chochote kwetu.Kwa muda huu mfupi toka amefika nimejitahidi kujenga ukaribu naye ili niweze kumsoma vizuri.Hatakuwa na shida usihofu”akasema Edwin

“Safi sana edwin.Sikukosea kukuweka hapo.Umekuwa ni msaada mkubwa kwangu na ninakuahidi kwamba hautajutia hiki unachokifanya.Matunda yake ni makubwa sana.Tumebakiza muda mchache tu na utaanza

kuyaona matunda.Kwa sasa endelea kufuatilia kwa karibu sana maendeleo ya Gosu Gosu na kutafuta namna nyingine ya kumuua kwani kitendo alichokifanya huyo daktari leo cha kushindwa kumuua tayari kimewasha taa nyekundu na wataanza kuchukua tahadhari kubwa wakimlinda” akasema Devotha

“Usijali madam ninafuatilia kwa karibu sana na tutamuondoa Gosu Gosu kabla hajaleta hatari yoyote kwetu” akasema Edwin

“Umekwisha wasiliana na Melanie?akauliza Devotha

“Melanie nimewasiliana naye asubuhi ya leo na hivi sasa niko njiani ninaelekea kupanda helkopta kuelekea Kagera ambako ninakwenda kuwapokea.Kila kitu kinakwenda vizuri.Kwa kuwa wataingia hapa Tanzania jioni watalala Kagera na kesho nitawaleta Dar es salaam”

“Edwin kuwa makini sana kwani unajua namna James Kasai anavyotafutwa kwa nguvu kubwa.Hili ni moja ya jambo gumu ambalo tumewahi

kulifanya na sikupenda wazo la Melanie la kutaka James aingie Tanzania kwani endapo akigundulika kila kitu kitakuwa kimekwisha.Serikali za afrika mashariki zimewekeza nguvu kubwa katika kumsaka James” akasema Devotha

“Nalifahamu hilo madam Devotha na nimekwisha jiandaa kikamilifu kuhakikisha James anaingia hapa nchini na kutoka bila matatizo yoyote.Hilo lisikupe hofu madam” akasema Edwin

“Sawa Edwi naomba tafadhali unijulishe kila hatua,kila kinachoendelea.Na kama kuna tatizo lolote tafadhali nijulishe haraka sana”akasema Devotha na kuagana na Edwin

“Sifahamu kwa nini Melanie aliamua kuingia katika mahusiano na Yule jamaa Gosu Gosu wakati akifahamu kwamba ni mtu hatari.Matokeo yake ndiyo haya tunalazimika kuanza tena mipango ya kumuua na kama tusipofanikiwa kumuua Yule jaama anaweza akawa ni mtu

hatari sana kwetu.Nitakaporudi toka Kagera nitakaa na vijana wangu tuone namna mpya ya kuweza kumuondoa Gosu Gosu” akawaza Edwin.

Aliwasili katika jengo la ofisi zao,akashuka garini na kuelekea katika ofisi yake.Akampigia simu rubani wa helkopta ya idara yao akamtaka ajiandae kwa safari ya kuelekea Kagera.Baada ya dakika ishirini akajulishwa kwamba helkopta iko tayari akachukua baadhi ya vitu vyake vichache muhimu

akatoka bila kuaga mtu na kuelekea katika helkopta akaondoka kuelekea Kagera.

****

Mathew na Ruby waliwasili Samawati Tower.Ni jengo lililokuwa na biashara nyingi hivyo watu walioingia na kutoka walikuwa wengi pia.

“Bado yuko hapa hapa” akasema Ruby aliyekuwa akimfuatilia Salome kwa kutumia program maalum katika kompyuta yake

“Mpigie simu mtake ashuke tuonane naye” akasema Mathew na Ruby akachukua simu akaziandika namba za Salome akampigia

“Hallow” akasema Salome baada ya kupokea simu

“Hallow Salome habari yako” akasema Ruby kana kwamba ni mtu anayemfahamu vyema

“Nzuri dada habari yako nawe”

“Salama kabisa.Samahani Salome yawezekana hunifahamu lakini mimi ninaitwa Dr Prisca ninafanya

kazi na Dr Sebastian ndiye aliyenipa namba zako za simu”

“Ouh sawa Dr Prisca nikusaidie nini?akauliza Salome

“Dr Sebastian amepatwa na safari ya ghafla leo na wakati akiondoka mimi sikuwepo alinipigia simu akanipa namba zako niwasiliane nawe kuna vitu Fulani ninavihitaji na aliniambia nikuone wewe” akasema Ruby

“Wewe uko wapi?akauliza Salome

“Niko hapa chini katika jengo ulimo.Unaweza ukashuka tafadhali tukaonana mara moja?akauliza Ruby

“Sawa ninakuja.Naomba kama dakika tano tu nitakuwa hapo chini” akasema Salome na kukata simu.Wakashuka garini na kwenda kusimama karibu na mlango mkubwa wa kuingilia ndani ya jengo.

“Huyu Salome lazima atakuwa ni mtu wa karibu na Dr Sebastian kwani baada ya kuwasiliana naye akazima simu kabisa.Tukimfuatilia huyu anaweza akatusaidia

kujua mahala aliko Dr Sebastian”akasema Mathew

“Nimeweka program Fulani katika simu yangu.Nitakapokuwa karibu naye program hiyo itaitafuta simu yake na kujiunganisha nayo kisha tutaanza kumfuatilia na kila pale atakapowasilian na Dr Sebastian tutafahamu” akasema Ruby.Baada ya dakika chache simu ya Ruby ikaita.Alikuwa ni Salome

“Hallow dada uko wapi?akauliza Salome.

“Niko hapa nimesimama karibu na maua haya ya rangi nyeupe” akasema Ruby

“Sawa nimekuona” akasema Salome na kukata simu.Baada ya dakika chache mwanamke mmoja aliyevaa suruali ya jeans rangi ya bluu akajitokeza.

“Habari yako dada” akasema Salome

“Nzuri Salome.Habari yako?

“Karibuni sana” akasema Salome.

“Ahsante.Huyu anaitwa Dr Cosmas sote kwa pamoja

tunafanya kazi kitengo kimoja na Dr Sebastian.Alinipigia simu na kunieleza kwamba amepatwa na safari ya dharura akanieleza nije nikuone.Amepatwa na dharura gani? Ruby akauliza

“Hata mimi hakuniambia amepatwa na dharura gani.Alinipigia simu mchana huu akaniambia kwamba anakuja kuniona.Alifika hapa nikaonana naye akaniambia kwamba amepata safari ya dharura ya kikazi akaniachia gari na funguo ya nyumba yake akapanda taksi na kuondoka”

“Alikueleza anakwenda wapi? Akauliza Mathew

“Hapana hakunieleza anakwenda wapi.Aliponikabidhi funguo za gari na za nyumba yake akaondoka.Nilidhani nyie wenzake mtakuwa mnajua ni kazi gani ya dharura iliyojitokeza”

“Alikuwa amebeba nini?akauliza Mathew

“Alikuwa na sanduku kubwa la nguo”

“Ni mara yake ya kwanza kuondoka ghafla namna hii au amekwisha wahi fanya hivyo

siku za nyuma?Mathew akauliza

“Hajawahi kuondoka kama alivyoondoa leo.Imekuwa ghafla mno na alionekana kuwa katika haraka kubwa” akasema Salome na Mathew akamtazama Ruby

“Hakuna mzigo mwingine alikuachia?akauliza Ruby

“Zaidi ya gari na funguo za nyumba yake hakuna kingine chochote alichoniachia”akajibu Salome

“Ahsante Salome.Kama hakukuachia chochote basi tutamsubiri hadi atakaporejea”

“Nini mlikuwa mnakihitaji toka kwake? Yawezekana amekiacha nyumbani kwake akasahau kuniambia.Ninaweza kwenda kuwatazamia nyumbani kwake” akasema Salome

“Ni vifaa vya kazi.Usijali tutawasiliana naye na kumuuliza mahala alikoviweka.Ahsante Salome tunashukuru kwa muda wako” akasema Ruby wakamuaga Salome na kuelekea katika gari lao.

“Do you believe her?akauliza Ruby

“Ndiyo.Hafahamu chochote.Alichosema ni cha kweli.Sebastin tayari amekwisha toroka na hatujui amekwenda wapi.Kwa kuwa suala hili tayari liko katika mikono ya polisi kama amekimbilia mikoni lazima atapatikana.These people are very smart.Walikwisha jiandaa kwamba baada tu ya kumuua Gosu Gosu basi Dr Sebastian aondoke haraka sana Dar es salaam” akasema Mathew huku akiliondoa gari

“Alichokifanya Dr Sebastian ni kucheza na Yule

muuguzi mkuu ambaye naamini ndiye aliyemuondoa Yule muuguzi katika chumba cha Gosu Gosu ndipo Sebastian alipopata nafasi ya kwenda kumchoma ile sindano ya sumu.Kwa bahati nzuri alikuwepo kijana wetu pale hospitali ambaye aliweza kusaidia sana kufikisha taarifa kwa madaktari ambao waliweza kuokoa maisha ya Gosu Gosu.Huu lazima ni mtandao mpana ambao unajua nini wanakifanya”akasema Mathew

“Ninachojiuliza kwa nini GosuGosu awe ni hatari kwao hadi watake kumuua? Hii ni mara ya pili wanajaribu kumuua na ninaamini wataendelea kujaribu tena na tena”akasema Ruby

“Ni kwa sababu kuna kitu anakifahamu na wanaogopa kwamba akipona anaweza akaweka wazi na wao hawati kijulikane.Naomba Mungu amsaidie Gosu Gosu apone kwani ni mtu anayeweza kutusaidia sana kufahamu kinachoendelea na hasa kuhusu huyu Melanie Davis

ambaye tunaamini ndiye Yule anayeshirikiana na James Kasai.Natamani sana kufahamu wawili hawa namna walivyokutana na kuanza mahusiano yao.Nataka kupata taarifa za kutosha kuhusu huyu Melanie Davis ambaye anaendelea kuumiza vichwa vyetu" akasema Mathew

"Nini kinafuata?Ruby akauliza

"Tunarejea tena hospitali.Wenzetu wanatuhitaji kule" akasema Mathew

Baada ya muda Ruby akaita

“Mathew”

“Unasemaje Ruby?akauliza Mathew

“Natambua ulisema hutaki kuulizwa kuhusiana na wapi ulikokuwa na nini hasa kilikutokea lakini inaniwia ugumu sana Mathew.Tafadhali natamani sana kufahamu kilichokutokea.Unaonekana umepitia masahibu makubwa” akasema Ruby na kuinamisha kichwa kwa sekunde kadhaa halafu akasema

“Hakuna siku ambayo sikuwahi kudondosha chozi kukulilia Mathew.Ninakupenda Mathew kiasi ambacho siwezi kueleza.Nimefurahi nimekuona tena.Nafsi yangu imetulia lakini nahisi kuna kitu kinaukata moyo wangu taratibu.Natamani sana kujua kinachoendelea Mathew katika maisha yako. Sifahamu nini kitatokea kesho.Utaondoka tena na kuniacha hapa peke yangu?” akasema Ruby na kulengwa machozi.Mathew

akaendelea kuendesha gari baada ya muda akasema

“Ruby kwa muda huu wote niliopotea sikuwahi kupitisha hata usiku mmoja bila kuileta sura yako kichwani kwangu.Umekuwa ukiishi ndani mwangu” akasema Mathew na kunyamaza kidogo

“Kama unakumbuka nilikuahidi kwamba baada ya kurejea kutoka kuwakomboa mateka mimi na wewe tungepata nafasi ya kwenda sehemu tukapumzike.Nilikuwa namaanisha kile nilichokisema lakini kwa bahati mbaya

sikuweza kurejea tena nikapotelea huko huko.Hata nikiwa huko nilikokuwa bado umeendelea kuwepo moyoni na katika akili yangu.Wanasema ili kujua thamani ya kitu ni hadi pale utakapokikosa.Nimekukosa kwa miaka mitatu na nimeiona thamani yako kwangu.Sitaki kukukosa tena Ruby kwani nakupenda pia.Lakini……” akasema Mathew na kutulia kidogo.Ruby akamkazia macho kusikia kile alichotaka kukisema

“Uliniuliza kama nitaondoka tena na kukuacha peke yako” akasema Mathew na kunyamaza baada ya dakika moja akasema

“Ndiyo nitaondoka baada ya operesheni hii kumalizika lakini nitarejea tena kwa ajili yako.Nafahamu unaumia ukisikia hivyo lakini ni lazima nipotee tena na nitakaporudi itakuwa ni moja kwa moja sintaondoka tena.Ninachokuomba pale nitakapoondoka usilie tena bali uwe mvumilivu ukiendelea kuniombea ili nirejee salama”

akasema Mathew na Ruby akakiegemeza kichwa katika kiti.

“Mathew neno lako ni amri kwangu.Chochote utakachokisema mimi nitakitii.Nitakusubiri kama ulivyoahidi kwani naamini wewe hutembea katika maneno yako.Ukiahidi kitu lazima ukitimize.Niko tayari kukusubiri hata kama itanigharimu maisha yangu yote kwa sababu wewe ni mwanaume pekee uliyejaa ndani ya moyo wangu”akasema Ruby huku

macho yake yakilengwa na machozi.Mathew akamtazama na kutabasamu

“C’mon cry baby.Please don’t cry “ akasema Mathew na Rubyakafuta machozi

“Jambo lingine nitakapoondoka tafadhali usijaribu kunitafuta nimekwenda wapi.Nafahamu wewe unao uwezo mkubwa wa kucheza na teknolojia na unaweza ukataka kufahamu mahala nilikoenda lakini nakuomba usifanye hivyo.Kuwa na imani nami

kwamba nitarejea” akasema Mathew

“Sintafanya kitu ambacho umenikataza kukifanya Mathew”akasema Ruby

“Good” akasema Mathew na ukimya ukatawala

“Natamani sana nijue kile kinachoendelea katika maisha ya Mathew lakini ninashindwa namna ya kumshawishi akanieleza.Hakuna anayefahamu alikuwa wapi.Ameibuka kutoka kusiko julikana na hataki kusema chochote.Ngoja niendelee kuwa mvumilivu kama

alivyonitaka yawezekana siku moja akanieleza kile kinachoendelea katika maisha yake” akawaza Ruby

“Mungu akinisaidia operesheni hii ikamalizaka salama nitarejea tena kwa Habiba Jawad nikafahamu ni kitu gani alinitaka nirejee nikafanye na nitakapokamilisha lazima nirejee nyumbani kwa ajili ya Ruby” akawaza Mathew

Waliwasili hospitali na kumfuata Austin katika chumba ambacho alikuwa amelazwa akiandaliwa kwa

ajili ya kufanyiwa upasuaji ili kutolewa kipande cha ini cha kumpandikiza Gosu Gosu.Mathew akamsimulia kile walichofanikiwa kukipata walikoenda kumfuatilia Dr Sebastian

“Hawa watu lazima watarejea tena kutaka kummaliza Gosu Gosu na hawatakata tamaa mpaka wahakikishe Gosu Gosu amekufa” akasema Austin

“Lazima kuna jambo ambalo Gosu Gosu analifahamu kuhusu hawa jamaa na wanaogopa

akifumbua macho anaweza akalisema ndiyo maana wanataka kumuua.Ninahisi anaweza kuwa amegundua kitu kuhusu Mel……..” akasema Mathew na kunyamaza baada wauguzi watatu kuingia mle ndani na kuwataka akina Mathew watoke kwani mgonjwa alikuwa anapelekwa kufanyiwa uchunguzi zaidi.Wakaagana naye na kumuahidi kwamba wataendelea kuwepo pale hospitali kufuatilia kila kinachoendelea.Walikwenda kukaa nje ya wodi ya wagonjwa

mahututi alimokuwa amelazwa Gosu Gosu.

“Natamani Gosu Gosu aamke sasa na aseme hata maneno mawili tu kutufumbulia fumbo hili”akasema Ruby

“Ruby usihofu hatujawahi kushindwa katika operesheni yoyote tuliyowahi kuwa pamoja na hata misheni hii pia tutaimaliza.Niamini” akasema Mathew.Waliendelea kukaa pale nje wakiwa kimya kila mmoja akiwaza lake.

Wakiwa pale nje mara akatoka Dr Masawe na alipomuona Mathew akamuita

“Sikujua kama uko hapa” akasema Dr Masawe

“Vipi maendeleo ya mgonjwa wetu?akauliza Mathew

“Mgonjwa maendeleo yake siwezi kusema ni mabaya sana wala mazuri.Ni hamsini kwa hamsini.Bado tunaendelea kufuatilia kwa karibu sana maendeleo yake.Austin anaendelea kufanyiwa vipimo ili tuone kama anaweza akafaa kumpa mgonjwa ini.Naomba

msiwe na wasiwasi tunafanya kila jitihada kuokoa maisha ya Gosu Gosu na endapo ikitokea akapoteza maisha basi ni mapenzi ya Mungu lakini sisi kwa upande wetu tunaweka nguvu kubwa sana katika kuhakikisha mgonjwa anapona.Kuhusu suala la Dr Sebastian tayari liko kwenye vyombo vya dola vinalishughulikia na lazima atapatikana.Alichokifanya ni kitu kib……..” Dr Masawe akanyamaza baada ya mwanamke aliyekuwa akipita mbele yao kujikuta akiangusha

mkoba aliokuwa ameushika mkononi kwa mstuko alioupata.Mathew akageuka kumtazama mwanamke Yule naye akastuka

“Kisa ! akasema Mathew kwa mshangao akimtazama mwanamke Yule aliyekuwa amesimama karibu yao huku akionekana kuwa katika mstuko mkubwa na mwili ukimtetemeka

“Mathew ! Ni wewe kweli au nimekufananisha? Akauliza Yule mwanamama kwa uoga

“Hujanifananisha Kisa.Ni mimi Mathew Mulumbi” akasema Mathew

“No that’s not true.Mathew is dead.Samahani” akasema Yule mwanamama huku akiinama aokote mkoba wake Mathew akamshika bega.

“Kisa ni mimi Mathew Mulumbi.I’m not dead” akasema Mathew.Taratibu na woga mkubwa Yule mwanamama akapiga magoti akakaa chini na kuanza kulia

“Kisa tafadhali usipige kelele eneo hili.Inuka

tafadhali” akasema Mathew lakini bado Kisa aliendelea kumwaga machozi.Mathew akatumia nguvu akamuinua na kumtoa eneo lile akampeleka katika kiunga kilichokuwa na majani mazuri

“Kisa tafadhali naomba unisikilize ! akasema Mathew

“Mathew niambie tafadhali kama kweli ni wewe”

“Ni mimi usihofu”

“Jamani nini hiki knaendelea?! Akasema Kisa na kuinua kichwa akamtazama Mathew

“Ni mimi Kisa usiwe na wasi wasi.Inuka tafadhali twende kule mgahawani tukazungumze” akasema Mathew na kumsaidia Kisa kunyanyuka akashika viatu mkononi wakaelekea katika hoteli iliyoko pale hospitali

“Ujio wangu huu unaweza ukasababisha mtu kufa kwa mstuko.Karibu watu wote wanajua kwamba nimefariki dunia ndiyo maana kila anayeniona anastuka sana na wengine wakitaka kukimbia wakidhani mimi ni mzimu” akawaza Mathew akitazamana

na Kisa aliyekuwa bado akimtazama Mathew kwa woga.

“Kisa naomba uvute pumzi ndefu tafadhali” akasema Mathew na Kisa akavuta pumzi ndefu

“Pole sana Kisa kwa mstuko ulioupata”

“Naomba unihakikishie kama kweli ni wewe Mathew” akasema Kisa

“Kisa ni mimi usiogope.Ni mimi Mathew Mulumbi unayemfahamu na si mzimu” akasema Mathew na Kisa akamwaga tena machozi.

“Tuliambiwa umefariki dunia” akasema Kisa akiendelea kulia.

“Nyamaza Kisa usilie tena.Mimi sijafa niko hai kama unavyoniona” akasema Mathew

“Tumelia sana Mathew.Tumekulilia mno jamani kwa nini Mathew?Nini kilitokea?akauliza Kisa na kuanza tena kulia

“Kisa imetosha.Usilie tena” akasema Mathew

“Niache nilie Mathew.Machozi haya ni furaha ya kukuona

tena.Sikutegemea kabisa.Bado naona kama niko njozini” akasema Kisa

“Hii si njozi Kisa.Ni kitu cha kweli kabisa.Ni mimi halisi” akasema Mathew

“Siamini.Haya ni maajabu makubwa” akasema Kisa akifuta machozi

“Sijui hata nianzie wapi Mathew.Nahisi kuchanganyikiwa”

“Pole sana Kisa.Vipi maendeleo yako?akauliza Mathew

“Ninaendelea vizuri Mathew.Mimi na wote kazini

tunaendelea vyema kabisa.Nini kilikutokea Mathew?Ulikuwa wapi?Kwa nini wakakuzushia umefariki dunia? Akauliza Kisa

“Kisa naamini una maswali mengi sana unataka kuniuliza lakini hapa si mahala pake.Nitatafuta nafasi tutakutana tutazungumza mengi sana kuhusiana na mimi nini kilinitoea hadi watu wakanizushia nimekufa” akasema Mathew

“Ni kweli Mathew.Nilikuwa nimekuja hapa kufuatilia maendeleo ya

Gosu Gosu.Toka alipopatwa na matatizo sikuwa nimekuja kumtazama.Nilikuwa na vikao vingi leo lakini kuna kitu kilikuwa kinanisukuma kuja hospitali kumbe ninakuja kukutana na muujiza huu mkubwa.Naamini hata wewe pia uko hapa kwa sababu yake" akasema Kisa

"Ndiyo niko hapa kufuatilia hali ya Gosu Gosu.Alikuwa anaendelea vizuri na aliweza kufumbua macho lakini kuna mtu alifika na kumchoma sindano ya sumu kwa lengo la

kumuua.Madaktari wamejitahidi sana kuokoa maisha yake na kwa sasa kinachoendelea anahitajika kupandikizwa ini ambalo limeharibika kutokana na sumu hiyo kali”

“Mungu wangu !! akasema Kisa

“Ndiyo hali inayoendelea sasa” akasema Mathew

“Mungu amsaidie aweze kupona” akasema Kisa akiwa ameiweka mikono kifuani

“Kwa hali aliyonayo tunahitaji kumuombea sana kwani lolote linaweza kutokea

lakini Mungu wetu ni mwema atamsaidia” akasema Mathew

“Gosu Gosu jamani nani lakini wanaotaka kumuua?Ni mtu mzuri sana hana tatizo na mtu.Hajawahi kugombana na mtu yeyote.Kazini kila mtu anampenda.Toka ilipokuja taarifa umefariki yeye ndiye ambaye amekuwa akisimamia biashara zote na hakuna aliyetegemea kama angeweza kusimamia kwa ufanisi namna ile lakini amefanya maajabu kila mtu akabaki anashangaa.Makampuni yako yote yamefanya vizuri na

kuendelea kustawi hadi tulipostuliwa na taarifa kwamba yameuzwa.Tulistushwa sana na maamuzi yale ya kuamua kuuza mali zako” akasema Kisa

“Nani ameuziwa makampuni yangu?akauliza Mathew na Kisa akaonekana kushangaa

“Ina maana hufahamu nani aliyenunua makampuni yako?

“Hapana sifahamu chochote”

“Mathew ni kweli hufahamu chochote kuhusiana na suala hili?akauliza Kisa

“Suala hili nimelikuta hapa hapa Dar es salaam.Sifahamu chochote” akasema

“Haya mbona maajabu ! akasema Kisa

“Tumetambulishwa mwanamke mmoja bilionea anaitwa Melanie Davis kuwa ndiye mmiliki mpya wa makampuni yako.Lakini kuna kampuni kama mbili hivi ambazo ziko bado chini ya Gosu Gosu” akasema Kisa

Mathew alistuka baada ya kusikia jina Melanie Davis likitajwa

“Umesema Melanie Davis?

“Ndiyo unamfahamu?

“Hapana simfahamu.Ametokea wapi?Ni mtanzania?Mathew akauliza

“Hakuna anayemfahamu vizuri huyo mmiliki mpya lakini inasemwa kwamba ni raia wa Ufaransa ila anazungumza kiswahili vizuri kabisa.Kwa ujumla kama nilivyosema bado hatumfahamu vizuri.Hajajiweka wazi kwetu

tumfahamu.Ni Gosu Gosu pekee ambaye yuko naye karibu sana na ndiye anayemfahamu vyema kwani alisafiri kwenda Ufaransa na aliporejea alikuja na huyo mwanamke akatutangazia kwamba ndiye mmiliki mpya” akasema Kisa

“Dah ! akasema Mathew

“Mpaka leo hatufahamu hata ofisi yake iko wapi kwani kila kitu ameendelea kushughulikia Gosu Gosu kama ilivyokuwa awali” akasema Kisa

“Unafahamu anakoishi huyo Melanie Davis?akauliza Mathew

“Hakuna anayejua.Kuna mambo yanafumbwa fumbwa sana hapa na ambaye anafahamu kila kitu ni Gosu Gosu pekee.Yeye ndiye anayeweza kuwa na majibu yote kuhusiana na huyo Melanie Davis”

“Basi usijali Kisa ninyi endeleeni na kazi kama kawaida nitalifuatilia suala hili kwa undani zaidi kujua nini hasa kilitokea hadi yakafanyika maamuzi haya ya

kuuza kampuni zangu.Tuachane na hayo wengine wote hawajambo?

“Wote wazima lakini tumempoteza mzee Msimbo na Julitha walipata ajali ya gari mwaka jana”

“Poleni sana”

“Sipati picha wafanyakazi watakapopata taarifa za kuwa uko hai.Itakuwa ni mshangao mkubwa sana lakini kila mmoja atashangilia.Mathew tulilia sana tulipopata taarifa za kifo chako kwa sababu wewe umetufanya tuishi kama familia moja.Umemfanya kila

mtu afanye kazi kwa bidii na kujituma.Umetufanyia mambo mengi makubwa ambayo siwezi kuyaeleza ndiyo maana nasema kwamba taarifa za kuwa upo hai zikiwafikia itakuwa ni shangwe kubwa sana na wengi hawataamini na wengine wanaweza wakapoteza hata fahamu kwa mstuko" akasema Kisa

"Kisa kuna kitu kimoja ambacho nataka tukubaliane"

"Kitu gani Mathew?

"Sitaki upeleke taarifa hizi wamba niko hai.Muda

utakapofika mimi mwenyewe nitakuja kuwatembelea lakini kwa sasa sitaki mtu mwingine yeyote afahamu labda kama ikitokea tukakutana kama tulivyokutana mimi nawe”

“Kwa nini Mathew hutaki wajue kuwa uko hai?

“Nina sababu zangu.Naomba unisaidie kwa hilo”

“Lakini wanakuja sana hapa hospitali kumjulia hali Gosu Gosu ipo hatari wakakukuta hapa”

“Ikitokea hivyo sawa lakini usiwaeleze chochote.Umenielewa Kisa?

“Nimekuelewa Mathew”

“Ahsante sana” akasema Mathew

“By the way unamfahamu mchumba wa Gosu Gosu? Akauliza Mathew

“Mchumba wa Gosu Gosu? Kisa akashangaa kidogo

“Ndiyo”

“Hapana simfahamu.Gosu Gosu ana mchumba?Anataka kuoa?akauliza Kisa

“Ndiyo.Nimeambiwa ana mchumba lakini sijamuona

akifika hapa hospitali kujua maendeleo ya mchumba wake” akasema Mathew

“Huyo atakuwa si mchumba lazima atakuwa ni mwanamke wa kupotezea wakati.Kama angekuwa kweli ni mchumba wake angekesha hapa hospitali akifuatilia maendeleo ya mchumba wake.Huyo lengo lake lilikuwa ni kumchuna pesa na alipoona Gosu Gosu amepata matatizo haya akaamini hawezi kupona akatokomea zake” akasema Kisa

Waliendelea na mazungumzo kidogo halafu Mathew akasema

“Kisa imekuwa vizuri nimekutana nawe umenijulisha mambo mengi ambayo sikuwa nikiyafahamu.Kwa kuwa tumekutana mahala hapa kwenye matatizo nakuahidi kutafuta tena nafasi nyingine nzuri tukae tuzungumze.Kuna mengi nataka kuyafahamu kutoka kwako”

“Mathew hata mimi nimefurahi mno kwa kuiona sura yako tena.Naamini leo

sintapata usingizi nikiwaza juu ya jambo hili” akasema Kisa na Mathew akasimama

“Natakiwa kwenda kufuatilia kwa karibu kinachoendelea kuhusu zoezi la kumpandikiza Gosu Gosu ini.Endapo mtu aliyejitolea kumpa ini Gosu Gosu vipimo vitaonyesha kwamba hawaendani basi tutakuja kuomba msaada kwa wafanyakazi kwani Gosu Gosu ana saa 48 tu kwa mujibu wa daktari kama asipopandikizwa ini katika muda huo atakufa”

“Mathew endapo itatokea hivyo nijulishe haraka sana na mimi nitazungumza na wafanyakazi.Nitawashawishi wajitokeze kuokoa maisha ya Gosu Gosu.Namba yako ya simu ni ile ile?akauliza Kisa na Mathew akacheka kidogo

“Sikuwepo kwa miaka mitatu nimekuta kuna mabadiliko mengi yametokea hivyo nitahitaji kupata laini mpya ya simu.Nipatie namba zako tafadhali” akasema Mathew na Kisa akampatia kadi yake ya biashara kisha wakaondoka kurejea kule

wodini ambako walimkuta Ruby

“Ruby huyu anaitwa Kisa Mwakalukwa ni mhasibu mkuu wa yaliyokuwa makampuni yangu,amefika hapa kujua maendeleo ya Gosu Gosu na kwa bahati nzuri tukakutana.Kisa huyu ni rafiki yangu anaitwa Ruby” Mathew akafanya utambulisho Ruby na Kisa wakasalimiana wakazungumza kidogo kisha Mathew akamtaka Kisa akaendelee na shughuli zake na endapo kutatokea kitu

chochote atamjulisha.Kisa akaaga na kuondoka.

“Ruby tutafute sehemu tukakae kuna watu wanakuja kumtazama Gosu Gosu ambao wanaweza kunikuta hapa na yakatokea kama yale ya Kisa” akasema Mathew

“Mathew hili suala la wewe kuonekana hai linawastua watu wengi ndiyo maana kila anayekuona anastuka mno.Wewe ni mtu mwenye roho nzuri kwa watu ndiyo maana wengi walikulilia walipopata taarifa za kifo chako na wanapokuja kukuona

ukiwa hai wengi wanaamini labda wewe si Mathew halisi ni mzuka” akasema Ruby

“Wewe unaamini nini?Mimi ni halisi au mzuka?akauliza Mathew

“Mzuka hauwezi kuwa na nguvu kitandani kiasi kile”Akasema Ruby na wote wakacheka.

Mathew alimtaka Jerry awajulishe kila kitakachokuwa kinaendelea wakaenda kukaa mbali kidogo na wodi ile ya wagonjwa mahututi

“Kuna jambo lingine nimelipata kutoka kwa Kisa” akasema Mathew

“Ni kweli mali zangu zimeuzwa na mtu aliyenunua mali hizo ni bilionea Melanie Davis”akasema Mathew

“Melanie Davis again?akauliza Ruby kwa mshangao

“Ndiyo”

“Mhh ! hili jambo mbona linazidi kujichanganya ! akasema Ruby

“Nilistuka sana aliponitajia jina hilo lakini sikutaka

agundue chochote”akasema Mathew na ukimya ukapita

“Kwa mujibu wa Kisa” Mathew akaendelea

“Gosu Gosu alisafiri kwenda Ufaransa na aliporejea ndipo alipowatangazia wafanyakazi wote kwamba makampuni yameuzwa na akamtambulisha mmiliki mpya ambaye ni Melanie Davis.Kisa anadai kwamba mpaka sasa hakuna anayemfahamu kiundani Melanie.Hakuna anayejua ametokea wapi anaishi wapi ni Gosu Gosu pekee.Nadhani hiki

kilichomtokea Gosu Gosu kutaka kuuawa kina mahusiano na Melanie Davis.Kuna mambo ambayo nadhani Gosu Gosu ameyafahamu kuhusu yeye na ndiyo maana anatakiwa auawe” akasema Mathew na kushika kichwa akawaza kidogo halafu akasema

“Kama Gosu Gosu alikwenda Ufaransa na aliporejea ndipo alipoanza kuonekana akiwa na Melanie Davis basi mambo yote ya mauziano yalifanyika huko kwa Peniela na ndiyo maana

alimuita Gosu Gosu kwani ndiye aliyekuwa akifahamu biashara zangu nyingi.Naamini Peniela atakuwa akimfahamu vyema huyu Melanie Davis.Oh God ! I didn't want this to happen.Sikutaka Peniela ajue kama niko hai ! akasema Mathew na kushika kichwa

"You want to call her?Ruby akauliza

"Gosu Gosu ambaye anaweza kutupa taarifa za Melanie hali yake ndiyo hii.Hawezi kutusaidia chochote kwa sasa.Peniela pekee ndiye anayeweza kutupa

taarifa za kumuhusu Melanie Davis kwani ndiye aliyenunua makampuni yangu.Hakuna namna lazima nimpigie simu Peniela nizungumze naye kuhusu suala hili na nimuombe anieleze kwa undani kuhusu Melanie Davis.Lazima atakuwa na taarifa zake za kutosha” akasema Mathew akafikiri kidogo kisha akasema

“Twende tuondoke hapa”

“Tunaelekea wapi?

“Nyumbani”

akajibuMathew kisha

wakaenda kumuaga Jerry wakaondoka

“Tunakwenda kufanya nini nyumbani?Ruby akauliza

“Kuna jambo nataka tukalifanye” akajibu Mathew

****

Walifika nyumbani kwa Mathew ambaye moja kwa moja akaelekea chumbani kwa GosuGosu akaanza kupekua katika kabati na kuipata hati ya kusafiria ya Gosu Gosu akaichukua wakaelekea ofisini

“Nataka kujua tarehe ambayo Gosu Gosu alirejea kutoka Paris Ufaransa kisha tujue kama Melanie Davis naye aliingia nchini siku hiyo hiyo” akasema Mathew na kumpa Ruby tarehe ambayo Gosu Gosu alirejea nchini akitokea Paris Ufaransa na Ruby akaanza kuifanyia kazi.Baada ya dakika kadhaa akasema

“Gosu Gosu alirejea nchini siku hiyo akitumia ndege ya shirika la ndege la Ufaransa ikipitia Nairobi Kenya.Melanie Davis pia alikuwemo katika

ndege hiyo naye akitokea Ufaransa”

“Kama wote waliingia nchini siku moja na walikuwa katika ndege moja ina maanisha kwamba walikutana nchini Ufaransa hivyo basi mtu ambaye anaweza akatusaidia kumfahamu Melanie ni Peniela” akasema Mathew na kuinamisha kichwa akavuta pumzi ndefu

“Hakuna ujanja lazima nimtafute Peniela” akasema Mathew na kuchukua kitabu ambacho aliandika namba za

simu za watu wengi akaitafuta namba ya Peniela

“Sina hakika kama atakuwa bado anatumia namba hii ya simu ngoja nijaribishe” akasema Mathew na kuziandika namba zile katika simu yake akapiga simu ikaanza kuita

“Simu inaita” akamwambia Ruby.Baada ya muda ikapokelewa

“Hallow hapa ni nyumbani kwa Peniela,nikusaidie nini tafadhali?ikauliza sauti ya mwanamke

“Ninaomba kuzungumza na Peniela tafadhali”

“Nimwambie nani anapiga simu?

“Mwambie kuna taarifa muhimu kutoka Tanzania” akasema Mathew

“Sawa naomba usubiri kidogo” akasema Yule mwanamama na Mathew akaendelea kusubiri.Baada ya dakika chache akasikia sauti ambayo ilimfanya asite kuitikia

“Hallow! Ikasema sauti ambayo aliitambua ilikuwa ya Peniela

“Hallow habari yako.Nani mwenzangu?akauliza Peniela

“Hallo Penny ! akasema Mathew na ukimya ukatanda

“Penny ! akaita Mathew

“Wewe ni nani?akauliza Peniela

“Umeshindwa kuitambua sauti hii? Mathew akauliza

“Niambie tafadhali wewe ni nani ama sivyo nitakata simu .Sipendi kuchezewa ! akasema Peniela kwa ukali

“Ni mimi Mathew Mulumbi” akasema Mathew na simu ikakatwa

“Amekata simu ! akasema Mathew

“Haamini kama kweli ni wewe ndiyo maana amekata simu.Mpigie tena” akasema Ruby na Mathew akapiga tena lakini simu haikupokelea.

“Ngoja nijaribu kutumia mtandao wa skype akiniona ataamini” akasema Mathew na kuchukua kompyuta yake akampigia Peniela kwa kutumia mtandao wa Skype.Simu ikaita na kupokelewa.Macho ya Peniela yalijaa machozi

“Tafadhali wewe unayetumia sura ya Mathew shindwa ! akasema kwa ukali Peniela

“Peniela tafadhali naomba unisikilize ! akasema Mathew

“Nimekwambia shindwa ! Rudi huko huko kaburini ulikotoka.Muache Mathew apumzike kwa amani ! akasema Peniela

“Peniela mimi si mzimu wala mchawi.Mimi ni Mathew Mulumbi mume wako !

“Mume wangu amekwisha fariki miaka mitatu iliyopita.Tafadhali naomba

uniondokee mchawi mkubwa wewe unayediriki kuvaa sura za watu” akasema Peniela

“Peniela naomba unisikilize.Nipe dakika chache tu kuna kitu ninataka kuzungumza nawe” akasema Mathew lakini Peniela hakujibu kitu aliendelea kulia

“Peniela kwanza nataka ufahamu mimi sijafa.Mimi ni mzima japo iliaminika kwamba nimefariki dunia.Si wewe tu uliyeamini hivyo bali kila mtu alijua kwamba nimekufa.Mimi ni mzima kabisa na ni Mathew Yule yule

mume wako unayemfahamu” akasema Mathew

“Nitazame vizuri Penny ni mimi Yule Yule nimerudi” akasema Mathew

“Haya mbona mauza uza ! akasema Peniela

“Si mauza uza Penny ni kweli nimerejea”

“Ee Mungu naomba unipe nguvu.Hili jambo limenizidi uwezo wa kulibeba” akasema Peniela na kuinamisha kichwa

“Peniela najua nimekustua sana lakini naom.....” Akasema Mathew na Peniela akamkatisha

“Whoever you are please I can’t talk right now ! akasema Peniela na kukata simu

“Amekata simu.Ndiyo maana sikutaka kuzungumza naye.Nilijua angepatwa na mstuko mkubwa sana” akasema Mathew

“Mpigie tena simu.Suala hili ni muhimu zaidi kuliko mstuko wake.Akipokea nenda moja kwa moja kumuuliza kuhusu suala hili la Melanie ambalo ndilo limekusababisha ukampigia simu masuala ya kifamilia huu si wakati wake”

akasema Ruby na Mathew akapiga tena simu ikapokelewa

“Wewe ndugu nimekwishakwambia niache usinisumbue.Unan……”

“Peniela kuna kitu nataka kujua.Nimekuta mali zangu nyingi hapa Dar es salaam zimeuzwa ninataka kujua je ni wewe uliyefanya jambo hili? Ni wewe uliyeuza? akauliza Mathew na Peniela akaonekana kustuka.

“Mali ?akauliza

“Ndiyo.Naamini sasa umekwisha anza kuamini kwamba mimi si mzimu bali ni

Mathew halisi.Nimekuta mali zangu nyingi zimeuzwa lakini sifahamu nani ameuza na kwa nini.Sina wa kumuuliza kwani Gosu Gosu amepigwa risasi yuko hospitali ndiyo maana nikaona nikupigie nikuulize jambo hili”

“Oh mon Dieu” akasema Peniela kwa lugha ya kifaransa akimaanisha oh Mungu wangu kisha akafunika uso kwa kiganja chake cha mkono

“Peniela tafadhali nahitaji sana kujua kuhusu jambo hili !

“Hivi ni wewe kweli Mathew?akauliza Peniela

“Ni mimi Peniela usihofu” akajibu Mathew

“Ni ngumu kuamini”

“Peniela tutazungumza mengi hapo baadae lakini naomba kwanza unipe jibu kuhusiana na hicho nilichokuuliza” akasema Mathew na Peniela hakumjibu kitu akakata simu.

“Amekata simu” akasema Mathew

“Tumekwama”

“Kuna kitu kimoja ambacho nalazimika kukifanya”

“Kitu gani?

“Natakiwa kwenda Paris Ufaransa”

“Paris?! Ruby akashangaa

“Ndiyo.Natakiwa kwenda Paris Ufaransa haraka sana kuonana na Peniela.Amepatwa na mstuko mkubwa na kama nisipomuwahi anaweza akaharibu mambo kwa kuzungumza na Melanie kwamba niko hai na ninaulizia mali zangu”

“Mathew kwa wakati huu haitakuwa rahisi kwani kuna mambo mazito yanayoendelea.Khalid Khalid na James Kasai wanawasili

nchini na tunakutegemea sana wewe katika zoezi hili.Ninakushauri usiende Paris bali mpigie simu tena Peniela na umtake aje Tanzania mzungumze na atakueleza kila kitu" akasema Ruby na Mathew akafikiri kisogo na kusema

"Ushauri mzuri sana" akasema Mathew na kumpigia tena simu Peniela.

"Jamani ninakuomba kakaangu usinisumbue tena kwa kunipigia simu"

"Peniela naomba unisikilize.Nakuhitaji uje

Tanzania nizungumze nawe.Ningeweza kuja Paris lakini sitaki kuleta mstuko kwa watoto.Nakuomba tafadhali uje Tanzania kama utaweza siku ya kesho nataka sana kuzungumza nawe.One more thing usimweleze mtu yeyote kuhusu mimi hasa watoto.Tafadhali Peniela nakuomba sana uje Tanzania kesho" akasema Mathew na kukata simu

"Amesemaje?Ruby akauliza

"Sikutaka kumpa nafasi ya kujibu chochote.Ninamfahamu

Peniela naamini atakuja”akasema Mathew na ukimya mfupi ukapita

“Ruby tupumzike kidogo kabla ya baadae kurejea tena hospitali kujua kile kinachoendelea huo” akasema Mathew

****

Saa tano za usiku geti la nyumba moja iliyozungukwa na migomba mingi likafunguliwa na gari mbili zikaingia ndani ya jumba lile.Lango la gereji

likafunguliwa gari moja ikapitiliza hadi ndani ya gereji

“Tumefika mahala tutakapopumzika kwa usiku wa leo kabla ya kueleka Dar es salaam hapo kesho” akasema Edwin Mbeko huku akifungua mkanda na kushuka akwafungulia wageni wake milango wakashuka.Kwa kutumia mlango mdogo uliokuwemo ndani ya gereji wakaingia ndani ya ile nyumba wakaenda sebuileni.

“Karibu sana” akasema Edwin

“Edwin tunashukuru sana kwa kazi kubwa uliyoifanya” akasema mmoja wa wale wageni wawili

“Usijali madam Melanie.Ni jukumu langu kuhakikisha unakuwa salama muda wote” akasema Edwin na kwenda kuleta chupa kadhaa za mvinyo akaziweka mezani akawakaribisha akina Melanie waendelee kunywa

Edwin Mbeko alikuwa ametoka kuwapokea Melanie na James Kasai na kuwapeleka katika nyumba moja mjini Bukoba kwa mapumziko ya

usiku ule kabla ya kuelekea Dar es salaam siku inayofuata.

“Sikuwepo Tanzania kwa siku kadhaa.Mambo yanakwendaje hapa?akauliza Melanie

“Mambo yanakwenda vizuri.Hakuna wasiwasi wowote”akajibu Edwin

“Juhudi za kumsaka James Kasai zimefikia wapi?akauliza Melanie huku akitoa kicheko kidogo na kumtazama James ambaye naye alitabasamu

“Kikosi cha umoja kinaendelea na mazoezi kabla

ya kuelekea Uganda muda wowote kitakapoamriwa kufanya hivyo.Kwa idara nyingine mpaka sasa hawajapata kitu chochote" akasema Edwin na James Kasai akatoa kicheko kidogo wakaendelea kunywa pombe .Baada ya muda chakula kikaletwa na kuwekwa mezani wote wakajumuika.

****

Mshale wa saa ulionyesha ni saa saba za usiku pale mlango wa chumba cha

upasuaji ulipofunguliwa na vitanda kutolewa vikisukumwa kuelekea wodini.Upasuaji wa kumpandikiza ini Gosu Gosu ulikuwa umemalizika.Saa mbili za usiku ndipo upasuaji ule uliochukua saa tano ulioanza.Mathew na Ruby walikuwepo hospitali wakisubiri upasuaji ule umalizike na muda mfupi baada ya upasuaji kumalizika Dr Masawe akatoka na kuwaita akina Mathew ofisini kwake akawajulisha kwamba upasuaji ulifanyika kwa mafanikio

makubwa akawataka wasiwe na wasiwasi tena.

Akina Mathew waliondoka hospitali na kurejea nyumbani kwa Mathew ilipata saa nane za usiku.Wakati Ruby akioga Mathew akaenda ofisini kwake akachukua kompyuta yake na kumpigia Habiba Jawad.

“Mathew Mulumbi.Inakaribia saa tisa za usiku sasa lakini bado sijapata usingizi hata kidogo.Nimekuwa na hofu kubwa juu yako kwani umezoea kunipigia simu saa nne au saa tano.Nini

kimekutokea leo?Ulikuwa katika hatari yoyote?Habiba akauliza

“Samahani mama kwa kukupa wasiwasi lakini sikuwa katika hatari yoyote nilikuwa hospitali” akasema Mathew na kumsimulia Habiba kila kitu kuhusu Gosu Gosu.

“Poleni sana.Naamini mgonjwa wenu huyo atapona inshallah” akasema Habiba

“Mama nimekupigia kupata taarifa za kuhusiana na ujio wa Khalid Sultan ambaye uliniambia atawasili nchini hapo kesho” akasema Mathew

“Umepata chochote kuhusu James Kasai?akauliza Habiba

“Bado sijafahamu ataingia vipi nchini lakini kuna mtu ambaye ninamfuatilia na nikifanikiwa kumpata naamini nitakuwa nimempata James Kasai.Ulinituma Dubai kushuhudia yakisainiwa makubaliano ya fedha kati ya IS na James kasai na alikuwepo mwakilishi wa James Kasai ambaye anatokea Tanzania.Huyo mwanadada anaitwa Melanie Davis na ambaye ndiye nimeanza

kumtafuta.Naamini nikimpata huyo basi nitakuwa karibu sana kumpata James kasai” akasema Mathew

“Una akili sana Mathew.Nilikutuma Dubai kwa kusudi kabisa nikakwambia utulie ujifunze na sasa umeona faida zake.Sikutaka kukueleza chochote kuhusu Melanie Davis nilitaka nikuache nikupime nione utafanya nini lakini kumbe umefanya kile ambacho nilitegemea ukifanye.Melanie Davis ndiye kiungo kati ya James Kasai na

IS.Kama James anakuja Tanzania lazima atakutana naye hivyo hakikisha unampata.Kuhusu Khalid Sultan atawasili kesho saa moja za jioni na ndege ya shirika la ndege la Ethiopia.Picha zake unazo naamini mtajipanga vyema kumfuatilia kujua kilichomleta Tanzania lakini ufunguo wa hili fumbo ni Melanie Davis”akasema Habiba

“Mama kuna chochote unakifahamu kuhusu Melanie ambacho unadhani kinaweza

kunisaidia kufahamu mahala alipo?Mathew akauliza

“Mathew wewe ni mtu mahiri sana katika kazi hii.Hata kama ningekuwa nikifahamu nisingekueleza kwani nataka uumize kichwa ili uweze kugundua mambo mengine mengi.Mimi nitakueleza yale mambo makubwa tu na mengine ni juu yako kuyafanyia kazi.Umenielewa Mathew?

“Ndiyo nimekuelewa mama”

“Vizuri.Nakutakia kazi njema na kesho nipate

mrejesho wa nini kinaendelea.Kumbuka Khalid Khalid na James Kasai hawapaswi kutoka salama nchini Tanzania.Kumbuka vile vie hakuna kuwaua watu hawa wawili kabla kwanza ya kufahamu nini wanakipanga kukifanya”

“Nimekuelewa mama” akasema Mathew na kuagana na Habiba Mathew akashusha pumzi

“Mambo yameiva.Habiba naye anakiri kwamba Melanie Davis ndiye mwenye ufunguo wa fumbo hili.Wapi alipo huyu

mwanamke?Ngoja nitulize kwanza kichwa na kujiandaa kwa siku ya kesho” akawaza Mathew na mara mlango wa ofisi yake ukagongwa.Akaifunika komputa yake haraka haraka na kwenda kuufungua akakutana na Lucy mtumishi wake wa ndani

“Karibu Lucy”

“Kaka samahani kwa kukusumbua.Ruby ameniambia kwamba nije nikuone huku” akasema Lucy na kunyamaza kidogo

“Kuna jambo ninataka kukwambia.Nimepigiwa simu na madam Peniela pale ulipoondoka akaniuliza kama kweli umerejea nikamuhakikishia kweli ni wewe na umerejea.Alikuwa analia sana na akaniambia kwamba nisikueleze chochote.Nimeona nije nikwambie kaka suala hilo”

“Ahsante sana Lucy.Umefanya vyema kunieleza”

“Sawa kaka.Vipi hali ya Gosu Gosu?

“Tayari amekwisha fanyiwa upasuaji wa kupandikizwa ini na kwa mujibu wa madaktari ni kwamba kila kitu kilikwenda vizuri.Usiwe na wasi wasi kama kuna chochote kibaya nitakujulisha” akasema Mathew na kuagana na Lucy

“Kama Lucy amemuhakikishia Peniela kweli ni mimi nimerejea basi lazima atakuja Tanzania .Huyu ndiye atakayenipa ukweli wote kuhusiana na Melanie Davis” akawaza Mathew na kutoka akarejea chumbani

“Khalid Sultan ataingia nchini kesho saa moja za jioni na ndege ya shirika la ndege la Ethiopia” Mathew akamwambia Ruby

“Hizi taarifa Mathew anazipata wapi? Lazima kuna mtu anawasiliana naye ambaye ndiye anayempa taarifa hizi.Natamani kumchunguza kujua kinachoendelea lakini naogopa akijua nitaharibu kila kitu na mimi sitaki kumkorofisha huyu jamaa” akawaza Ruby

“Kuhusu Melanie Davis” Mathew akaendelea

“Naamini kesho tutapata kila kitu kuhusu yeye kwani nina uhakika mkubwa Peniela lazima atakuja.Alimpigia simu Lucy kupata uhakika kama kweli ni mimi niliyempigia simu”akasema Mathew

“Do you miss her?akauliza Ruby

“Not much” akajibu Mathew

“Ni mke wko wa ndoa nilidhani ungekuwa na hamu sana ya kutaka kumuona” akasema Ruby

“Nina hamu sana ya kutaka kuwaona watoto wangu”

“Kwa nini mama yao huna hamu ya kutaka kumuona?akauliza Ruby

“Ruby tusiongelee mambo hayo tafadhali” akasema Mathew

****

Saa kumi na mbili za asubuhi Mathew na Ruby walipofika hospitali tayari Austin alikwisha zinduka kutoka usingizini na alikuwa

anaendelea vizuri.Taarifa ya madaktari waliokuwa wanafuatilia hali ya Gosu Gosu toka alipotolewa chumba cha upasuaji ilionyesha alikuwa anaendelea vizuri.Saa moja za asubuhi wakalazimika kuondoka kurejea katika makazi yao ambako Ruby aliacha gari lake kwani alihitajika kwenda ofisini kwake asubuhi hiyo.Baada ya Ruby kuondoka kwenda kujiandaa Mathew naye akajiandaa halafu akaondoka kuelekea uwanja wa kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es

salaam.Alikuwa anamtafuta mtu mmoja aliyeitwa Salim Chongo.Huyu ni rafiki yake wa muda mrefu.Aliwahi kufanya kazi katika idara ya ujasusi kabla ya kuacha baada ya kupata kazi katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere katika idara ya usalama.Aliekekezwa ofisi mpya ya Salim na kuelekea huko.Aligonga mlango wa kioo na mwanadada aliyekuwamo ndani akamkaribisha ndani akaeleza shida yake ya kuonana na Salim akamuombwa asubiri kwani

Salim alikuwa katika kikao cha kazi ambacho kilikaribia kumalizika.

Ilipita saa moja na dakika ishirini ndipo kikao kilipomalizika na Salim akaingia mle ofisini.Alistuka alipomuona Mathew

“Mathew Mulumbi ! akasema Salim kwa mshangao

“Salim” akasema Mathew huu akisimama wakakumbatiana.

“Umepotelea wapi Mathew?Nina zaidi ya miaka mitatu hatujaonana”

“Nilikuwa nje ya nchi ndiyo maana hatujaonana” akasema Mathew na Salim akamkaribisha ofisini kwake

“Mathew nimefurahi sana nimekuona leo.Karibu sana” akasema Salim

“Salim ninashukuru sana lakini nimekuja nina shida ndugu yangu nahitaji msaada wako”

“Shida gani Mathew?

“Kuna kumbu kumbu ya kamera nataka kuipitia” akasema Mathew na Salim akatoa kicheko kidogo

“Mathew usiniambie mpaka sasa bado hujaacha ile kazi”akasema Salim

“Hapana sijaacha.Bado ninaendelea nayo”akajibu Mathew

“Mulumbi wewe ni mtu wa ajabu sana.Pamoja na utajiri wote huu ulio nao lakini bado unaendelea kufanya kazi hizi za hatari.Waachie vijana ili ule maisha.Uliyoyafanya yanatosha” akasema Salim.

“Kuna yale maandishi mgongoni kwangu uliwahi kuyasoma ukacheka sana

unayakumbuka?Mathew akauliza

“Kama sijasahau uliandika People sleep peaceably on their bed at night only because rough men stand ready to do violence on their behalf.Nadhani umeandika hivyo”

“Exactly.Kazi ile iko damuni na kamwe siwezi kuiacha” akasema Mathew

“Nini unahitaji nikusaidie Mathew?akauliza Salim.Mathew akachukua karatasi akaandika tarehe kisha akasema

“Ninataka kupitia kumbu kumbu za kamera kwa tarehe hiyo”

“Nini hasa unataka kukitazama Mathew?Salim akauliza

“Kuna mtu ninamfuatilia ambaye aliingia nchini tarehe hiyo akitokea Ufaransa kwa kutumia ndege ya shirika la ndege la Ufaransa kupitia Nairobi” akasema Mathew na Salim akatazama katika kompyuta yake akasema

“Ni kweli tarehe hiyo kulikuwa na ndege ya shirika la ndege la Ufaransa”

Salim akamtaka Mathew amfuate wakaingia katika mlango uliokuwemo mle chumbani wakaingia katika chumba chenye kompyuta runinga zaidi ya kumi kisha akaitafuta tarehe ile aliyoiandika Mathew na muda ambao ndege ile ya Ufaransa iliwasili nchini.Mathew akawatambua Gosu Gosu na Melanie ambao ni miongoni mwa abiria waliokuja na ndege ile

“Huyu mwanamke ndiye hasa nataka kufuatilia” akasema Mathew

Baada ya kukamilisha taratibu akaruhusiwa kuingia nchini Salim akabadili kamera na kuhamia katika kamera ya sehemu ya abiria wanaowasili.Melanie alionekana akiwa na Gosu Gosu halafu mwanamke mmoja akawasogelea akasalimiana na Melanie

“Simamisha hapo” akasema Mathew na kumtazama Yule mwanamke ambaye alimpokea Melanie uwanjani.Nataka kupata picha ya huyu mwanadada aliyempokea huyu mgeni”

akasema Mathew na Salim akamchapishia ile picha kisha wakaendelea kufuatilia katika kamera.Walihamia kamera nyingine ya kwenye maegesho ya magari na kuwaona wakiingia katika gari.Mathew akachukua namba za gari lile akamshukuru Salimu akamuaga na kuondoka.Baada ya kuingia katika gari lake akampigia simu Ruby

“Ruby vipi maendeleo yako?akauliza Mathew

“Ninaendelea vizuri na kazi.Vipi kuna habari yoyote mpya?akauliza Ruby

“Nimetoka kuonana na rafiki yangu mmoja wa muda mrefu anaitwa Salim anafanya kazi idara ya ulinzi uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere.Nimepitia kumbu kumbu za kamera za ulinzi zilizoko uwanjani pale siku waliyorudi Gosu Gosu na Melanie Davis.Nimemfuatilia Melanie alipokewa uwanjani na mwanadada mmoja ninakutumia picha yake sasa hivi ili umtafute ni nani” akasema Mathew na kumtumia Ruby ile picha ya Yule mwanamke aliyempokea

Ruby uwanja wa ndege.Akawasha gari na kuondoka.Baada ya dakika tano Ruby akampigia simu

“Anaitwa Felista Kabasa ni mfanya biashara anaishi mtaa wa Mwakisule nyumba 204”

“Ahsante Ruby ninaelekea huko sasa hivi” akasema Mathew

Mathew alifika mtaa wa Mwakisule kama alivyoelekezwa na Ruby akaitafuta nyumba 204 akashuka garini na kuelekea getini akabonyeza kengele ya mlangoni baada ya muda

mfupi akatokea mama mmoja mnene akamkaribisha Mathew kwa tabasamu

“Karibu sana kaka”

“Ahsante mama yangu”

“Nikusaidie nini?akauliza Yule mama

“Ninamtafuta dada mmoja anaitwa Felista Kabasa” akasema Mathew

“Felista?akauliza Yule mama

“Ndiyo” Mathew akajibu

“Hapana haishi hapa huyo dada” akasema Yule mama

“Nimeelekezwa anaishi hapa”

“Waliokuelekeza au kama ni yeye kakuelekeza amekudanganya kaka yangu.Haishi hapa huyo mtu.Humu ndani ninaishi mimi,mume wangu na watoto wetu wawili na wala hatuna mtoto anayeitwa Felista hata mtumishi wetu wa ndani hana jina hilo” akasema Yule mama

“Samahani sana yawezekana nimekosea lakini nimeelekezwa ni nyumba hii” akasema Mathew na kutoa picha akamuonyesha Yule mama

“Unamfahamu huyu dada?akauliza Mathew

“Hapana simfahamu na wala sijawahi kumuona mtaa huu” akasema Yule mama

“Una hakika hujawahi kumuona mtaa huu? akauliza Mathew

“Kwanini nikudanganye kaka yangu?Huyu dada sijawahi kumuona mtaa huu.Kaka yangu kuwa makini siku hizi wanawake wamekuwa wadanganyifu sana” akasema Yule mama

“Ahsante nakushukuru sana” akasema Mathew na

kurejea katika gari lake akaondoka.Akachukua simu na kumpigia Ruby

“Ruby nimetoka katika nyumba ile uliyonielekeza kwamba anaishi Felista nimekutana na mtu mwingine kabisa.Felista nimemkosa” akasema Mathew

“Lakini taarifa zake zinaonyesha anaishi hapo.Yawezekana labda alikuwa akiishi hapo lakini amehama.Ngoja niendelee kumchimba zaidi kama nitapata taarifa zake” akasema Ruby

Baada ya kutoka mtaa wa Mwakisule Mathew akarejea nyumbani kwake na moja kwa moja akamfuata Lucy akamuonyesha ile picha ya Yule mwanadada

“Melanie amekuwa akifika mara kwa mara hapa umewahi kumuona akiwa na huyu mwanamke?akauliza Mathew

“Huyu ni dereva wake anaitwa Joyce.Amekuwa akija naye hapa kila ajapo.Akiwa chumbani na Gosu Gosu Joyce hubaki sebuleni na mimi ndiye ninaye muhudumia” akasema Lucy

“Una hakika jina lake ni Joyce?

“Ndiyo.Jina lake ni Joyce na hata Melanie humuita hivyo Joyce”

“Amewahi kukueleza mahala anakoishi?akauliza Mathew

“Hapana hajawahi kunieleza.Hatujawahi kuzungumzia chochote kuhusu yeye” akasema Lucy

“Ahsante sana Lucy” akasema Mathew na kurejea katika gari lake akaondoka halafu akampigia simu Ruby

“Ruby nimetoka nyumbani sasa hivi nimeelezwa na Lucy kwamba huyu mwanamke ambaye umepata taarifa zake anaitwa Felista jina lake ni Joyce.Ni dereva wa Melanie”

“Joyce?akauliza Ruby kwa mshangao kidogo

“Ndiyo.Kwa mujibu wa Lucy hilo ndilo jina lake” akasema Mathew

“Mbona taarifa zake hazisemi hivyo?akauliza Ruby

“Nimegundua hawa watu wanatumia majina bandia.Mtandao huu wa Melanie ni mkubwa na

wamejipanga vyema.Wanajua wanachokifanya.Kwa sasa ninaelekea hospitali kujua maendeleo ya wagonjwa kwani kutokana na kazi tutakayokuwa nayo baadae yawezekana tusiweze tena kupata nafasi ya kwenda kuwaona wagonjwa” akasema Mathew

“Nami pia ninakuja hapo hospitali” akasema Ruby

****

Helkopta ya idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi

ikitokea Kagera ilitua katika sehemu ya kutulia ndani ya uwanja wa bohari la idara ambako huhifadhiwa vitu mbali mbali vya idara ya SNSA vile vile kuna karakana ya kutengeneza magari na vifaa mbali mbali vya idara.Edwin Mbeko alikwisha mpa maelekezo dereva wake ampelekee gari lake katika bohari na tayari gari lilikwisha fika.Helkopta ilipotua gari la Edwin Mbeko likaanza kusogea taratibu.Injini ilipozimwa gari la Edwin likasogezwa karibu zaidi na

helkopta mlango ukafunguliwa akashuka Edwin Mbeko akafuatiwa na James Kasai na Melanie na wote wakaingia katika gari la Edwin ambaye alimtaka dereva wake aingie katika helkopta wakutane ofisi kuu.Akashika usukani na kuondoka eneo lile.

“Karibuni Dar es salaam” akasema Edwin Mbeko.James Kasai hakuonekana kuwa na wasi wasi wowote

Kutoka bohari kuu la SNSA moja kwa moja walielekea nyumbani kwa Melanie.

“Karibuni ndani” Melanie akawakaribisha ndani Edwin na James

“Ahsante sana Melanie” akasema Edwin Mbeko lakini kabla hajaketi simu yake ikaita.

“Hallo” akasema Edwin

“Edwin unaongea na Annabel”

“Madam Annabel habari yako?

“Nzuri.Sijakuona ofisini na hakuna taarifa yoyote.Uko wapi?akauliza Annabel ambaye ni Ruby

“Ninakuja madam nilipata dharura nje ya mkoa.Tayari nimerejea na nitafika hapo ofisini muda si mrefu” akasema Edwin

“Sawa Edwin” akasema Ruby na kukata simu.

“Melanie tayari mmefika salama.Ninahitajika ofisini .Nilikwambia kwamba kuna mkurugenzi mpya ameletwa na Rais ndiye huyo ananihitaji.Nitawasiliana nawe tena baadae kwa ajili ya zoezi la kumpokea Khalid” akasema Edwin

“Edwin ahsante sana kwa kazi kubwa uliyoifanya ya kutufikisha salama Dar es salaam.Nakutegemea sana hapo baadae katika kuhakikisha Khalid anaingia nchini salama bila matatizo yoyote”akasema Melanie

“Jambo lingine Melanie suala la Gosu Gosu ni kama nilivyokueleza kwamba jaribio la kumuua hospitali lilishindikana hivyo basi hii ni taa nyekundu kwa watu wake wa karibu na kuwafanya waimarishe ulinzi na vile vile wanaweza wakaanza

kuchunguza nani wanaotaka kumuua Gosu Gosu.Wakati tunatafuta namna nyingine ya kumuua Gosu Gosu tafadhali usitumie zile simu zako zote bali tumia simu mpya niliyokupa na wala wala usiende hospitali.Naamini ndani ya siku mbili hizi tayari tutakuwa tumepata mpango mpya wa kumuua.Kama alivyosema Devotha huyu jamaa ana ukaribu na watu hatari ambao wanaweza wakaharibu mipango yetu hivyo kwa sasa jiweke mbali na

Gosu Gosu”akasema Edwin na kuondoka .

****

Ruby aliwasili hospitali na kukutana na Mathew ambaye alimpa taarifa za maendeleo ya Gosu Gosu na Austin.

“Mungu mkubwa.Naamini Gosu Gosu atapona tu” akasema Ruby

“Umechimba zaidi kupata taarifa za Yule mwanamke niliyekutumioa picha yake Joyce?akauliza Mathew

“Ndiyo lakini sijaona taarifa zake nyingine zaidi ya zile nilizokutumia.Nimeshangaa uliponiambia eti anaitwa Joyce” akasema Ruby

“Kwa mujibu wa Lucy ni kwamba yule mwanamke anaitwa Joyce na ni dereva wa Melanie.Kama nilivyokueleza simuni hawa watu wanaonekana wanatumia majina bandia.Sasa ninaanza kuamini lile wazo lako kwamba yawezekana kabisa Melanie Davis na Melanie Chuma akawa ni mtu

mmoja.Ruby huu ni mtandao mkubwa na una watu makini sana.Wanajua wanachokifanya na ndiyo maana hata fedha za kutoka IS zinapita kwao bila vyombo vya fedha kugundua.Kila aliyemo katika mtandao huu inakuwa vigumu sana kumfuatilia na kumpata” akasema Mathew na kumtazama Ruby

“Nadhani kwa sasa tujielekeze zaidi kwa Khalid Sultan ambaye atawasili nchini jioni ya leo kwa ajili ya kukutana na James Kasai.Tukimfuatilia Khalid

atatufikisha kwa James lakini kuna tatizo limejitokeza”akasema Mathew

“Tatizo gani Mathew?akauliza Ruby

“Kuna vijana ambao Austin aliwaandaa kwa ajili ya kutusaidia katika operesheni hii na nilitegemea jioni ya leo kuwa nao katika zoezi la kumfuatilia Khalid lakini wamenipigia simu wakati nikija hospitali na kunieleza kwamba wamepata safari ya kikazi kwenda Morogoro hivyo hawataweza kushiriki katika operesheni yetu hadi pale

watakaporejea”Mathew akanyamaza baada ya muda akaendelea

“Ninataka tuwashirikishe idara yako katika zoezi hili ili waweze kumfuatilia Khalid toka atakapoingia nchini hadi pale atakapokuwa amefikia.Pale SNSA mna kila kitu kinachohitajika katika zoezi hilo mnao watu na vifaa vya kutosha hivyo itakuwa vyema kama tukiwashirikisha kufuatilia Khalid lakini usiwaeleze kama anakuja nchini kukutana na James Kasai inaweza ikazua taharuki

kubwa.Ujio wa James Kasai itabaki ni siri yetu kwa sasa” akasema Mathew.

“Ni wazo zuri pia kwani tunao watu wa kutosha wenye mafunzo na ujuzi mkubwa pale SNSA”akasema Ruby

“Nataka zoezi zima la kumfuatilia Khalid litakalofanywa na idara yako liunganishwe katika ofisi yangu nami pia nifuatilie lakini asijue mtu yeyote kama ninafuatilia.Can you do that? akasema Mathew

“Nitakuwa pamoja nawe wakati wa kufuatilia zoezi

hilo.Utanipa maelekezo nini cha kufanya na mimi nitakuwa nikiwasiliana na timu itakayokuwa ikiendelea na zoezi hilo la kumfuatilia Khalid” akasema Ruby na kunyamaza baada ya simu ya Mathew kuita alikuwa ni Lucy

“Lucy” akasema Mathew

“Kaka Mathew samahani kwa usumbufu.Nimekupigia kukujulisha kwamba mama Peniela yuko hapa nyumbani amefika sasa hivi” akasema Lucy

“Peniela amekuja?! Akauliza Mathew akionyesha mshangao kidogo.

“Ndiyo amekuja muda si mrefu na amesema nikupigie simu kuwa anakuhitaji hapa nyumbani” akasema Lucy

“Sawa Lucy ninakuja hapo nyumbani muda si mrefu” akasema Mathew na kukata simu akashusha pumzi

“Mambo yameiva.Peniela amekuja” akasema Mathew

“Dah ! akasema Ruby

“Natakiwa nikaonane naye.Usiogope hakuna kitakachoharibika.Andaa timu

kwa ajili ya zoezi la jioni na unijulishe kila kinachoendelea”akasema Mathew

“Kama Peniela atakuwepo haitakuwa vyema mimi kuja nyumbani kwako jioni lakini nitakuunganisha na kila kinachoendelea” akasema Ruby

“Ruby lazima uje nyumbani na tutaongoza zoezi kutokea pale.Jambo hili ni muhimu mno” akasema Mathew na kuagana kila mmoja akaingia katika gari lake na kuondoka.

“Nilijua tu lazima Peniela atakuja.Nashukuru kwa ujio wake kwani utanisaidia kufahamu mambo mengi kuhusiana na Melanie Davis lakini hata hivyo liko tatizo.Lazima Peniela atataka kufahamu kilichokuwa kimenitokea.Nilikuwa wapi,kwa nini nikatangazwa nimekufa na mambo mengine kadha wa kadha.Nitafuata maelekezo ya Habiba sintamueleza mtu yeyote hata Peniela mahala nilikokuwa” akawaza Mathew akielekea nyumbani kwake

OFISI KUU SNSA

Ruby alirejea ofisini kwake na muda mchache baadae mlango wa ofisi yake ukagongwa akaingia Edwin Mbeko

“Habari yako madam Annabel” akasema Edwin kwa adabu

“Edwin ulikuwa wapi?Toka jana hujaonekana hapa ofisini na hakuna taarifa zozote za mahala ulikokuwa” akasema Ruby

“Madam kama nilivyokueleza uliponipiga simu kwamba nilikuwa nimekwenda nje ya mkoa kikazi” akasema Edwin

“Ninataka kupata orodha ya kila operesheni inayoendelea hivi sasa ndani ya SNSA na kila pale unapohitaji kwenda nje ya mkoa nijulishe tafadhali.Mimi hapa ni mgeni bado kuna mmbo mengi siyafahamu ninakutegemea sana wewe hivyo usipokuwepo inanipa ugumu katika kazi zangu” akasema Ruby

“Sawa madam nitakupa orodha ya operesheni zote zinzaoendelea na samahani sana kwa kilichotokea.Hakitajirudia tena” akasema Edwin kwa adabu.

“Nataka kuzungumza na wafanyakazi wote ndani ya dakika tano.Kuna zoezi ambalo linatakiwa kupewa uzito mkubwa” akasema Ruby

“Sawa madam” akajibu Edwin na kutoka kwenda kuwakujulisha wafanyakazi kwamba mkurugenzi atazungumza nao muda mfupi

ujao.Zilipita dakika tano kama alivyokuwa ameahidi Ruby akatoka ofisini kwake akaelekea katika ukumbi mkubwa.Edwin akawataka wafanyakazi wote kuacha kazi zao kumsikiliza mkurugenzi ambaye alianza kwa kuwasalimu halafu akageukia mbele kulikokuwa na runinga kubwa

“Nafahamu zipo operesheni mbali mbali ambazo mmekuwa mkiendelea nazo hapa ningependa kuzifahamu zote na tayari nimekwisha muelekeza Edwin

aniwekee mezani orodha ya operesheni zote zinazoendelea hivi sasa.Pamoja na kazi nzuri mnazoendelea nazo sasa hivi lakini kuna zoezi moja muhimu sana ambalo nataka wote tujielekeze huko kuanzia sasa” akasema Ruby akageukia runingani akabonyeza kitanza mbali picha kubwa ikatokea.

“Anaitwa Khalid Sultan Khalid” akasema Ruby na kunyamaza kidogo

“Anatokea Syria.Ni mmoja kati ya watu wa juu kabisa wa kundi la IS ambaye anahusika na milipuko mikubwa.Huyu

mtu anakuja nchini Tanzania” Ruby akanyamaza kidogo kisha akaendelea

“Ujio wake nchini Tanzania unatufanya tuamini kwamba IS wanapanga tena shambulio lingine kubwa hivyo ni jukumu letu kama idara yenye dhamana ya kuhakikisha nchi inakuwa salama kufanya kila lililo ndani ya uwezo wetu kuhakikisha hakuna tena shambulio lingine ambalo litatokea hapa nchini Tanzania” akasema Ruby na kunyamaza tena kidogo.

“Leo saa moja za jioni Khalid ataingia nchini na ndege ya shirika la ndege la Ethiopia akitokea Cairo Misri.Tutamfuatilia kuanzia atakaposhuka katika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere hadi atakapofikia.Tunatakiwa kufahamu kila anachokifanya hapa nchini,tumjue kila anayekutana naye.Khalid haji Tanzania kwa mapumziko tunaamini kuna kitu kikubwa kinachomleta hivyo basi zoezi hili ni muhimu mno.Edwin utapanga timu ya watu wetu kuanzia uwanja wa ndege wa

Julius Nyerere kwa ajili ya kumfuatilia Khalid kila mahala anakoenda hadi mahala atakapofikia.Naomba niwakumbushe kwamba hii ni operesheni muhimu mno hivyo tuwekeze nguvu kubwa na ujuzi wetu wote katika operesheni hii.Ninyi ni wazoefu katika mambo haya mmekwisha fanya operesheni mbali mbali na kwa mafanikio makubwa hivyo naamini hata katika zoezi hili litafanyika kwa ufanisi mkubwa sana.Mkumbuke pia kwamba IS wametekeleza shambulio

lingine baya sana hapa nchini siku chache zilizopita na bado machozi ya walichokifanya hayajakauka hivyo tusiwape nafasi hata ndogo ya kutekeleza tena shambulio lingine katika ardhi yetu ya Tanzania.Ni wakati wa kuung'oa mzizi wa IS hapa nchini na zoezi hilo litaanza usiku wa leo.Khalid atatuongoza kuweza kuwafahamu washirika wake hapa nchini" akasema Ruby na kuwatazama wafanyakazi wale waliokuwa kimya wakimsikiliza

“Mkumbuke pia kwamba IS wanashirikiana na James Kasai ambaye nchi zetu zinamsaka kwa udi na uvumba na nina uhakika kwa kumfuatlia Khalid tunaweza pia kupata taarifa za kumuhusu James Kasai.Narudia tena kuwasisitiza ndugu zangu kwa kiasi kikubwa sana usalama wa nchi unatutegemea sisi hivyo tukishindwa sisi tutakuwa tumewapa IS ushindi na nafasi ya kumwaga tena damu ya watanzania.Tusikubali tena damu yoyote ikamwagwa na

magaidi hawa.Tupambane kufa na kupona kwa ajili ya nchi yetu.Nadhani mmenielewa.Kuna yeyote mwenye swali kuhusiana na zoezi hili la jioni ya leo? Akauliza Ruby na kuwatazama wafanyakazi waliokuwa kimya wakimsikiliza.Hakuna aliyeuliza swali lolote.

“Hakuna swali naamini mmenielewa vizuri.Ahsanteni sana.Sasa tuanze maandalizi” akasema Ruby na kumtaka Edwin waelekee ofisini kwake.

“Edwin kama ulivyosikia kwamba mtu huyu anayekuja

Tanzania Khalid Sultan Khalid ni mtu hatari sana.Ni mtaalamu wa milipuko mikubwa na IS wamekuwa wakimtumia sana nchini Syria.Ninaamini kwamba ujio wake hapa Tanzania si bure lazima kuna jambo anakuja kulifanya.Lazima IS wanapanga kufanya shambulio lingine hapa nchini.Kama nilivyoeleza kwamba tutaanza kumfuatilia Khalid toka atakaposhuka ndegeni.Nataka upange vijana mahiri kabisa wenye ujuzi na uozefu wa kutosha katika kazi

wamfuatilie Khalid.Sitaki lifanyike kosa hata moja” akasema Ruby

“Sawa madam Annabel jambo hilo linakwenda kutekelezwa kwa ufanisi wa aina yake.Tunayo timu ya vijana mahiri wenye uwezo mkubwa ambao watafanya zoezi hilo.Hizi ni kazi zetu na tuna uzoefu mkubwa wa kuzitekeleza”

“Nitashukuru sana kama zoezi likienda vizuri” akasema Ruby

“Madam ninataka kufahamu kama taarifa hii ya

ujio wa huyo mtu imetoka katika chanzo cha kuaminika” akasema Edwin.Ruby akamtazama na kusema

“Taarifa imetoka katika chanzo kisichokuwa na shaka hata kidogo”

“Unaweza kunishirikisha nikajua chanzo cha taarifa hiyo? Akauliza Edwin

“Huniamini Edwin?akauliza Ruby huku akitabasamu

“Ninakuamini madamAnnabel lakini ninataka tu kuchukua tahadhari kwani tumewahi

kupata taarifa kama hizo na tukatumia nguvu kubwa kujiandaa lakini baadae tukagundua kwamba si taarifa za kweli ndiyo maana tumekuwa tunataka kujiridhisha kila pale tunapopata taarifa kama hiyo kujua chanzo chake kama kinaaminika ii tusije jikuta tunatumia muda na rasilimali kwa taarifa ambayo haina ukweli wowote” akasema Edwin

“Ni jambo zuri Edwin kujiridhisha kila pale mnapopata taarifa kama hizi

lakini kwangu mimi nakuomba usiwe na wasiwasi wowote.Nina uhakika na kile ninachokisema.Naomba ukaanze kufanya maandalizi” akasema Ruby na Edwin akatoka akaelekea sehemu Fulani iliyojificha akachukua simu na kumpigia simu Melanie katika namba ambayo huitumia kwa ajili ya kuwasiliana na watu muhimu tu.

“Edwin” akasema Melanie

“Melanie kuna jambo limetokea nimeona nikujulishe mapema”

“Jambo gani?akauliza Melanie

“Tumetoka katika kikao muda mfupi uliopita.Huwezi amini mkurugenzi wetu tayari anafahamu kuhusu ujio wa Khalid” akasema Edwin

“That’s not true ! akasema Melanie

“Nakwambia ukweli.Hata mimi hapa nilipo mwili unanitetemeka siamini nilichokisikia kutoka kwa mkurugenzi.Sifahamu amepata wapi taarifa hizo” akasema Edwin na Melanie akashusha pumzi

“Hizi ni taarifa za kustusha sana Edwin.Ujio wa Khalid ulikuwa ni kitu cha siri kubwa” akasema Melanie

“Inashangaza namna mkurugenzi alivyofahamu “

“What are we going to do Edwin?akauliza Melanie

“Nadhani njia nzuri ni kutafuta namna ya kumjulisha Khalid abadili uelekeo na asije tena Tanzania”

“That’s impossible.Tayari Khalid yuko angani anakuja Tanzania.Hatuwezi kuahirisha safari yake.Kwa nana yoyote ile lazima Khalid aingie

nchini.Jukumu zima liko juu yako hivyo fanya kila linalowezekana kuhakikisha Khalid anaingia nchini bila matatizo yoyote” akasema Melanie na Edwin akawa kimya akitafakari

“Edwin ! akaita Melanie

“Nakusikia Melanie”

“Kama nilivyokueleza kwamba fanya kila linalowezekana kuhakikisha Khalid anaingia nchini hata kama tayari taarifa za ujio wake zimekwisha ifikia idara yako.Nini mnakusudia

kukifanya kuhusu Khalid?akauliza Melanie

“Nimeelekezwa kuweka timu itakayomfuatilia kutoka uwanja wa ndege hadi mahala atakapofikia”akasema Khalid

“Imekuwa vizuri umepewa jukumu hilo wewe mwenyewe hivyo basi hakikisha unaivuruga timu hiyo inayomfuatilia Khalid.Umenielewa Edwin?akauliza Melanie

“Nimekuelewa Melanie.Niachie jambo hili nitalishughulikia”

“Good.Nijulishe tafadhali kila kinachoendelea huko.Edwin kwa namna yoyote hakuna kushindwa katika hili.Ukishindwa tutakuwa tumeshindwa wote kwani mategemeo yetu yote yako kwako” akasema Melanie na kukata simu.

“Dah ! Huyu mkurugenzi amenistua sana.Amejuaje kuhusu Khalid?Amekuja jana tu lakini tayari ameanza na nguvu kubwa namna hii.Natakiwa kujitahidi sana katika jambo hili kwani kama wakiwafinikiwa kumfuatilia

Khalid wanaweza wakagundua kuhusu James Kasai na wakifika hatua hiyo sote ambao tuko kwenye mtandao tunakwenda kuangamia.Natakiwa kujitahidi mno kuhakikisha kwamba zoezi zima la kumfuatilia Khalid linavurugika” akawaza Edwin na kurejea ndani akaenda moja kwa moja katika meza ya mwanadada mmoja mfupi mwembamba akamtaka amfuate wakaenda katika chumba kimoja kilichokuwa na

kompyuta kadhaa na hakukuwa na mtu.

“Dina unakumbuka uliwahi kuniomba mkopo wa fedha wiki iliyopita.Bado unahitaji zile fedha?akauliza Edwin

“Ndiyo bado ninahitaji sana”akajibu Dina

“Ni kwa ajili ya nini? Akauliza Edwin

“Ni ada kwa mdogo wangu ambaye amekosa mkopo wa serikali kwenda chuo kikuu.Mimi ndiye ninayemsomesha”

“Kiasi gani unahitaji?akauliza

“Milioni tano”

“Nitakupa hizo fedha.Mara mbili ya hizo unazohitaji.Nitakupa milioni kumi” akasema Edwin na Dina akaruka ruka kwa furaha

“Uko tayari sasa hivi nikakupatie hizo fedha?akauliza Edwin

“Niko tayari Edwin.Mungu akubariki sana” akasema Dina kwa furaha kubwa.Haraka haraka wakaingia garini na kuondoka kuelekea nyumbani kwa Edwin

“Edwin pamoja na furaha nliyonayo kwa kukubali kunikopesha fedha tena kiasi kikubwa kama hicho nina wasi wasi kwamba yawezekana nikashindwa kurejesha kwa wakati”akasema Dina wakiwa garini

“Usiwe na wasi wasi Dina.Fedha hizo ninakupa na si mkopo”akasema Edwin na Dina akastuka

“Unanipa siyo mkopo?!

“Ndiyo”

“Ni fedha nyingi sana hizo mtu kupewa bila kutakiwa kurejesha”

“Sitaki unirejeshee hata shilingi moja lakini kuna kitu nitahitaji kutoka kwako”

“Kitu gani Edwin?akauliza Dina

“Si kitu kikubwa ni msaada mdogo tu”

“Nieleze tafadhali”

“Nitakueleza usijali” akasema Edwin

Walifika nyumbani kwake akamkaribisha Dina sebuleni na baada ya dakika chache akarejea akiwa na mfuko wa karatasi uliojaa mabunda ya noti.

“Hizi ni milioni kumi” akasema na kumkabidh Dina ambaye alitokwa na machozi ya furaha.

“Edwin ninashukuru sana.Naona ni kama muujiza mkubwa.Sikutegemea kabisa”akasema Dina

“Dina baada ya kupata kiasi hicho naamini mdogo wako atakwenda shule bila matatizo.Kuna kitu kidogo ninakihitaji kutoka kwako”

“Sema Edwin unahitaji kitu gani?akauliza Dina

“Jioni ya leo tutakuwa na zoezi la kumfuatilia Khalid

Sultan kama alivyosema mkurugenzi.Ninataka unisaidie kuvuruga mfumo wetu kwa dakika mbili tu kisha uurejeshe tena katika hali yake ya kawaida” akasema Edwin

“Sijakuelewa Edwin” akasema Dina

“Ni hivi.Tutakuwa na zoezi la kumfuatilia Khalid Sultan jioni ya leo.Wakati zoezi hilo linaendelea mimi nitakupa ishara na utavuruga mfumo wetu wote kwa dakika mbili halafu utaurejesha tena kama kawaida.” Akasema Edwin na Dina akaonekana kushangaa

“Are you serious Edwin?Yaani kwa kazi hiyo ya dakika mbili unanipa kiasi chote hiki cha fedha?akauliza Dina

“Ndiyo Dina.Nataka unisaidie kwa kazi hiyo pekee”

“Usijali nitakufanyia vile utakavyo”

“Thank you” akasema Edwin

“Lakini ni vipi kama nikigundulika nimevuruga mfumo wetu wakati wa zoezi muhimu?

“Mimi ndiye kiongozi wa operesheni hiyo.Hivyo hakuna

yeyote atakayekuletea tatizo endapo itagundulika.Lakini wewe ni mtaalamu sana wa mambo haya ya mtandao hivyo ufanye katika namna ambayo hakuna atakayeweza kugundua.Fanya ionekane ni hitilafu za kiufundi au hali ya hewa au chochote unachoweza ili mradi isigundulike ni kitu kimefanyika makusudi” akasema Edwin

“Sawa Edwin nitafanya hivyo”

“Kumbuka utafanya pale tu nitakapokupa ishara”

akasema Edwin kisha wakaondoka kurejea kazini.

****

Mathew aliwasili nyumbani kwake

“Mungu naomba unisaidie” akawaza na kushuka garini akaelekea ndani akakutana na Lucy mlangoni

“Karibu kaka”

“Ahsante Lucy.Yuko wapi Peniela?

“Yuko katika chumba cha mapumziko anakusubiri huko” akasema Lucy

“Nashukuru sana Lucy” akasema Mathew na kupanda ngazi kuelekea katika chumba cha mapumziko kilichopo ghorofani.Kupitia mlango mkubwa wa kioo akamuona Peniela akiwa amesimama dirishani akitazama nje.Akaufungua mlango taratibu na kuingia ndani.Peniela aliposikia mlango ukifunguliwa akageuka wakagonganisha macho.Kila mmoja alisimama mahala pale akimtazama mwenzake kwa dakika mbili na taratibu michirizi ya machozi

ikaonekana mashavuni mwa Peniela

“Hallo Penny” akasema Mathew

“Hallow Mathew” akasema na kuchukua kitambaa akafuta machozi

“Karibu sana.Pole na safari” akasema Mathew na kumtaka Peniela aketi.

“Ahsante sana kwa kuja Peniela.Nimefurahi kukuona tena” akasema Mathew

“Mathew I’m sorry nimeshindwa nifanye nini baada ya kuiona sura yako.Nimeshindwa

nikukumbatie niangue kilio au nifanye nini” akasema Peniela

“Nafahamu Peniela uko katika mstuko bado na itachukua muda kuamini kama kweli ni mimi lakini naomba nikuthibitishie kwamba ni mimi Yule Yule unayenifahamu” akasema Mathew

“Kwa nini Mathew umetutesa kiasi hiki?Unajua ni mateso gani mimi na watoto tumeyapitia ? akauliza Peniela

“Ninafahamu Peniela na sipati neno zuri la kuwaomba samahani kwa wakati mgumu

mliopitia lakini hata wewe mwenyewe unafahamu nising.....”

“Hapana hufahamu kitu chochote Mathew ! akasema Peniela kwa ukali na kumkatisha Mathew

“Hufahamu chochote kuhusu mateso ambayo mimi na watoto tumeyapitia.Ungejua kama tutateseka usingetengeneza kifo chako!

“Penny sikufanya hivyo na siwezi kufanya hivyo hata siku moja.Unajua ni namna gani ninakupenda wewe na watoto

hivyo nisingeweza kufanya kitu ambacho kingewaumiza”

“Mathew ninajuta kukupenda mtu kama wewe.Ningejua kama nitaishi maisha kama haya nikiwa nawe katu nisingekubali kuolewa nawe!

“Usiseme hivyo Peniela”

“Ni lazima niseme ili ufahamu.Ninajuta kuishi na mtu kama wewe.Unadiriki hata kutunga kifo chako na hufikirii familia yako itateseka kiasi gani.Kitu gani umekikosa Mathew.Nimekupa utajiri mkubwa maisha ya kifahari

lakini bado unarudia kazi zako hizi zisizo na maana yoyote.Unapata nini kutoka katika kazi hizi zinazokufanya uipe familia yako mateso makubwa?Maneno yale ya Peniela yakaonekana kumchoma sana Mathew

“Peniela una haki ya kunitukana mimi matusi ya kila namna unayoyafahamu lakini katu usithubutu kuitukana na kuidharau kazi yangu.Ni kazi hii hii ambayo leo unaidharau ndiyo kazi ambayo imekufanya leo hii ukajulikana dunia

nzima.Isingekuwa kwa kazi hii usingekuwa Peniela huyu wa leo hivyo nakuonya usithubutu kudharau kazi yangu !

“Lazima niseme ! Kazi hiyo imekuingizia nini hadi sasa? Toka umeanza kuifanya kazi hii hakuna manufaa yoyote uliyowahi kuyapata zaidi ya hasara.Umeipoteza hadi familia yako ya kwanza kwa sababu ya kazi hii lakini bado hujajifunza na sas……”

“Peniela stop !! akasema Mathew kwa hasira

“You want to hit me?Go ahead hit me I’m not scared of you ! akatamba Peniela

“Sifahamu nani kakuloga Mathew hadi unaacha hivi vyote nilivyokupa na kurejea katika kazi kama hizo zisizo na mshahara wowote.I didn’t know you are such a stupid…..” Peniela hakumaliza kile alichotaka kuisema akajikuta ameanguka sakafuni baada ya kulambwa kofi zito.Akagala gala pale chini na kuinuka akavua kiatu chake akaipiga meza ya kioo ikavunjika akachukua kipande cha kioo

akakirusha lakini Mathew akawa hodari akakikwepa halafu akamfuata tena na kumnasa kofi lingine zito Peniela akajikuta amekaa sofani.Damu zilianza kumtoka mdomoni.

“Nimekuonya dhidi ya dharau na kejeli zako kwa kazi yangu.Nitukane utakavyo lakini si kutukana na kudharau hiki ninachokifaya.Do you know what I’m going through right now?Nina majukumu mazito ya kuisadia nchi hivyo sintavumilia kejeli za mtu kama wewe.Sintajali wewe ni

mke wangu au nani lakini utakaponikosea heshima katika kazi yangu lazima nikufunze adabu ! Hii ni mara ya kwanza ninakupiga toka nimekuoa na nimekupiga kutokana na dharau ulizozionyesha.Ulipaswa kunionea huruma badala ya kuanza kunikejeli.Unadai umenipa utajiri ?Mimi ndiye niliyekupa huo utajiri ambao leo hii unakupa kiburi!
Akafoka Mathew

“Everything came from blood.You have nothing you

stupid ! akafoka Peniela huku akilia

“Fine.Kwangu mimi utajiri wa mali si kitu na sihangaiki nao.Ninahangaika kwa ajili ya nchi yangu na watu wake wakae kwa amani na wala sihitaji mtu anilipe kwa kazi hiyo bali ni Mungu mwenyewe ndiye atakayenilipa kwa njia anazojua yeye mwenyewe hivyo tafadhali usinitusi kuhusu mali hizi ambazo ninaweza kuzitafuta na kupata kushinda hata hizo ulizonazo.Nimekuta umeuza

mali zote na sijakulaumu kwa sababu sihangaiki na mali”

“Kama uhangaiki na mali kwa nini ukanipigia simu?

“Nilitaka kupata uhakika kama ni wewe uliyeuza”

“Ni mimi nimeuza jasho langu.Siwezi kuacha mali zangu kwa mtu asiye na shukrani hata chembe!

“Ni wewe ambaye umekosa shukrani kwangu kwani kama nisingesimama imara mimi haya yote usingekuwa nayo”

“Huna uimara wowote Mathew.Ungekuwa imara

usingetengeneza kifo chako na kuiacha familia yako katika mateso makubwa”

“I didn’t fake my death but .....” akasema Mathew na kunyamaza kidogo

“Hukuonekana kuumizwa na kifo changu hata kidogo ndiyo maana hukusumbuka kutafuta ukweli hukusumbuka hata kutafuta kaburi langu liliko”

“Ninajutia hata machozi niliyoyamwaga kwa ajili yako.Hustahili machozi yanguMathew ! Wewe ni mtu mnyama sana !

“Ninalifahamu hilo.Sikustahili machozi yako kwa sababu tayari ulikwisha nitoa ndani ya moyo wako.Nafahamu mapenzi kati yetu yalikwisha zamani ni mimi ambaye niliendelea kubembeleza na ulipopata taarifa za kifo changu ulishukuru” akasema Mathew na kuvuta pumzi ndefu

“Ninafahamu kuhusu mapenzi yako na Nahum kijana wa kutoka Israel.I saw you and I was hurt”akasema Mathew na Peniela akabaki kimya akimtazama Mathew

“Ulifanya haraka sana kuamua kuwa na mwanaume mwingine wakati hujaupata ukweli halisi kuhusu kifo changu”

“Ouh kumbe ulikuwa unanifuatilia ! Stupid. ! akasema Peniela na kufuta damu kwa kitambaa

“Imekuwa vizuri kama ulikuwa unanifuatilia na umegundua kwamba nilikuwa na mwanaume mwingine anayejitambua kuliko wewe !

“Nahum alikuwa anakuchezea tu Peniela.Alikuwa ni jasusi wa

Israel na alikuwa kazini! akasema Mathew na Peniela akawa kimya.Baada ya muda akasema

“Sijali kama alikuwa ananichezea ama vipi lakini alikuwa anajielewa kuliko wewe.Sitaki mjadala mrefu na wewe.Nimesafiri usiku kucha kuja hapa Tanzania kwa ajili ya kitu kimoja tu” akasema Peniela na kunyamaza akamtazama Mathew

“Nimekuja kulimaliza hili” akasema tena na kufuta machozi

“Mathew nilitegemea kuwa mwanamke mwenye furaha kubwa katika maisha yangu lakini imekuwa kinyume chake nimekuwa ni mwanamke mwenye mateso makubwa kuliko furaha.Nyakati nilizowahi kuwa na furaha toka nimekuwa nawe ni chache sana.Nimejitahidi kuvumilia nikitegemea labda siku moja mambo yatabadilika lakini hakuna dalili zozote za mabadiliko na ninaendelea kuumia na wewe mwenzangu huonekani kujali furaha yangu na wanangu.Umesema

nisidharau kazi yako na siwezi kufanya hivyo lakini kwa kauli hiyo umedhihirisha wazi kwamba umechagua kazi kuliko mimi na watoto.Hauoni tena thamani yetu ndiyo maana umekuwa ukiendelea na maisha yako huku sisi tukimwaga machozi kila siku kukulilia na kukuombea.Sitaki kuendelea na maisha haya Mathew na Mungu atanisamehe kwa maamuzi haya niliyoyachukua" akasema Peniela na kuinuka akaenda kuchukua mkoba wake akaufungua na kutopa bahasha

ya khaki akampatia Mathew akaifungua na kukuta ni nyaraka za mahakama za kutengua ndoa.Mathew akaziweka karatasi zile na kumtazama Peniela kwa hasira

“Utanisamehe Mathew hayo ndiyo maamuzi niliyoyachukua na sintabadili tena maamuzi yangu.Nataka niwe na furaha katika maisha yangu na furaha hiyo siwezi kuipata nikiwa nawe hivyo nimeamua kuachana nawe ili kila mmoja aendelee na maisha yake kwa amani.Wewe utaendelea na kazi yako

ambayo ni ya muhimu kuliko sisi na mimi nitaendelea na maisha yangu na kama Mungu akinijalia basi nitampata Yule ambaye atanipa furaha ya maisha ninayoihitaji" akasema Peniela na Mathew akazichukua tena zile karatasi akazisoma kisha akamtazama Peniela

"Are you sure you want to do this?akauliza Mathew

"I'm sure 100%" akajibu Peniela

"Please sign the papers Mathew.Hakuna namna unayoweza ukanishawishi

nikabadili maamuzi yangu.It’s over please accept it.Kuhusu mali usiwe na wasiwasi nitakugawia robo ya mali zangu zote” akasema Peniela.Mathew akatafakari akavuta pumzi ndefu na kusema

“Arlight let’s end this.Lakini…” akasema Mathew na kumtazama Peniela

“Naomba ufahamu kwamba ninapo weka saini makaratasi haya ninaufunga mlango ambao hautafunguliwa tena.Lifahamu hilo na

ninaomba uwe na uhakika na hiki unachotaka kukifanya”

“Saini karatasi Mathew.I don’t care if there is a door or window between us.Ninachokihitaji ni kuachana nawe rasmi.Siwezi kuishi na mtu ambaye anakufa na kufufuka.Hujui lini atakufa kifo cha kweli.Siwezi kuendelea kuteseka kiasi hiki.Labda Mungu atakujalia utampata Yule ambaye atakuelewa na atakuwa tayari kuishi nawe lakini mimi nimeshindwa kukuelewa na siko tayari kuendelea kuishi

nawe” akasema Peniela.Mathew akazitazama tena zile karatasi kwa makini

“Kama alivyotamka yeye mwenyewe kwamba it’s over.Hakuna namna ninavyoweza kumshawishi akabadili maamuzi yake na mimi siwezi nikaacha kazi hii muhimu kwa nchi nikamfuata mwanamke.Kwangu nchi kwanza na mengine baadae kwa hiyo niko tayari kuitoa sadaka ndoa yangu.Ngoja nimuache aende kwani sintaweza kumpa furaha anayoihitaji katika maisha

yake.Nitakuwa mchoyo kama nitaendelea kung'ang'ania kuwa naye" akawaza Mathew

"Peniela naomba unisikilize" akasema Mathew

"Nimekuelewa kile unachokitaka na nitakutimizia.Sitaki kuwa mchoyo nataka ukaitafute furaha ya maisha unayoihitaji lakini kabla ya kuweka saini karatasi hizi kuna mambo ambayo nataka tukubaliane" akasema Mathew na kunyamaza kidogo halafu akasema

“Kwanza kabisa ni kuhusu watoto.Ninaomba sana jambo hili liwe ni letu peke yetu na watoto wasifahamu chochote.Wataendelea kufahamu kuwa nimefariki dunia hadi hapo baadae mambo yangu yatakapotulia nitawatafuta na kuwaeleza ukweli.Jambo la pili ni kuhusu mali” akanyamaza tena kidogo

“Sihitaji chochote kutoka katika mali zako Peniela.Kama uliamua kunitengea fungu langu ligawanye mafungu manne na kila mtoto wangu apate fungu lake.Jambo la tatu

kuna msaada ninauhitaji kutoka kwako”

“Kama umekataa mali nilizokupa unataka nikusaidie nini tena? akauliza Peniela.

“Ninahitaji taarifa”

“Taarifa zipi unahitaji?akauliza Peniela

“Nataka kumfahamu Yule mtu uliyemuuzia mali za hapa Dar es salaam Melanie Davis” akasema Mathew na uso wa Peniela ukaonyesha mshangao

“Melanie Davis?! Kwa nini unataka kumfahamu?

“Ninahitaji kupata taarifa zake.Wewe ndiye

unayemfahamu vyema hivyo basi nakuomba unipe taarifa zake” akasema Mathew

“Unataka kumfanya nini Melanie? Tafadhali naomba usimguse mimi ndiye niliyemuuzia mali zangu na zilizobaki nikampa Gosu Gosu.Sikujua kama utafufuka tena” akasema Peniela

“Peniela narudia tena kukukumbusha kwamba sihitaji mali.Ninao uwezo wa kuishi maisha ya aina yoyote ile hivyo mali si kipaumbele kwangu.Huyu Melanie sihitaji kumsumbua kwa chochote

kuhusu mali alizonunua kwani amenunua kihalali kabisa”

“Kwa nini sasa unataka taarifa zake?

“Utanipa taarifa zake au haunipi?Mathew akauliza

“Utanifanya nini kama nisipokupa taarifa zake?

“Sintasaini karatasi hizi na wewe utaendelea kuwa mke wangu hadi kifo kitutenganishe” akasema Mathew na kuweka kalamu chini.

“Simfahamu Melanie Davis vizuri.Niliwatangazia watu wangu wa karibu hasa

wafanya bishara kuhusu mpango wangu wa kuuza mali zilizoko Tanzania na kuwataka wanisaide kutafuta mnunuzi.Walikuja wanunuzi wengi lakini akajitokeza Melanie ambaye alikuja na bei nzuri na kuwazidi wale wote waliokuja mwanzo hivyo basi nikamuuzia kila kitu”

“Melanie anatajwa kuwa mmoja wa mabilionea wakubwa nchini Ufaransa utajiri ambao alirithi kutoka kwa wazazi wake.Wewe umekuwa miongoni mwa mabilionea wa Ufaransa je

umewahi kumsikia Melanie Davis hapo kabla?akauliza Mathew.Melanie akafikiri na kusema

“Hapana sikufahamu Melanie kabla”

“Umewahi kuwasikia wazazi wake?akauliza Mathew

“Hata wazazi wake sina kumbu kumbu kama nimewahi kuwasikia.Taarifa hizi zote umezipata wapi?akauliza Peniela

“Ukiacha haya makampuni uliyomuuzia hapa Tanzania unazifahamu biashara zake nyingine? Akauliza Mathew

“Hapana sizifahamu”

“Ikawaje ukamuuzia kampuni zako mtu ambaye humfahamu vyema?akauliza Mathew

“Nilihitaji mnunuzi na alipojitokeza sikutaka kumchunguza mara mbili nikamuuzia” akajibu Peniela

“Unafahamu yalipo makazi yake jijini Paris? Mathew akauliza

“Mathew sihitaji maswali yako tena.Kama unahitaji kumfahamu mtafute wewe mwenyewe ukamuhoji ! akasema Peniela kwa ukali

“Peniela I real need your help.Muda mfupi ujao nitakapoweka saini yangu katika hizi karatasi utakuwa ni mwisho wetu na mlango utafungwa.Only God knows when we’ll meet again hivyo basi huu ni msaada wangu wa mwisho ninakuomba unisaidie.Ni muhimu sana kwangu na ….” Akasema Mathew na Peniela akamkatisha

“Melanie ana umuhimu gani kwako? Kwa nini unatafuta taarifa zake

unamchunguza? Akauliza Peniela

“Peniela nisingependa kukueleza chochote kwa sa…”

“Kama hutanieleza sababu za kutafuta taarifa za Melanie sintakueleza chochote ninachokifahamu” akasema Peniela.

“Arlight unataka kufahamu? Ni kwamba mtu uliyemuuzia makampuni yako hapa Tanzania Melanie Davis ana mahusiano na kikundi cha kigaidi cha IS na vile vile ana mashirikiano na James Kasai

kiongozi wa kundi la waasi ambaye hivi karibuni alifanya shambulio hapa nchini ambalo liliua wake za marais wa Tanzania,Congo na Rwanda.IS wamekuwa wakimtumia Melanie kupitishia fedha kwenda kwa James Kasai.Umemuuzia mali mtu hatari kabisa kwa usalama wa nchi yetu" akasema Mathew na Peniela akabaki mdomo wazi na mara simu ya Mathew ikaita alikuwa ni Dr Masawe.

"Samahani nataka kuipokea hii simu" akasema Mathew na kuipokea ile simu

“Dr Masawe” akasema Mathew

“Mathew nimekupigia kukupa taarifa kwamba tumepokea taarifa muda mfupi uliopita kutoka polisi kwamba mwili wa Dr Sebastian umeokotwa ufukweni akiwa amekufa.Polisi wanasema alipigwa risasi ya kichwa”

“Sebastian ameuawa! Mathew akashangaa

“Ndiyo Mathew ameuawa”

“Dr Masawe suala hili ni kubwa.Nitafika hapo hospitali tutazugumza kwa kirefu zaidi.Nashukuru sana kwa

taarifa” akasema Mathew na kukata simu akamtazama Peniela.

“Unafahamu kama Melanie na Gosu Gosu wana mahusiano ya kimapenzi?akauliza Mathew

“Ndiyo ninafahamu.Ni mimi ndiye niliyewaunganisha.Nilimuita Gosu Gosu Ufaransa kwa ajili ya kufanya mauziano na Melanie na walipokutana wakapendana wakawa wapenzi” akasema Peniela

“Tunahisi kwamba Gosu Gosu kuna kitu alikigundua

kuhusu Melanie ndiyo maana wakataka kumuua.Alipigwa risasi nyingi ili afariki lakini siku yake haikuwa imefika akanusurika na jana likafanyika tena jaribio lingine la kutaka kumuua.Daktari mmoja alitumika kumchoma sindano ya sumu Gosu Gosu kwa bahati mbaya jaribio hilo la kumuua halikufanikiwa lakini imelazimu Gosu Gosu kufanyiwa upasuaji wa kupandikizwa ini jana usiku kwani ini lake liliharibiwa kabisa na sumu.Melanie ni mwanamke hatari kabisa hata

wewe ujihadhari naye sana kwani mtandao wake ni mkubwa” akasema Mathew

“Kwa hiyo hivi sasa unaendesha zoezi la kumsaka Melanie Davis?akauliza Peniela

“Ndiyo.Ninamsaka Melanie Davis na ndiyo maana ninahitaji sana msaada wako”

“Mathew unamtafuta Melanie kwa sababu anashirikiana na magaidi wa IS au kwa sababu amenunua mali zako? Peniela akauliza

“Kwa mara nyingine tena Peniela nakukumbusha

kwamba mimi sihitaji mali.Hizi zote ni mali zako na mimi nilikuwa msimamizi wake tu hivyo sina kinyongo chochote na Melanie kununua mali zangu.Nilikuwa naendelea na operesheni yangu ya kuwasaka magaidi na ndipo Melanie Davis alipojitokeza na nikaanza kumfuatilia na kugundua ndiye aliyenunua mali zangu. Sikuwa na sehemu nyingine ya kuweza kupata taarifa zake ila kwako ndiyo maana nikakupigia" akasema Mathew

“Nilichokueleza ndicho kitu niachokifahamu kuhusu Melanie labda nitakusaidia kufanya uchunguzi na nikipata taarifa zozote za kumuhusu yeye nitakujulisha” akasema Peniela

“Nitashukuru sana” akasema Mathew

“Maswali yamekwisha can you sign now?akauliza Peniela

Mathew akaishika kalamu na kumtazama Peniela kisha akaanza kusaini zile karatasi.Alipomaliza akazirudisha ndani ya bahasha na kumkabidhi Peniela

“Ahsante Mathew na samahani sana kwa maamuzi haya ” akasema Peniela.

“Usijali Peniela.Ninakupongeza kwa maamuzi haya magumu ambayo umeyafanya.Unahitaji furaha katika maisha yako na mimi si mtu sahihi ninayeweza kukupa hiyo furaha.Maisha yangu hayataweza kubadilika kamwe kwani nililetwa duniani kwa ajili ya kazi hii na nitandelea nayo hadi siku ya kufa kwangu.Ninakushukuru sana kwa kunivumilia kwa muda mrefu na samahani vile

vile kwa kuwasababishia maumivu makubwa lakini halikuwa kusudi langu kuwaumiza.Ninachokuomba wakuze watoto katika maadili mazuri wawe na bidii katika masomo,wamjue Mungu wafundishe kusaidia watu wenye uhitaji kwa kuwa wao wamezaliwa katika utajiri mkubwa.Wasaidie kuhakikisha wanatimiza ndoto zao lakini kamwe,narudia tena kamwe usiruhusu mtoto wangu yeyote akafanya kazi kama ninayoifanya mimi.Sitaki waje kuishi maisha kama ninayoishi

mimi.Sitaki wayapitie yale ninayoyapitia.Waweke mbali kabisa na dunia hii ninayoishi mimi.Nadhani umenielewa Peniela” akasema Mathew na Peniela akafuta machozi

“Nimekuelewa Mathew na mimi pia ninakuomba samahani sana kila pale nilipokukosea.Najua sikuwa mkamilifu nimekukwaza mara nyingi,tuliwahi kutengana na mimi nilikuwa chanzo,nimewahi kuwa na mahusiano na wanaume kadhaa ulifahamu lakini

ulinivumilia.Nisamehe sana kwa yote” akasema Peniela

“Hakuna mwanadamu mkamilifu.Sote tuna mapungufu yetu na mimi niliyafahamu mapungufu yako nikayakubali na kuyabeba.Nategemea Yule atakayekuja baada yangu naye atakuwa mvumilivu kama mimi.Ninakutakia kila la heri Peniela”akasema Mathew na kusimama

“Mathew kabla hatujapeana kwa heri ya kuonana kuna kitu nataka kukifahamu.Ulizungumza

kuhusu Nahum.Umemfahamuje?Ulifa hamuje kama mimi na yeye tulikuwa na mahusiano?akauliza Peniela na Mathew akaketi

“Haitakuwa na umuhimu wowote tena kwako kwa sasa lakini kwa umeuliza nitakueleza ukweli wa kile kilichotokea” akasema Mathew na kumsimulia kuanzia Olivia Themba alivyotekwa na SNSA,sakata la Edger Kaka na hadi operesheni ile ya kuwakomboa mateka waliotekwa na IS na hadi

alivyopigwa risasi na kutekwa.Mashavu ya Peniela yaliloa machozi

“Nilipofumbua macho nilijikuta katika chumba chenye kiza na baadae nikagundua nilikuwa nchini Israel. Nilianza kupatiwa mateso makali na nimeteswa kwa muda wa miaka mitatu” akasema Mathew na kuvua fulana akamuonyesha Peniela makovu ya vidonda vilivyotokana na mateso aliyoyapata.Peniela akafumba macho hakutaka

kutazama.Mwili wa Mathew ulijaa makovu ya vidonda.

“Haya ndiyo niliyoyapitia huko Israel kwa miaka mitatu.Sikumbuki ni mara ngapi nilipoteza fahamu wakati nikiteswa lakini ni mara nyingi.Pamoja na mateso hayo makali lakini sikuwahi kufungua mdomo wangu kusema chochote na ndipo walipoamua kuitumia familia yangu kunilazimisha niongee.Wakamtuma Nahum Yatom aje Ufaransa aanzishe mahusiano nawe na lengo lake likafanikiwa.Nahum alikuwa

ni jasusi kutoka shirika la ujasusi la Israel Mossad.Hakuwa na malengo yoyote nawe bali alikuwa kazini.Zilifungwa kamera chumbani kwako na Mossad walikuwa wanafuatilia kila mlichokuwa mnakifanya na Nahum.Nilionyeshwa mkiwa chumbani mkifanya mapenzi na Nahum nikaumia sana na Mossad walikuwa wakihitaji niumie ili niweze kuzungumza na kwa maumivu niliyokuwa nayo nikajikuta nikianza kuzungumza” akasema Mathew

“It was true then ….” Akasema Peniela akifuta machozi

“Nini Peniela?

“Kabla ya kuuawa Nahum aliniambia uko hai nikutafute lakini nikapuuza maneno yake”

“Alikwambia hivyo?akauliza Mathew

“Ndiyo aliniambia hivyo” akajibu Peniela

“Nani alimuua Nahum?Mathew akauiza

“Hadi leo hii haijulikani nani waliomuua”

“Lazima atakuwa ameuawa na Mossad” akasema Mathew

“Mathew I’m sorry sikuyafahamu hayo yote uliyoyapitia” akasema Peniela

“Usijali Penny yamekwisha pita ila nakuomba usimueleze mtu yeyote haya niliyokueleza”

“Sintamueleza mtu yeyote Yule” akasema Peniela

“Naamini sasa utakuwa huru Peniela jitahidi uwe na furaha katika maisha yako.Usiwaze chochote kuhusu mimi.Maamuzi haya

uliyoyafanya ni maamuzi sahihi kwa wakati sahihi” akasema Mathew na Peniela akaendelea kulia.

“Mathew please I need a hug” akasema Peniela na Mathew akainuka akaenda kumkumbatia.

“Mathew I’m very sorry ! akasema Peniela akilia na kumwaga machozi katika bega la Mathew

“Peniela unahitaji kuwa jasiri wala usisikitike kwa maamuzi haya uliyoyachukua” akasema Mathew na kumuachia Peniela.

“Unarejea leo Paris?Mathew akauliza

“Nimekuja na ndege yangu ninaondoka leo hii kurejea Paris.Kabla sijaondoka naomba unipeleke nikamuone Gosu Gosu” akasema Peniela na Mathew akamuogoza hadi katika gari lake wakaondoka kuelekea hospitali kumtazama Gosu Gosu.

“Watoto wanaendeleaje?akauliza Mathew

“Kwa sasa wametulia wanaendelea vizuri na masomo na maisha yao kwa

ujumla lakini kwa miaka miwili hapo nyuma walikuwa wameathiriwa sana na kifo chako”

“Ndiyo maana sitaki wafahamu chochote kuhusu mimi kuwa hai kwa sasa hadi hapo baadae.Nakuomba tena usiwaeleze chochote kuhusu mimi” akasema Mathew

“Sintawaeleza chochote kwani watachanganyikiwa zaidi”

“Peniela …” akaita Mathew

“Unasemaje Mathew?

“Naomba ufahamu hayakuwa mategemeo yangu

maisha yetu yawe namna hii.Sikutegemea kama siku moja tungemaliza mahusiano yetu namna h……” akasema Mathew na Peniela akamkatisha

“Mathew tumekwisha yamaliza hayo kitu cha msingi ni kutazama yale ya mbele yetu.Muda wowote ukihitaji kitu chochote tafadhali usisite kuniambia.Namba yangu ya simu ni ile ile”akasema Peniela

“Am I doing the right thing?akajiuliza Peniela na kumtazama Mathew kwa jicho la wizi

“Namuonea huruma sana Mathew kwa mambo anayoyapitia.Mwili wake umeumizwa vibaya sana hadi nilisisimkwa mwili nilipoyaona makovu yale katika mwili wake.Sikuufahamu ukweli na nikadhani alitengeneza kifo chake kumbe alikuwa katika mateso.Nimechanganyikiwa.N ifanyaje wakati tayari amekwisha saini hizi karatasi?Nilimtamkia maneno mabaya sana yaliyomuudhi hadi akaamua kunipiga kitu ambacho hajawahi kukifanya toka tumekuwa wapenzi.I was

so stupid.Nilikurupuka sana kufanya maamuzi kama haya kwa mtu kama huyu ambaye amekwisha fanya mambo mengi sana kwa ajili yangu.Amesimama nami katika nyakati ngumu ambazo hakuna aliyewezaa,amenivumilia kwa mengi,huyu ni mwanaume wa kipekee kabisa na ninaumia kwa hiki nilichokifanya lakini maamuzi haya ni kwa faida yetu sote.Mathew amechagua kuendelea na kazi yake ya ujasusi” akaendelea kuwaza Peniela.

Walifika katika hospitali kuu ya Mtodora alikolazwa Gosu Gosu.Mathew akafanya mpango na Peniela akaruhusiwa kuingia kwenda kumuona Gosu Gosu akamwaga machozi alipomuona akiwa amelala kitandani hana fahamu.Baada ya kutoka kumuona Gous Gosu Mathew akampeleka katika chumba alimolazwa Austin akamtambulisha kwa Peniela.

“Huyu ndiye aliyejitolea sehemu ya ini alilopandikizwa GosuGosu” akasema Austin na Peniela akamshukuru kwa kile

alichokifanya.Baada ya zoezi hilo kukamilika Peniela hakuwa na kitu cha ziada ulikuwa ni wakati wake wa kuondoka kurejea Paris.Mathew akamsindikiza uwanja wa ndege

“Nimeumizwa sana na hali ya Gosu Gosu.Nakuahidi nitakwenda kutafuta taarifa za kuhusu Melanie Davis na nitakujulisha” akasema Peniela wakiwa garini

“Ahsante sana” akasema Mathew

Hakukuwa na mazungumzo mengi garini

hadi walipofika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere.Mathew akashuka na kumfungulia Peniela mlango

“Penny this is it.” Akasema Mathew

“Mathew thank you for everything” akasema Peniela wakakumbatiana na kwa mara ya mwisho Mathew akambusu Peniela

“Please go and don’t look back” akasema Mathew na Peniela akaelekea ndani ya jengo la uwanja wa ndege wa Julius Nyerere huku machozi yakimdondoka.

Mathew hakuondoka pale uwanjani hadi alipoiona ndege ya Peniela yenye maandishi makubwa Penny air ubavuni, ikipaa na kuondoka.

“Kwa heri Peniela”akasema Mathew na kuingia katika gari lake akaondoka.

“Naona kama ndoto lakini ni kweli nimeachana na Peniela.Nimetoka naye mbali,tumepitia mengi na hatimaye safari yetu imehitimishwa rasmi leo.Inaniumiza kuacha na mtu ambaye niliahidi kuishi naye

hadi kifo lakini ahadi hiyo imeshindwa kutimia” akawaza Mathew

Kutoka uwanja wa ndege wa Julius Nyerere akarejea nyumbani kwake akaenda moja kwa moja chumbani kwake na kuchukua albamu lenye picha mbali mbali alizowahi kupiga na Peniela na familia yake.

“Tumewahi kuwa na nyakati nyingi nzuri lakini kwa sasa sina hakika kama ninaweza tena kumfanya Peniela awe na furaha.Siwezi kumlaumu kwa maamuzi

aliyoyachukua.Natakiwa kusonga mbele na maisha yangu” akawaza Mathew na kumpigia simu Ruby akamjulisha kilichotokea kati yake na Peniela na Ruby akamuahidi kwamba atamfuata nyumbani kwake.

Ndege ya Peniela ilipokaa sawa angani akachukua simu yake ya intaneti akampigia mtu Fulani na simu ikapokelewa

“Peterson ni mimi Peniela.Ninapozungumza nawe hivi sasa niko Afrika.Niliondoka jana jioni

lakini kwa sasa niko angani narejea Paris”akasema Peniela

“Peniela pole kwa safari ndefu” akasema Yule jamaa aliyekuwa akizungumza na Peniela simuni

“Nashukuru Peterson.Nimekupigia simu kuna kazi muhimu nataka unisaidie kuifanya.Kuna mtu mmoja anaitwa Melanie Davis.Huyu anatajwa kuwa mmoja wa mabilionea wa jiji la Paris.Nataka umfanyie uchunguzi wa kina na kesho asubuhi uniletee ripoti nyumbani” akasema Peniela

“Peniela nini hasa unachotaka tukichunguze kwa huyo Melanie Davis? Akauliza Peterson

“Kila kitu kuhusu maisha yake.Ametokea wapi,wazazi wake,anakoishi hapa Paris,anafanya biashara gani na ziko wapi,akaunti zake za benki,marafiki zake ni akina nani wanafanya nini n.k.Nataka kujua kila kitu mnachoweza kukipata kuhusu Melanie”akasema Peniela

“Sawa mama Peniela.Hiyo ni kazi ndogo sana kwetu.Kesho saa kumi na mbili

za asubuhi nitakugongea mlango kukupa ripoti” akasema Peterson na kuagana na Peniela

“Ngoja niwatumie hawa wapelelezi wa kujitegemea kumchunguza Melanie.Mathew amenistua sana kuniambia kwamba anashirikiana na magaidi wa IS.Lakini Melanie ni mwanamke mwenye uzuri wa kipekee kabisa kwa nini anashirikiana na magaidi wa IS?Kinachoniumiza zaidi ni kwamba anajificha nyuma ya biashara nilizomuuzia

kutekeleza mambo yake.Mathew aliniambia kwamba amekuwa akipokea kiasi kikubwa cha fedha kutoka IS.Yawezekana ni fedha hizo hizo ndizo ambazo alizitumia kununulia kampuni nilizomuuzia.Imeniuma sana na ninajiona mjinga.Niliona aibu kubwa mbele ya Mathew aliponiuliza sababu ya kuuza mali zetu kwa mtu anayeshirikiana na magaidi.” akawaza Peniela na sura ya Mathew ikamjia akaanza kutiririkwa machozi

“Mathew amepitia mateso makubwa sana kwani mwili wake wote umejaa makovu ya vidonda vilivyotokana na mateso makali aliyokuwa akiteswa.Kwa nini lakini Mathew ameamua kuchagua kuendelea kufanya kazi hii na kuacha maisha mazuri aliyokuwa akiishi?akajiuliza Peniela

“Mathew amenifanya niwachukie magaidi na watu wanaowasaidia kama akina Melanie kwani ndio waliomfanya Mathew ashindwe kutulia na kutumia

muda wake mwingi akihangaika kupambana nao hadi kufikia hatua hii ya kutengana” akawaza Peniela

****

Ruby alifika nyumbani kwa Mathew saa kumi na mbili na nusu za jioni

“Samahani Mathew nimechelewa sana nilikuwa nafuatilia maandalizi ya zoezi la jioni ya leo.Kila kitu kimekwisha andaliwa” akasema Ruby wakaelekea katika ofisi ya Mathew na

Ruby akajiunga na ofisi yao na picha kutoka katika kamera mbali mbali katika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere zikaanza kuonekana.

“Tayari vijana wamejipanga vizuri.Wapo walioko ndani kabisa ya uwanja na katika sehemu mbali mbali za uwanja na Khalid atafuatiliwa toka atakaposhuka uwanjani hadi atakapoingia ndani ya gari na watu wetu wengine wamejipanga sehemu mbali mbali.Kwa ujumla maandalizi

yote yamekamilika” akasema Ruby

Saa moja na dakika tano za jioni ndege ya shirika la ndege la Ethiopia ilitua katika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere jijini Dar es salaam.Lango la ndege likafunguliwa abiria wakaanza kushuka.Edwin Mbeko ambaye ndiye aliyekuwa akiongoza operesheni ile kutoka ofisi kuu ya SNSA akawataka watu wake wakae makini.Hatimaye Yule aliyekuwa akisubiriwa akatokeza katika mlango wa

ndege.Alikuwa amevaa suti ya rangi ya bluu

“Khalid Sultan anashuka ndegeni.Narudia Khalid Sultan anashuka ndegeni” mmoja wa watu wa SNSA aliyekuwa ndani ya uwanja akawajulisha ofisi kuu

“Tumekupata namba 3.Endelea kumfuatilia.Namba 5 jiandae Khalid anaelekea upande wako” akaelekeza Edwin Mbeko.

Khalid Sultan aliingia ndani ya jengo la uwanja wa ndege kwa ajili ya kukamilisha taratibu za kuingia

nchini.Baada ya kukamilisha taratibu Khalid akaruhusiwa kuingia Tanzania.

“Khalid tayari ameruhusiwa kuinga nchini anaelekea sehemu ya abiria wanaowasili” akasema jamaa mwingine aliyekuwamo ndani ya jengo la uwanja.

Kamera za ndani ya sehemu ya abiria wanaowasili ilimuonyesha Khalid akiingia kisha akapokewa na vijana wawili wadogo waliokuwa wameshika bango lenye jina la KSK.Wakasalimiana na kumsaidia kuyabeba

masanduku yake kuelekea katika maegesho.

“Khalid anatoka nje ya uwanja anaelekea eneo la maegesho ya magari” akaripoti jamaa mwingine

“Endeleeni kumfuatilia” akaelekeza Edwin

“Kwa nini Khalid amepokewa na vijana wale wadogo?Nilitegemea angepokewa na watu wazima” akasema Ruby kwa mshangao lakini Mathew hakumjibu kitu

Vijana wale wawili walimuongoza Khalid hadi katika gari moja aina ya Prado

rangi nyeupe wakaingia na kuondoka pale uwanjani.

“Khalid anaondoka hapa uwanjani” jamaa aliyekuwa nje eneo la maegesho ya magari akaripoti

“Namba nane na timu yako kazi kwenu anzeni kumfuatilia.Mtu huyu ni makini sana hivyo mjitahidi kuweka umbali kati yenu ili asijue kama anafuatiliwa.Mtamfuatilia kwa msaada wa Satelaiti” akaelekeza Edwin

Wakati zoezi la kumfuatilia Khalid likianza

Ruby alikuwa anashughulikia kuzitambua picha za wale vijana wawili waliompokea Khalid uwanja wa ndege na baada ya muda akaguna.

“Vijana wale ni wadogo na inaonekana hawajafikia umri wa kusajiliwa katika sehemu mbali mbali za usajili kwa ajili ya kupata vitambulisho vya taifa leseni nk.” Akasema Ruby.Bado Mathew hakumjibu kitu alikuwa kimya kabisa

Katika runinga mchoro mwekundu na wakijani iliendelea kuonekana ikijongea.Mchoro mwekundu

ukiwa ni wa gari alilopanda Khalid na mchoro wa kijani ukiwa ni wa gari la SNSA linalomfuatilia Khalid.

“Mmelikaribia sana gari la Khalid tafadhali acheni umbali kidogo” Edwin Mbeko akatoa maelekezo.

Gari lile alilopanda Khalid lilipita barabara kadhaa na halafu likafika katika mzunguko wa chama.Ghalfa mawasiliano yakakatika.

“Nini kimetokea?Mathew akamuuliza Ruby

“Sifahamu.Mawasiliano yamekata ghafla” akasema

Ruby na kuchukua simu yake akampigia Edwin

“Edwin kompyuta yangu imekata mawasiliano ghafla.Kuna tatizo lolote huko?akauliza Ruby

“Madam Annabel kuna tatizo limetokea si kwako tu bali hata huku.Kuna matatizo katika satelaiti tunayotumia na timu imeanza kulishughulikia hilo tatizo” akasema Edwin

“Kuna tatizo limetokea katika satelaiti na wanalishughulikia” Ruby akamwambia Mathew ambaye alipiga meza kwa hasira

“Usikasirike Mathew.Wanashughulikia suala hili na muda si mrefu litakuwa tayari” akasema Ruby

“Ofisi kuu kuna tatizo gani?Mawasiliano yamekatika ghafla hatulioni tena gari la Khalid” akasema kiongozi wa timu iliyokuwa ikimfuatilia Khalid.

“Kuna tatizo limetokea lakini linashughulikiwa na muda si mrefu mawasiliano yatarejea tena” akasema Edwin

Baada ya dakika mbili mawasiliano yakarejea lakini mduara uliokuwa ukionekana

ni mmoja tu wa kijani ambao ni gari la SNSA, gari alilopanda Khalid halikuwa likionekana

“We’ve lost him ! Tumempoteza Khalid.How could they let this happen?! Mathew akafoka

“I don’t know Mathew” akajibu Ruby kwa uoga kisha akampigia simu Edwin hakupokea.Akampigia tena simu mtu mwingine akapokea na kumjulisha kwamba Edwin alikuwa na timu ya ufundi wakijaribu kujua nini kilitokea

“Ruby do something ! akasema Mathew

“Nadhani natakiwa niende ofisini nikajue nini hasa kilitokea”

“Hata kama ukienda bado haitasaidia kitu.Khalid tumekwisha mpoteza.Dakika mbili ni nyingi sana kwa gari.Hatutaweza kumpata mida hii.Kwa nini tatizo hili limejitokeza sasa wakati wa zoezi muhimu kama hili? Akauliza Mathew

“Mathew matatizo kama haya ya kukatika mawasiliano

hutokea mara nyingi” akasema Ruby

“Nafahamu Ruby lakini..oh my God ! akasema Mathew na kushika kiuno

“Jaribu kufuatilia zile namba za gari alilopanda Khalid” akasema Mathew na Ruby akacheza na kompyuata yake baada ya muda akasema

“Namba zile ni bandia hazipo hazijulikani katka mfumo wa usajili wa namba za magari” akasema Ruby

“Dah ! Mathew akasema na kukaa juu ya meza.Akafikiri halafu akasema

“Ruby nisikilize”

“Hili suala lililotokea halikutokea kwa bahati mbaya.Huu ni mchezo umechezwa”

“Mathew tusifike huko kwanza.Hii yaweza kuwa ni hitilafu ya kiufundi imetokea.Tusubiri timu ya ufundi ifanye uchunguzi wake na tutagundua nini hasa kilitokea” akasema Ruby

“Ruby nafahamu hitilafu kama hizi huwa zinatokea lakini hiki kilichotokea usiku huu na tukampoteza Khalid si bahati mbaya.Hiki ni kitu

kilichopangwa” akasema Mathew

“Nani anaweza akafanya kitu kama hiki?akauliza Ruby

“Hebu jiulize kwa nini wametumwa watoto wadogo kwenda kumpokea Khalid? Ni kwa sababu walifahamu kuwa Khalid anafuatiliwa na mtu ambaye angeenda kumpokea angechunguzwa yeye ni nani ndiyo maana wakawatumia wale watoto kwenda kumpokea ambao hatuwezi kuwatambua.Khalid ni mtu mkubwa na hawezi kupokewa na wale watoto wadogo.Kama

haitoshi namba za gari lile alilopanda Khalid ni za bandia na waliweka namba hizo bandia ili tusiweze kumtambua mmiliki wa gari hilo.Walijua tunamfuatilia na ndiyo maana wakajiandaa namna hii.Huu ni mtandao mkubwa Ruby una watu makini na wanajua wanachokifanya.Walifahamu tunamfuatilia Khalid ndiyo maana mawasiliano yakakatika na hilo lilifanyika ili kulipoteza gari la Khalid kwani mawasiliano yaliporejea gari lile halikuonekana tena.Tunachotakiwa kujiuliza

ni je wamefahamuje kama tunamfuatilia Khalid? Wamefahamuje mipango yetu? Wamewezaje kukata mawasiliano kati ya ofisi kuu na timu iliyokuwa inamfuatlia Khalid? Akauliza Mathew na baada ya kufikiri kidogo Ruby akasema

“Nadhani tuanze kulitafutia majibu hili swali la mwisho ulilouliza kwamba mawasiliano yamekatikaje? Akasema Ruby

“Kwa ninavyofahamu mimi mfumo wa mawasiliano wa idara kama hii umejengwa

katika mfumo ambao si rahisi kwa mtu wa nje kuuingilia na kufanya chochote anachokitaka.Imetumika teknolojia ya hali ya juu sana”

“Unataka kuniambia kwamba mtu wa nje hawezi kuingia katika mfumo na kukata mawasiliano kati ya ofisi kuu na watu walioko nje ya ofisi? Akauliza Mathew

“Hapana haiwezekani.Ili kukata mawasiliano kati ya ofisi kuu na watu walioko nje ya ofisi lazima kwanza mfumo ukutambue hapa ninamaana ya kwamba lazima uwe ndani

ya mfumo wetu ndipo unaweza ukafanya kitu kama hiki kilichofanyika” akasema Ruby

“Kwa maana hiyo kama mawasiliano yalikatwa makusudi mtu aliyefanya hivyo lazima atakuwa anatoka ndani ya SNSA” akasema Mathew

“Ndiyo” akasema Ruby

“Mathew nina….” Akasema Ruby na kunyamaza baada ya simu yake kuita alikuwa ni Edwin

“Edwin ! akasema Ruby

“Madam Annabel samahani nilishindwa kupokea simu yako

uliponipigia.Nilikuwa na timu ya wataalamu tukifuatilia kujua nini hasa kilichotokea na kusababisha mawasiliano kukatika.Kwa mujibu wa wataalamu wetu ni kwamba lilikuwa ni tatizo la kawaida ambalo linaweza kutokea kufuatia hali mbaya ya hewa na hakukuwa na makosa yoyote ya kibinadamu” akasema Edwin

“Sawa Edwin hakikisha jambo kama hili halitokei tena siku nyingine hasa tunapokuwa katika operesheni kubwa kama hizi.Mmefikia

wapi katika kumsaka Khalid?Kuna mafanikio yoyote?

“Mpaka sasa hakuna madam na hatujui mahala alikoelekea kwa sababu mahala pale ambako mawasiliano yalikatikia pana njia nne hivyo hatujui njia ipi gari lile lilielekea.Tunaendelea na uchunguzi madam kujua mahala alikoelekea.Ninaamini tutalipata tu lile gari” akajibu Edwin

“Edwin hakikisha ndani ya muda mfupi tunfahamu mahala aliko Khalid”

“Usijali madam tunaendelea na zoezi hilo” akajibu Edwin na Ruby akakata simu akamueleza Mathew kile alichoambiwa na Edwin.

“Ruby ninaamini mno utaalamu wako katika masuala haya ya kompyuta na mawasiliano kuliko mtu mwingine yeyote na ndiyo maana hata kule Uingereza ulikokuwa unafanya kazi hawakutaka kukuacha uende.Sina hakika kama ndani ya idara ya SNSA kuna mtu mwenye utaalamu mkubwa wa

kompyuta kama ulio nao wewe.Nataka ulifanyie uchunguzi suala hili ili tujue kama kweli ni tatizo la kukatika kwa mawasiliano kama inavyodaiwa?akasema Mathew

“Ushauri wako ni mzuri Mathew.Itanilazimu sasa nielekee ofisini na uchunguzi huo nikaufanyie nikiwa pale ndipo nitakapoweza kujua nini hasa kimetokea.Ninakuomba twende wote” akasema Ruby

“Mimi si mfanyakazi wa SNSA hivyo nikionekana pale haitaleta picha nzuri kwako

utaonekana unaleta ndani ya idara watu wasiohusika” akasema Mathew.

“Mimi ndiye mkuu wa idara hivyo usiwe na wasiwasi wowote”akasema Ruby.Hawakupoteza muda wakaingia katika gari la Ruby wakaondoka kuelekea ofisi kuu ya SNSA.

****

Baada ya mawasiliano kukatika kati ya ofisi kuu ya SNSA na timu iliyokuwa ikimfuatilia Khalid

Sultan,jamaa aliyekuwa katika usukani wa gari lile alilopanda Khalid ambaye aliweka kifaa Fulani sikioni kwa ajili ya mawasiliano akaelekezwa kuendelea na mpango kama ulivyokuwa umepangwa.Dereva Yule akaelekea katika barabara ya Arusha halafu akakata kulia akaingia mtaa wa Mtepa akaingia katika shule moja ya watoto wadogo.Khalid na watu wengine wawili wakashuka na kuingia katika gari lingine lenye rangi nyeusi,likatoka ndani ya ile shule na kuelekea

Kisulo Car wash Khalid na watu wale wawili wakashuka na kuingia katika gari ambalo kulikuwa na dereva mwanamke ambaye alilliondoa lile gari mahala pale.Safari ilikuwa ya kimya kimya hadi walipofika katika makazi ya Melanie Davis geti likafunguka gari likaingia ndani.Khalid na wale jamaa wawili wakashuka garini wakapokewa na Melanie Davis akawakaribisha ndani.

“Khalid karibu sana Tanzania,karibu sana Dar es salaam.Utatusamehe kwa mzunguko mrefu hii ni kwa

sababu za kiusalama”akasema Melanie

“Ninawapongezeni kwa tahadhari kubwa mlizozichukua.Ninyi ni watu makini sana nimefurahishwa na umahiri wenu katika kuhakikisha ninakuwa salama” akasema Khalid wakitumia lugha ya kiingereza

“Khalid kwa kuwa umefika salama nadhani ningekupeleka chumbani kwako ukaoge kisha tupate chakula halafu mazungumzo yataanza”

“James Kasai amekwisha fika?akauliza Khalid

“James Kasai amekwisha wasili yuko chumbani kwake akipumzika.Utaonana naye baadae” akasema Melanie na kumpeleka Khalid katika chumba alichoandaliwa kisha akarejea sebuleni walikokuwa wale watu wawili waliokuja na Khalid.

“Madam sisi tumemaliza kazi yetu tuliyopewa ambayo ilikuwa ni kuhakikisha mgeni anafika hapa salama na sasa tunaweza kuondoka”akasema mmoja wa wale jamaa.

“Ahsanteni sana kwa kumfikisha mgeni

salama.”akasema Melanie na kumtaka Joyce dereva wake awapeleke wale wageni.

Baada ya Khalid kuoga akaelekea sebuleni ambako alikutana na James Kasai.Wakasalimiana kwa furaha

“Nimefurahi sana kukutana nawe James”akasema Khalid

“Mimi pia” akasema James

Melanie akawapeleka katika chumba cha chakula wakapata chakula cha usiku pamoja.Wakati wakipata chakula Edwin Mbeko

akawasili na kujumuika na akina Melanie mezani kwa chakula.

****

Ruby na Mathew waliwasili ofisi kuu ya SNSA wakashuka garini na kuelekea moja kwa moja katika ofisi ya Ruby ambako Mathew alikaribishwa kisha Ruby akatoka na kumfuata Edwin ofisini kwake.

“Karibu madam” akasema Edwin

“Edwin nataka kufahamu mahala mlikofikia hadi sasa katika kumtafuta Khalid” akasema Ruby

“Madam mpaka sasa bado hatujafanikiwa na mimi ninajiandaa kwenda kuungana na timu ya nje kuendelea na zoezi la kumsaka Khalid.Hatutalala leo hadi tuhakikishe Khalid amepatikana”

“Nataka nipate taarifa ya wataalamu wetu kuhusiana na namna tukio lile la kukatika mawasiliano lilivyotokea” akasema Ruby

“Madam awali tulidhani labda kuna mkono wa mtu katika tukio lile lakini baada ya wataalamu wetu kufanya uchunguzi wao wanasema kwamba ni hali mbaya ya hewa ndiyo iliyopelekea tukio lile kutokea” akasema Edwin

“Sawa Edwin.Namtaka mkuu wa idara ya ufundi ofisini kwangu mara moja” akasema Ruby na kuelekea katika ukumbi mkubwa ambako kazi zilikuwa zinaendelea.

“Naomba mnisikilize tafadhali” akasema Ruby na

watu wote wakaacha shughuli zao na kumgeukia Ruby.

“Asubuhi niliwaeleza kuhusiana na ujio wa Khalid Sultan Khalid na namna gani mtu huyo alivyo hatari kwa nchi yetu.Niliwaeleza kwamba mtu huyu anatoka IS na ni mtaalamu wa milipuko mikubwa na niliweka wazi hofu yangu kwamba kuna uwezekano mkubwa IS wanaandaa tena shambulio lingine kubwa hapa nchini ndiyo maana Khalid amekuja nchini.Pamoja na kujipanga vizuri sana kumfuatilia Khalid

lakini teknolojia imetuangusha na tumejikuta tukimpoteza Khalid bila kutarajia na sasa tuna kazi nyingine kubwa ya kumsaka Khalid na kujua mahala alipo.Lazima tufanye kila tuwezalo kuhakikisha tunampata Khalid.Uwezo huo tunao kwani tunao uwezo wa kuona asilimia tisini ya kamera zote za usalama zilizoko barabarani,tunao uwezo wa kudukua mitandao yote ya simu hapa nchini hivyo hatuna sababu yoyote ya kutufanya tushindwe kufahamu mahala alipo Khalid.Tumieni kila

tulichonacho katika idara yetu kuhakikisha Khalid anapatikana.Edwin anakwenda kuungana na timu ya nje kuendelea na zoezi la kutafuta mahala aliko Khalid na sisi tulioko hapa tuendelee pia na zoezi hilo.Tunakesha hapa usiku wa leo hakuna mtu atakayeondoka kwenda nyumbani hadi tuhakikishe Khalid anapatikana" akasema Ruby kisha akaelekea ofisini kwake.Mara tu alipoingia ofisini Fidelis mkuu wa idara ya ufundi akaingia Ruby akamchukua wakaelekea

katika chumba kidogo cha mazungumzo kilichokuwa pembeni ya ofisi ile ya Ruby.

“Fidelis wewe ndiye mkuu wa idara ya ufundi nataka uniambie nini hasa kilichotokea na kusababisha mawasiliano yakakatika hadi tukampoteza mtu muhimu kabisa?akauliza Ruby na Fideli akaanza kumuelezea kile alichokigundua katika uchunguzi wake.Wakati wakiendelea na mazungumzo akaingia Edwin na kumkuta Mathew akiwa ameketi sofani akamsalimu halafu akafungua

mlango wa kioo wa chumba walichokuwamo Ruby na Fidelis wakizungumza.

“Madam ninaondoka ninakwenda kuonana na vijana kuendelea na lile zoezi” akasema Edwin

“Sawa Edwin .Nataka mawasiliano ya mara kwa mara tafadhali”akasema Ruby na Edwin akatoka. Baada ya takribani dakika ishirini za mazungumzo Fidelis akatoa ofisini kwa Ruby.

“Watu wa idara hii hawajanifahamu vyema mimi ni nani”Ruby akamwambia

Mathew baada ya kutoka kuzungumza na Fidelis

“Huyu jamaa aliyetoka hapa muda mfupi uliopita anaitwa Fidelis ni mkuu wa idara ya ufundi.Baada ya tukio lile kutokea huyu jamaa na timu yake ndio waliochunguza kujua kilichotokea.Nilimuita hapa ili anieleze kwa kina nini hasa kilichotokea lakini maelezo anayonipa hayaingii akilini ni kama vile anampa maelezo mtu ambaye hana ujuzi wowote wa kompyuta.Kwa bahati nzuri hapa idarani hakuna anayejua

uwezo wangu katika mambo haya ya teknolojia ya kompyuta” akasema Ruby

“It’s time to show them who you real are.Mimi bado naamini kabisa kwamba kuna kitu hapa katika lile tukio” akasema Mathew

“Mathew ninataka kulishughulikia suala hili na nitakuomba univumilie hadi pale nitakapomaliza kazi yangu”

“Usijali Ruby endelea na kazi yako.Tunahitaji sana kuufahamu ukweli” akasema Mathew

“Thank you my love” akasema Ruby huku akitabasamu kisha akaanza kazi katika kompyuta yake.

****

Baada ya kupata chakula Melanie akawaongoza akina Khalid katika chumba cha mazungumzo.

“Khalid na James Kasai karibuni sana Tanzania karibuni sana Dar es salaam” akasema Melanie

“Melanie ninashukuru sana kwa mapokezi mazuri

sana hadi mkanifikisha hapa.Nilisema pale awali na ninarudia tena kwamba ninyi ni mahiri sana katika mipango yenu.Mnastahili pongezi kubwa.Ni mara yangu ya kwanza kufika Tanzania na sikutegemea kukutana na watu wenye ujuzi mkubwa namna hii kama ninyi.Kingine ambacho kilinipa mawazo mengi sana ni kama James Kasai angeweza kuingia hapa nchini kufuatia kutafutwa sana na nchi za Afrika mashariki kutokana na lile shambulio la hivi majuzi.Nilipoambiwa

kwamba tayari yuko hapa nchini sikuamini hadi pale nilipomtia machoni.Ninajisikia fahari kufanya kazi na watu kama ninyi.Kama mmeweza kufanikisha kumuingiza James Kasai nchini Tanzania licha ya ulinzi mkali ulioko mipakani na kila sehemu basi mnaweza kufanya kitu chochote hapa nchini" akasema Khalid

"Ahsante sana kwa pongezi Khalid.Tunao uwezo wa kufanya chochote hapa nchini lakini haya yote yanawezekana kwa sababu ya huyu mtu hapa" akasema

Melanie na kumshika bega Edwin

“Anaitwa Edwin Mbeko.Huyu ni mkurugenzi wa idara ya siri ya usalama wa ndani ya nchi.Yeye ndiye anayechukua nafasi kubwa katika haya yote yanayoendelea hivi sasa.Hata katika mipango yetu yote tutakayoipanga huyu ndiye hasa ambaye ataitekeleza” akasema Melanie

“Hongera sana Edwin.Kazi yako tumeiona.Ni kazi nzuri sana” akasema Khalid.

“Nadhani sasa tuendelee na mazungumzo” akasema Melanie

“Nmeelekezwa nije Tanzania na wakuu wangu kwamba kuna kazi ya kufanya lakini sijui ni kazi gani kwa hiyo ninyi ndio mnaotakiwa mnipe taarifa ni kitu gani hasa nimekuja kukifanya huku Tanzania” akasema Khalid na Melanie akampa ishara James Kasai aendelee.

“Jambo kubwa ambalo limetukutanisha hapa ni kujadiliana kuhusu mpango wa kuwaua marais wa

Tanzania na Congo kwa bomu la kujitoa mhanga” akasema James

Wakati mazungumzo ya kuhusu mpango wa kuwaua marais Dar Fabian Kelelo na Patrice Eyenga yakiendelea nyumbani kwa Melanie Davis, katika ofisi kuu ya SNSA Ruby aliendelea na zoezi la kujaribu kutafuta chanzo cha mawasiliano kukatika ghafla na kupelekea Khalid kupotea.Dakika arobaini zimekwisha pita toka alipoanza zoezi hilo.Mathew Mulumbi badi alikuwa ofisini

kwa Ruby akisubiri zoezi lile limalizike.Mawazo yake yalikuwa mbali sana.Kichwa chake kilijaa mawazo ya namna walivyoachana na Peniela.Alikumbuka historia yao walikotoka mambo waliyopitia na hadi walivyoachana.

“Mambo yanayokuja kichwani kwangu kuhusu mimi na Peniela ni kama ninatazama filamu lakini hii si filamu bali ni kitu cha kweli kabisa.Ni maisha halisi ambayo mimi na Peniela tumeyaishi.Tulikuwa na

mipango mingi sana ya siku za usoni lakini yote hatawezekana tena” akawazaMathew

“Sasa niko huru wa kuwa na mwanamke mwingine na kama nikiambiwa nichague basi Ruby anafaa sana kuchukua nafasi ya Peniela lakini je ni vipi kama yatamkuta kama yale ya Peniela je ataweza kuvumilia au nitakuwa ninamuumiza huyu binti malaika?Kila ninapomtazama Ruby ninapata mawazo mengi sana.Najua ananipenda na

mimi pia ninampenda lakini…….”

“Mathew ulikuwa sahihi”akasema Ruby na kumtoa Mathew mawazoni akasimama

“Unasemaje Ruby?akauliza

“Ulikuwa sahihi.Mawasiliano kukatika hakukusababishwa na hali ya hewa kama inavyodaiwa bali ni kitendo kilichofanywa na mtu kwa makusudi”

“Oh my God ! Unaweza ukafahamu nani aliyefanya hivyo?akauliza Mathew.Ruby

akaendelea kubonyeza kompyuta yake na baada ya dakika tatu akasema

“Tatizo hilo lilitokea katika stesheni 5” akasema Ruby na kufungua faili Fulani

“Stesheni 5 ni ya mtu anaitwa Edina Mkwena”

“Ruby are you sure? Mathew akauliza

“I’m sure”akasema Ruby

“Jambo hili lilifanywa kitaalamu sana lakini kwa bahati mbaya hawakujua kama mimi ni mtaalamu zaidi yao.Hawafahamu kama nimeanza kucheza na

kompyuta toka nikiwa na miaka minne na kwa maisha yangu yote ndicho kitu ambacho nimekuwa ninakifanya.Nilifanya vyema kutojitambulisha kwao uwezo wangu na sasa tumeanza kupata picha ya namna mambo yanavyokwenda katika idara hii" akasema Ruby

"Nilijua tu kwamba lazima jambo lile limefanyika kwa makusudi kabisa hasa ukiangalia mahala ambako mawasiliano yalikatikia kwenye mzunguko wenye barabara nne na baada ya

mawasiliano kurejea hatujui gari lile lilifuata barabara ipi.Mpaka hapa tayari tumeanza kupata mwanga kwamba kuna mtu ndani ya idara hii anahusika katika lile tukio.Yawezekana huyu amepandikizwa maalum kwa ajili ya kufuatilia kila kinachoendelea ndani ya hii idara na kuwapa taarifa hao waliomtuma.Yuko hapa kwa malengo maalum na inawezekana huyo ndiye aliyewapa taarifa kwamba Khalid anafuatiliwa na wakapanga wafanye vile

walivyofanya.Hawa watu kama nilivyokwambia kwamba ni watu makini sana na wanajua wanachokifanya.Wameotesha mizizi yao karibu kila sehemu muhimu ya serikali" akasema Mathew

"What are we going to do? Akauliza Ruby

"Tayari tumepata chanzo hivyo hatupaswi kwenda naye haraka.Tunachotakiwa kufanya ni kumchunguza kwa siri sana kila anachokifanya.Tufuatilie mawasiliano yake tujue anaowasiliana nao na

wanawasiliana nini,tufunge kamera za siri nyumbani kwake na kufuatiliakila kinachoendelea hapo kwake.Huyu ndiye atakayetuongoza kuelekea mahala walipo waliomtuma.Anza kwa kujenga naye urafiki.Muweke karibu yako ili iwe rahisi kumfuatilia” akasema Mathew na Ruby akainua simu akapiga stesheni 5 ambayo ni ofisi ya Edina lakini simu ikaita bila kupokelewa.Akapiga tena simu ikaita haikupokelewa.

“Hapokei simu” akasema Ruby na kumpigia mtu mwingine akamtaka akamuangalie Edina ofisini kwake.Baada ya dakika mbili simu ikaita Ruby akaipokea akajulishwa kwamba Edina hakuwepo ofisini kwake.Ruby akampigia simu mtu mwingine akamuita ofisini kwake akamtaka akamtafute Edina

“Nina wasiwasi kama atakuwepo bado mahala hapa” akasema Mathew

“Nilitoa maelekezo asiondoke mtu yeyote leo kwenda nyumbani hadi

tuhakikishe tumempata Khalid hivyo lazima atakuwepo hapa hapa ndani” akasema Ruby.

“Kwa mujibu wa taarifa nilizonazo ni kwamba Khalid anakuja nchini kuonana na James Kasai.Nashawishika kuamini kwamba mtandao huu ambao umemleta nchini Khalid ndio ambao unamleta na James Kasai hapa Dar es salaam.Huyu Edina ni muhimu sana kwetu kwa sasa kutusaidia kuufahamu mtandao huu” akasema Mathew

“Kwa nini tusimkamate tukamuweka ndani na kumfanyia mahojiano ya kina akateswa na akaeleza kila kitu anachokifahamu kuhusiana na mtandao wao na watu waliomtuma?akauliza Ruby

“Tungeweza kufanya hivyo lakini tutawastua na kuwapeleka mafichoni.Tumfuatilie taratibu na kwa karibu sana tutafika hadi kwa watu waliomtuma” akasema Mathew

Wakati wakiendelea na mazungumzo mlango wa ofisi ya Ruby ukafunguliwa

akaingia Yule jamaa ambaye alitumwa kwenda kumtafuta Edina.

“Madam nimezunguka kila kona Edina hayupo” akasema Yule jamaa

“Una hakika hayumo humu ndani?Ruby akauliza

“Hayupo.Nimetafuta kila sehemu hayupo” akajibu Yule jamaa na kutoka.

“Hayuko hapa.Tayari amekwisha ondoka” akasema Mathew

“Ameondokaje?akauliza Ruby na kuinua simu akapiga geti kuu akawauliza kama

Edina amepita pale getini usiku ule na kwenda nje akajibiwa kwamba hajapita pale kwani kila anayetoka lazima apitishe kadi yake ya ufunguo katika mashine iliyoko getini.

“Hata geti kuu wanasema hawajamuona akitoka” akasema Ruby

“Kuna mageti mangapi hapa ya kuingia na kutoka?

“Geti lililopo ni moja tu na ambalo kila mfanyakazi lazima apite ili ajulikane kama hayupo au yupo ndani.Kama hajaonekana getini basi lazima

atakuwa yuko humu humu ndani’

“Kama yuko humu ndani yuko wapi?akauliza Mathew

“Hapo ndipo ninapokosa majibu.Naomba unipe dakika mbili” akasema Ruby na kushuka hadi katika ukumbi ule mkubwa

“Samahani jamani naomba tusikilizane” akasema Ruby na watu wote wakaacha kazi wakamgeukia kumsikiliza

“Kuna mwenzetu mmoja ambaye haonekani humu ndani na taarifa ya geti kuu inaonyesha kwamba hajatoka

anaitwa Edina.Kuna yeyote anaweza akasaidia kujua mahala alipo?Kuna yeyote ambaye amemuona sehemu yoyote humu ndani?akauliza Ruby

‘Tafadhali kama kuna yeyote amemuoa au anajua mahala alipo anieleze ninamuhtaji sana kuna kazi ya muhimu nahitaji kumpatia sasa hivi” akasema Ruby na watu wakaanza kuulizana lakini hakuna aliyefahamu mahala alipo.

“Kuna yeyote anayefahamu nyumbani

kwake?akauliza Ruby na watu zaidi ya watano wakanyoosha mikono

“Naomba mmoja wenu anielekeze nyumbani kwake.Namuhitaji sana” akasema Ruby na dada mmoja akamuelekeza mahala anakoishi Ruby

“Ahsanteni sana.Endeleeni na kazi zenu.Kumbukeni kabla ya mapambazuko lazima tuwe tumempata Khalid Sultan” akasema Ruby na kurejea ofisini kwake.

“Mathew uko sahihi.Huyu Edina hayuko humu

ndani.Tayari amekwisha ondoka lakini sifahamu ameondokaje” akasema Ruby

“Yawezekana amekwenda mahala na atarejea tena”akasema Mathew

“Nimeelekezwa mahala anakoishi.Twende tumfuate nyumbani kwake yawezekana tukapata kitu muhimu cha kuweza kutusadia kumfahamu vyema huyu mtu” akasema Ruby wakaondoka kuelekea katika gari lake

SAA MOJA ILIYOPITA

Ofisi kuu ya SNSA ilikuwa katika heka heka kubwa kila idara ndani ya ofisi hiyo wakijaribu kutafuta sababu ya mawasiliano kukatika ghafla na kukwamisha zoezi la kumfuatilia Khalid Sultan Khalid.Wakati watu wanaohusika na masuala ya ufundi wakijitahidi kurejesha mawasiliano,Edwin akaingia katika chumba kilichojulikana kama chumba cha seva ambamo kulikuwa na kompyuta nyingi

kubwa.Hakuna aliyemjali kila mmoja alikuwa anashughulika akamfuata Edina aliyekuwa amesimama akiangalia kile kilichokuwa kinaendelea akamshika mkono na kumpa kijikaratasi.Edina akatoka mle ndani akaenda maliwato akakikunjua kile kikaratasi na kukisoma

“Baada ya mawasiliano kurejea nataka nikupeleke nyumbani ukahifadhi fedha zako wakiziona hapa wataanza kuulizana ulikozitoa.Jitahidi utokapo asikuone mtu nenda hadi

katika gari langu fungua mlango jifiche kiti cha nyuma halafu utanitumia ujumbe nitakupeleka nyumbani ukahifadhi mzigo wako na kukurudisha” ndivyo ulivyosomeka ule ujumbe

Mawasilinao yalirejea na kazi zikaendelea kama kawaida na baada ya muda mkurugenzi akawasili na kuzungumza na wafanyakazi na kisha likaanza zoezi la kumsaka Khalid Sultan.Wakati zoezi likindelea Edina akachukua bahasha yake iliyokuwa na fedha akatoka kama vile anaelekea

maliwato na kuelekea moja kwa moja katika maegesho ya magari ya wakuu wa idara,analifahamu gari la Edwin akafanya kama alivyoelekezwa akaingia katika kiti cha nyuma halafu akamtumia ujumbe Edwin kumjulisha kwamba tayari amekwisha ingia garini.Edwin akamuaga Ruby kisha akatoka akaingia garini na kutoka.Baada ya kutoka katika geti kuu Edina aliyekuwa amejificha kiti cha nyuma akaibuka na kukaa

“Ahsante sana Edwin kwa msaada huu mkubwa” akasema Edina

“Usijali Dina” akasema Edwin ambaye alionekana kutohitaji maongezi akafungua mziki kwa sauti ya juu

Walifika nyumbani kwa Edina wakashuka garini,Edna akamkaribisha ndani

“Edwin karibu ndani kutana na mdogo wangu anaitwa Stella.Huyu ndiye anayesoma chuo kikuu na ile fedha ni kwa ajili yake” akasema Edina.Edwin na Stella wakasalimiana.Dina

akamuandalia Edwin juisi ya matunda kisha akaelekea chumbani kuhifadhi zile fedha

“Nimefurahi kuonana nawe Stella.Dada yako amekuwa anatueleza sana sifa zako na bidii yako kubwa katika masomo” akasema Edwin

“Nashukuru sana” akasema Stella.

“Stella naomba maji ya kunywa tafadhali” akasema Edwin na Stella akainuka kwenda kumchukulia Edwin maji ya kunywa katika friji mara Edwin akaingiza mkono

katika mfuko wa koti na kutoa bastora iliyofungwa kiwambo cha kuzuia sauti na mara tu Stella alipogeuka akaizinga bastora na kuachia risasi iliyompata Stella kati kati ya paji la uso akaanguka.Sauti ya glasi kuvunjika ikamstua Edina aliyekuwa chumbani.

“Stella ! akaita Edina lakini hakujibiwa akafungua mlango wa chumba akatoka ili kuangalia kuna nini akakutana na risasi mbili zilizompata katikati ya paji la uso akaanguka chini.Edwin akawaongeza tena risasi ili

kuhakikisha hakuna anayebaki hai kisha akaingia ndani ya chumba alimotoka Edina akavaa glovu mikononi akafungua kabati kubwa la nguo akafungua droo ndogo akazikuta fedha ambazo Edina alikuwa amezihifadhi akazichukua na kutoka

“I’m sorry Dina” akasema Edwin na kuchukua simu za Edina na mdogo wake akachukua ufunguo akafunga mlango kwa nje akaondoka.

“Sasa nielekee kwa Melanie” akawaza Edwin

****

Mathew na Ruby waliwasili katika nyumba anayoishi Edina.Waliegesha gari mbele ya nyumba ile ambayo haikuwa na uzio wakaelekea mlangoni.Taa ya nje ilikuwa inawaka Mathew akagonga mlango lakini hakujibiwa.Akagonga tena lakini hakujibiwa.

“Inawezekana hayupo nyumbani’ akasema Ruby

“Kama hayupo itakuwa vizuri kwetu,tuingie ndani pengine tunaweza kupata kitu

cha kutusaidia” akasema Mathew na kuchukua vifaa vyake ambavyo humuwezesha kufungua kitasa au kufuli la aina yoyote ile kisha akaufungua ule mlango wa nyumba ya Edina.

“Jesus Christ ! akasema Mathew kwa mstuko na kwa haraka akatoa bastora yake

“Kuna nini Mathew?akauliza Ruby naye akaingia ndani

“Edina ?!! akasema Ruby kwa mstuko.Mathew akaingia kwa tahadhari katika vyumba vyote lakini hakukuwa na mtu

yeyote akarejea sebuleni akaigeuza miili ile ya Edina na mdogo wake

“Wameuawa usiku huu” akasema kisha wakaingia chumbani wakaanza kukagua kama wangeweza kupata kitu chochote cha kuwasaidia lakini hawakupata chochote wakatoka na kuondoka

“Hawa watu ni wakatili wakubwa sana.Baada ya kumtumia Edina wameamua kumuua kwani waliohofia labda angeweza kugundulika.Ni watu wenye kuchukua tahadhari kubwa

kila wakati.Ruby unapaswa uwe makini sana kwani watu hawa wana mtandao mkubwa na hata idara yako tayari wameotesha mizizi yao.Naamini Edina hayuko peke yale lazima kuna watu ambao bado wapo ndani ya idara”

“Mathew nimejikuta nikiingiwa na woga wa ghafla”

“Usiogope Ruby niko nyuma yako hakuna yeyote ambaye atathubutu kucheza na maisha yako” akasema Mathew.

“Tunaelekea wapi hivi sasa? Akauliza Ruby

“Turejee SNSA.Nahitaji kumuhoji Yule mkuu wa idara ya ufundi”

“Unadhani kuna kitu anakifahamu?akauliza Ruby

“Naamini hivyo.Kuna kitu anakifahamu kuhusu jambo hili” akasema Mathew

“Itanilazimu kutumia madaraka yangu ili ukamuhoji Fidelis kwani wewe si mfanyakazi wa SNSA lakini ni vipi endapo hatakuwa anafahamu chochote? Akauliza Ruby

“SNSA iko chini ya Rais na anafahamu hiki tunachokifanya hivyo hakuna yeyote atakayekuuliza kitu chochote.Umepewa madaraka hivyo lazima uyatumie.Usijali kuvunja taratibu katika kutafuta taarifa za muhimu” akasema Mathew

“Ruby umepewa idara nyeti sana uiongoze hivyo jifunze kufanya maamuzi magumu pale inapohitajika.Nina uhakika mkubwa kwamba huyu jamaa Fidelis kuna kitu anakifahamu kuhusu hiki kilichotokea.Ruby

idara yako imeingiliwa na kirusi kibaya sana.Una kazi kubwa ya kukiondoa kirusi hicho.Inaonekana tayari mabeberu hawa wamekwisha otesha mizizi katika idara yako na wanaitumia katika kufanikisha mipango yao na hii inakuweka katika hatari kubwa sana lakini usihofu nitakulinda" akasema Mathew

"Kwa hiki kilichotokea leo ninaamini hicho ukisemacho.Idara hii ilianzishwa kwa ajili ya usalama wa ndani wa nchi lakini naweza sema kwamba

bado haijafanya kazi yake ile inayotakiwa.Imekuwa ikitumiwa katika kufanikisha mipango mbali mbali miovu dhidi ya nchi yetu na mkosi ulianzia kwa Devotha.Kama utakumbuka huyu alikuwa ni wakala wa Mossad hapa nchini na ikaendelea hivyo hadi kwa aliyefuata aliitwa Tamar.Kuna kazi kubwa ya kuisafisha idara hii ili ifanye kazi iliyokususdiwa”akasema Ruby

“Umemtaja Devotha umenikumbusha mbali sana.Yuko wapi Yule mwanamke?akauliza Mathew

“Sifahamu yuko wapi labda wale walioko hapa nchini Gosu Gosu na Austin wanaweza wakafahamu mahala alipo.Sitaki kabisa kufahamu chochote kuhusu Yule mwanamke ninamchukia sana alitaka kuniua pasi na kosa” akasema Ruby na ukimya ukapita

“Najaribu kujiuliza Edina ametokaje pale ofisini wakati kuna geti moja tu? Nani kamuua? Akasema Ruby

“Usiumize sana kichwa Ruby niachie jambo hilo

tutapata majibu yake” akasema Mathew

“Tumekuwa na mambo mengi sana hata nimesahau kuuliza kuhusu Peniela.Nini kilitokea?Alikueleza chochote kuhusu Melanie Davis? Halafu mbona kaondoka haraka namna hiyo?Nilitegemea angelala hapa Dar es salaam kwa mume wake” akasema Ruby

“Peniela alikuja kwa jambo moja tu” akasema Mathew na kunyamaza kidogo

“Alikuja kuhitimisha ndoa yetu.Mimi naye basi tena”

“Mmeachana?! Ruby akashangaa

“Ndiyo” akajibu Mathew na kumsimulia Ruby kila kitu kilichotokea kati yake na Peniela

“Mathew I’m so sorry.I don’t know what to say” akasema Ruby

“Usijali Ruby haya ni mapito katika maisha”

“Sikutegemea kama mambo yangekuwa namna hii.Lakini Peniela amechukua maamuzi ya haraka sana” akasema Ruby

“Simlaumu Peniela kwa maamuzi aliyoyachukua kwani yote haya nimeyataka mimi mwenyewe.Nilichagua kazi badala ya familia.Nimewaumiza sana ana haki ya kuendelea na maisha yake bila mimi.Anahitaji mtu ambaye atampa furaha katika maisha yake jambo ambalo mimi nimeshindwa.Haya ndiyo maisha yangu na lazima niyakubali” akasema Mathew

“Kikubwa ambacho ninashukuru ameahidi kunisaidia kutafuta taarifa za

Melanie Davis.Kama akilifanikisha hilo atakuwa ametusaidia jambo kubwa sana” akasema Mathew

“Mathew you are mine now.Hakuna yeyote au chochote cha kunitenganisha nawe.Mimi ndiye hasa ninayestahili kuwa nawe.Mimi ndiye Yule ambaye niliumbwa kwa ajli yako.Ninakupenda zaidi ya ninavyojipenda mwenyewe.Ahsante Peniela kwa maamuzi haya uliyoyachukua ambayo yameniachia mimi uwanja wa kutawala.Sasa mpira uko

kwangu na katu siwezi kushindwa kufunga” akawaza Ruby

Walifika ofisi kuu ya SNSA wakaelekea ofisini kwa Ruby ambaye bila kuchelewa akapiga simu idara ya usalama ndani ya SNSA akawataka wamchukue Fidelis wampeleke katika chumba cha mahojiano namba 2 halafu akaelekeza kamera zote katika chumba hicho cha mahojiano namba mbili zizimwe.Baada ya dakika chache akataarifiwa kwamba Fidelis tayari amepelekwa katika chumba cha mahojiano

“Mathew mtu unayemuhitaji tayari amekwisha pelekwa katika chumba cha mahojiano” akasema Ruby na kumuongoza Mathew hadi katika chumba alimowekwa Fidelis.Mlinzi aliyekuwa mlangoni akaufungua mlango Ruby na Mathew wakaingia. Ruby akachomoa nyaya zote zilizounganishwa na kamera kwa tahadhari kwani hakuwaamini wafanyakazi wa idara ile.

“Mathew he’s all yours” akasema Ruby.Mathew akavuta kiti na kuketi.

“Madam what’s going on? Who is this guy? akauliza Fidelis

“My name is Mathew Mulumbi.Nitakuuliza maswali naomba unijibu kwa usahihi” akasema Mathew

“Huwezi ukaniuliza chochote.Wewe si mfanyakazi wa hapa na siwezi kukujibu chochote.Madam nini kinaendelea hapa?Kwa nini umenileta hapa?akauliza

Fidelis na kutaka kunyanyuka.

“Sit down ! akasema Mathew kwa ukali

“I’m not going to sit down.Wewe ni nani wa kunipa amri…aaaagghhhh !!!.” Fidelis hakumaliza sentensi yake akajikuta chini baada ya kupigwa kofi zito.Mathew akamfuata pale chini alipoanguka na kumtaka ainuke aketi kitini.Bila ubishi Fidelis akainuka na kuinua kiti ambacho nacho kilikuwa kimeanguka akaketi

“Jina lako nani?akauliza Mathew

“Fidelis Makweba”

“Unashughulika na nini hapa SNSA?akauliza Mathew

“Mimi ni mkuuwa idara ya ufundi ambayo kazi yetu ni kuhakikisha mifumo yetu yote inakuwa salama muda wote na kompyuta zote zinakuwa katika hali nzuri” akajibu Fidelis.

“Usiku wa leo wakati wa zoezi la kumfuatilia Khalid likiendelea mawasiliano yalikatika kati ya ofisi kuu na watu wetu waliokuwa

barabarani.Nini kilisababisha hali ile kutokea?akauliza Mathew na Fidelis akaanza kuelezea kiufundi tatizo lililotokea

“Hata mkurugenzi aliniita akaniuliza nikamueleza kila kitu kuhusiana na hiki kilichotokea” akasema Fidelis na Mathew akamgeukia Ruby

“Fidelis maelezo uliyonipa hayana ukweli wowote”akasema Ruby na Fidelis akaonyesha mstuko mkubwa.Ruby akaanza kumpa maelezo kuhusiana na kile

kilichotokea.Matone ya jasho yakaonekana usoni kwa Fidelis

“Wewe kama fundi mkuu lazima ufahamu kitu hiki” akasema Ruby na kuhitimisha maelezo yake

“Umesikia alichokisema mkurugenzi wako.Unakubaliana na maelezo yake?akauliza Mathew na Fidelis akawa kimya.Alijaribu kufungua midomo ikabaki inamcheza

“Ukimya wako ni jibu kwamba alichokisema mkurugenzi wako ni kitu cha

kweli kabisa” akasema Mathew na kumtazama Fidelis

“Khalid Sultan Khalid ni mtu hatari sana ambaye amekuja nchini kwa lengo la kupanga shambulio kubwa.Idara yenu imefahamu kuhusu ujio wake na kuweka mikakati ya kumfuatilia kujua alichokuja kukifanya hapa nchini vile vile kuwafahamu washirika wake.IS wana mzizi wao hapa nchini na sasa wanataka kusambaa katika bara zima la Afrika.Operesheni ile ya kumfuatilia Khalid ingetuwezesha kuwafahamu

washirika wake na mtandao mzima wa IS hapa nchini lakini kwa makusudi kabisa umeshiriki katika kukwamisha zoezi lile la kumfuatilia Khalid na sasa hatujui yuko wapi wala washirika wake ni akina nani.Kwa hiki ulichokifanya umeiweka nchi katika hatari kubwa na unajua adhabu wanayopewa watu kama wewe ambao wanahatarisha usalama wa nchi.Fidelis ninataka nikusaidie kukuondoa katika kitanzi hiki ulichojivisha lakini hadi pale utakaponieleza ukweli wote.Kwa nini ulisema

uongo kuhusu tukio lile?Kwa nini ulimdanganya mkurugezi wako? Tuanzie hapo” akasema Mathew.Fidelis hakujibu kitu alibaki kimya

“Fidelis muda unakwenda naomba tafadhali unijibu maswali niliyokuuliza” akasema Mathew Fidelis hakujibu kitu

“Fidelis nafahamu hauko peke yako katika jambo hili.Nani wengine ulishirikiana nao?akauliza Mathew lakini bado Fidelis aliendelea kuwa kimya

“Fidelis unapokaa kimya unazidi kupoteza nafasi ya kusaidiawa” akasema Mathew

“Labda ngoja nikufahamishe kitu Fidelis.Tatizo hili lilianzia stesheni 5 ambayo ni ya Edina.Naamini jambo hii ulilifahamu vizuri lakini ukakubali kupindisha ukweli.Kwa taarifa yako ni kwamba baada ya kugundua kwamba ni Edina ambaye alifanya kitendo kile nilianza kumtafuta bila mafanikio nikaamua kumfuata nyumbani kwake nimekuta

ameuawa”akasema Ruby na sura ya Fidelis ikaonyesha mstuko mkubwa

“Watu waliomtumia Edina wamemuua kikatili.wewe unayo nafasi nzuri ya kusaidiwa yasikukute kama yaliyomkuta Edina lakini tutakusaidia tu pale ambapo utatueleza ukweli nani alikutuma useme uongo kuhusiana na tukio lile?akauliza Mathew na Fidelis alionyesha uoga mkubwa

“Fidelis hii ni nafasi pekee ya kukuokoa umeipata na

kama ukishindwa kuitumia basi tutakukabidhi kwa vyombo vya dola ufunguliwe mashtaka ya kuhatarisha usalama wa taifa.Naomba ufunguke tafadhali” akasema Mathew lakini Fideli bado alikuwa kimya

“Fidelis una watoto?akauliza Mathew na swali lile likaonekana kumstua Fidelis na akaikumbuka sauti ya Edwin masikioni

“Endapo ukithubutu kufunguka na kusema ukweli kuhusiana na tukio hili hutaiona tena familia yako !

Fidelis aliyakumbuka maneno haya aliyoambiwa na Edwin akahisi baridi

“Fedha alizonipa Edwin zimeniponza natamani niwaeleze ukweli hawa watu lakini nahofia familia yangu kwani Edwin alinionya nisithubutu kusema ukweli kuhusu jambo lile kwani ama sivyo nitaikosa familia yangu. Natakiwa kuendelea na msimamo wangu wa kutokusema chochote.Mambo tayari yameshaharibika” akawaza Fidelis

“Fidelis ninaanza kuchoshwa na tabia yako ya kujifanya bubu.Hii ni mara ya mwisho ninakuuliza nani waliokutuma useme uongo kuhusu kukatika kwa mawasiliano katika zoezi muhimu? akauliza Mathew bado Fidelis alikuwa kimya

“Hujanifahamu vyema kijana, mimi huwa sipendi mzaha ninapokuwa kazini” akasema Mathew na kunyanyuka akamfuata Fidelis akamuinua akampeleka katika nguzo akachukua kamba akamfunga mikono nyuma ya

nguzo na miguu akaikaza barabara kwa kamba.

“Kwa kuwa umekataa kufunguka kwa njia ya amani sasa tunaingia katika njia ya pili ya kutumia nguvu.Kabla sijaanza zoezi langu ninakupa nafasi ya mwisho ya kunieleza ukweli” akasema Mathew.Fidelis alikuwa anatetemeka mwili lakini hakusema chochote.Bado aliendelea na msimamo wake wa kukaa kimya.Mathew akachukua kopo dogo la gesi akaliwasha kisha akaanza kuunguza vidole vya mikono

“Aaaaaaghhhh !! Fidelis akapiga ukulele mkubwa

“Nani alikutuma?akauliza Mathew lakini Fideli hakujibu kitu aliendelea kulia huku akihisi maumivu makali.Mathew akamchoma tena na gesi lakini bado Fidelis aliendelea kugugumia maumivu makali bila kusema chochote

”This isn’t working” akasema Mathew na kuchukua mashine ndogo ya umeme.

“Fidelis mimi ni mtu mbaya sana kama ukinifanyia mchezo.Unaonekana

kunichezea na mimi sitaki mchezo” akasema Mathew na kuiwasha mashine ile akamchoma Fidelis kwa umeme akaanza kutetemeka Mathew akaizima

“Uko tayari kuzungumza? akauliza Mathew lakini Fidelis aliendelea kuwa kimya

“Huyu bazazi anacheza na mimi” akawaza Mathew na kuitupa ile mashine ya umeme

“C’mon Fidelis tell me the truth !! akasema Mathew.Fidelis hakufumbua mdomo wake kutamka chochote.Mathew akazidi

kukasirika akaanza kumporomoshea Fidelis magumi mazito sehemu mbali mbali za mwili wake.Ndani ya muda mfupi uso wa Fidelis haukuwa ukitazamika ulikuwa umeloa damu.Ruby akamfuata na kumzuia Mathew asiendelee kumpiga

“Mathew imetosha.Umekwisha muumiza sana.Bado tunamuhitaji atupe taarifa muhimu” akasema Ruby.Bado Mathew aliendelea kumtazama Fidelis kwa hasira.

“Fidelis ! Fidelis ! akaita Ruby lakini Fidelis hakuitika alikuwa anamwagika damu mdomoni na alionekana hana fahamu.Haraka haraka Ruby akafungua mlango na kumtaka Yule mlinzi aliyekuwa mlangoni akawaite watu wa afya haraka sana.

“Mathew ulitaka kumuua kabisa huyu mtu” akasema Ruby

“Bado nina hasira naye.Hawajui nimepitia mambo gani hadi kufanikiwa kuipata taarifa ile muhimu ya Khalid lakini kwa fedha chache

wanazopewa wanadiriki kuvuruga misheni yetu na kuhatarisha usalama wa nchi.Watu kama hawa si wa kuwavumilia hata kidogo ! akafoka Mathew

Mlango ulifunguliwa na watu wanne wakaingia wakiwa na machela.Wakamfungua Fidelis wakampakia katika machela na kuondoka naye.

“Mathew nafahamu una hasira sana na watu hawa lakini nakuomba jitahidi kujizuia kutumia nguvu kupitiliza kwani ugeweza kumuua Fidelis na ungeniweka

mimi katika matatizo” akasema Ruby

“I’m sorry.Ni kweli nilikuwa na hasira naye sana.Huyu jamaa anafahamu kila kitu lakini anaogopa kusema.Yuko tayari kuvumilia mateso makali kwa ajili ya kuwaficha watu hao waliomtuma” akasema Mathew

“Baada ya kushindwa kupata taarifa kutoka kwa Fidelis nini kinaendelea?akauliza Ruby

“Tayari tunaye mtu ambaye anahusika katika

mpango ule wa kuvuruga zoezi la kumfuatilia Khalid.Fidelis anafahamu nani aliyemtuma lakini anamficha.Kwa sasa yeye ndiye pekee anayeweza kutueleza ukweli.Tumsubiri atakapozinduka tutaendelea naye lazima atueleze kila kitu anachokifahamu” akasema Mathew

****

Mishale ya saa ilizidi kuyoyoma na nyumbani kwa Melanie Davis bado kikao kiliendelea.Melanie na James

Kasai walimueleza Khalid Sultan Khalid mpango wao wa kuwaua marais wawili kwa kutumia bomu.Khalid baada ya kuyasikia mawazo yao aliyakubali na kukubaliana na pendekezo lao kwamba bomu litakalotumiwa kuwaua marais hao wawili liwe la kujitoa mhanga.Alieleza aina ya bomu linalohitajika,namna atakavyolitengeneza na madhara yakayoweza kuletwa na hilo bomu.Baada ya watu wote kuzungumza juu ya nafasi zao katika mpango ule ikafuata zamu ya Edwin

Mbeko.Huyu ndiye ambaye alitegemewa kumaliza mchezo wote .Mpango ule wote ulimtegemea yeye ili ukamilike

“Katika kuukamilisha mpango huu nitafanya hivi.Nitahitaji mtu kwa ajili ya kujitoa mhanga.Mtu huyo ataingizwa uwanja wa ndege akiwa amevaa mavazi ya askari wa kutuliza ghasia.Mara nyingi askari hawa huvaa fulana nene za kujikinga na risasi lakini huyu wa kwetu fulana yake haitakuwa kwa ajili ya kujikinga na risasi bali litakuwa ni bomu.Hakuna

ambaye atamtilia shaka mtu huyo kuwa si askari hivyo atajitahidi kuwasogelea marais na akiwakaribia umbali Fulani atajilipua” akasema Edwin na kufafanua namna atakavyomuingiza ndani ya uwanja mtu huyo atakayevaa mavazi ya askari polisi na kubeba bomu.Kila mmoja akatoa mawazo yake kuhusiana na wazo lile la Edwin na baada ya majadiliano wakafikia makubaliano.Khalid aliahidi kumleta haraka sana nchini mtu ambaye angeweza kubeba

bomu hilo na kujitoa mhanga.Baada ya kufikia makubaliano Edwin Mbeko akaondoka kurejea ofisi kuu ya SNSA.

Mara tu alipoingia ndani ya ofisi zao akakutana na hali isiyo ya kawaida.

“Kuna nini hapa?Mbona watu wako namna hii?akauliza Edwin na kuelezwa kile kilichomtokea Fidelis.Edwin akahisi miguu ikimtetemeka kwa mstuko alioupata.Hakutegemea kama Fidelis angeweza

kugundulika.Akaelekea ofsini kwake na kukaa juu ya meza

“Huyu mwanamke amegunduaje kama Fidelis anafahamu kilichotokea?Kama ameweza kugundua mawasiliano yalikatwa makusudi basi lazima atakuwa amefahamu nani aliyefanya hicho kitendo.Nilifanya jambo zuri sana kumuua Edina.Kwa sasa natakiwa kumuondoa Fidelis pia halafu nianze kushughulika na huyu mwanamke kwani nisipomshughulikia mapema anaweza akaharibu mipango

yetu yote” akawaza Edwin na kuelekea sehemu ya afya alikokuwa amelazwa Fidelis.Tayari alikwisha pata fahamu na Edwin alipoingia akamtambua mara moja

“Fidelis ! akasema Edwin

“Edwin ! akasema Fidelis kwa sauti dhaifu.

“Nini kimetokea Fidelis?akauliza Edwin

“Annabel anafahamu..aagh ! akasema huku akigugumia kwa maumivu

“Anafa…fahamu kila kitu” akasema Fidelis

“Umemueleza chochote? Akauliza Edwin na Fidelis akatingisha kichwa kukataa

“Vizuri sana.Nimekwisha ita gari la wagonjwa linakuja tunakupeleka hospitali kuu ya Mtodora ukapate matibabu makubwa” akasema Edwin kisha akafungua mlango akachungulia nje kama kuna mtu halafu akarejea ndani akachukua mto akamgandamiza Fidelis kwa nguvu pale kitandani.Fidelis alianza kuhangaika kutafuta hewa lakini tayari mwili wake ulikwisha kuwa dhaifu hivyo

hakuweza kushindana na Edwin.Baada ya muda Fidelis akatulia Edwin akatoa ule mto na kumtazama tayari Fidelis hakuwa na uhai.

“I’m sorry Fidelis” akasema Edwin na kuweka kitanda vizuri halafu akafungua mlango na kutoka mbio akiita madaktari ambao walifika kwa haraka sana kuangalia kuna nini.Haraka haraka wakampima lakini tayari Fidelis alikwisha fariki.Edwin akionekana kuwa na hasira akaelekea katika

ukumbi ambako kazi zilikuwa zinaendelea.

“Naombeni mnisikilize ndugu zangu ! akasema Edwin na watu wote wakamgeukia.

“Kuna taarifa mbaya nimewaleteeni.Mwenzetu,ndugu yetu Fidelis amefariki dunia muda mfupi uliopita ! Sura zote zikaonyesha mstuko mkubwa kwa taarifa ile

“Nimejulishwa kwamba mkurugenzi wetu mpya akiwa na mtu ambaye ameambatana naye ambaye si mfanyakazi wa idara yetu walimuita Fidelis katika chumba cha mahojiano

na kisha wakamlazimisha aseme tukio lile la kukatika kwa mawasiliano lilifanywa makusudi.Fidelis alikataa na ndipo alipoanza kupigwa.Huu ni unyama mkubwa amefanyiwa Fidelis.Mkurugezi amevunja kanuni za idara kwanza kwa kumuingiza ofisini mtu ambaye si mfanyakazi wa idara hii ya siri ya serikali lakini pili mtu huyo ambaye hatumfahamu ni nani amesababisha kifo cha mwenzetu.Hatuwezi kulikubali jambo hili.Mkurugenzi huyu ana siku ya pili katika ofisi na

tayari ameanza kuleta humu ndani watu wasiohusika nina mashaka naye sana kama anaweza akaongoza idara hii nyeti kabisa kwa nchi.Ndugu zangu nchi kwa sasa inatutegemea sana sisi hivyo hatuwezi kuongozwa na mtu kama huyu katika wakati huu.Kanuni zetu ziko wazi kwamba wafanyakazi wa idara wanao uwezo wa kumuondoa katika ofisi kwa muda wa siku saba mkuu wa idara endapo ataonekana kushindwa kumudu majukumu yake vyema au kuvunja kanuni na

taratibu za idara au kuwa kikwazo katika kufanikisha mambo muhimu kwa usalama wa nchi.Katika siku saba hizo suala la kuondolewa ofisini mkuu wa idara litafikishwa kwa Rais kujadiliwa na kisha kutolewa maamuzi.Nyote mnazo kanuni na mnazifahamu hivyo basi kwa kitendo alichokifanya mkurugenzi leo amevunja kanuni na kukwamisha zoezi la kumtafuta Khalid Sultan kwani Fidelis ni mmoja wa watu ambao tunawategemea sana hapa katika idara.Hata

lilipotokea lile tatizo la kukatika kwa mawasiliano yeye ndiye aliyeshughulika na timu yake na wakafanikiwa kurejesha tena mawasiliano.Ninawaomba mniunge mkono tumuondoe mkurugenzi katika nafasi yake mara moja ili zoezi la kumtafuta Khalid liendelee usiku huu" akasema Edwin na watu wote wakaonekana kukubaliana naye.

"Ahsanteni sana kwa kuniunga mkono.Sasa ninakwenda kumuondoa mkurugenzi ili asiendelee

kutuvuruga” akasema Edwin na kuelekea katika ofisi ya Ruby

Ruby akiwa katika ofisi yake na Mathew alijulishwa na daktari mkuu wa idara kwamba Fidelis amefariki dunia.Ilikuwa ni taarifa iliyomstua sana Ruby na kumfanya aweke mezani mkono wa simu

“Kuna nini Ruby mbona umestuka sana?

“Nimetaarifiwa na daktari mkuu kwamba Fidelis amefariki dunia”

“That’s not true !

“Ni kweli Mathew.Fidelis amefariki dunia” akasema Ruby

“Imetokeaje?Nini kimesababisha kifo chake?akauliza Mathew na kabla Ruby hajajibu mlango ukafunguliwa akaingia Edwin Mbeko akiwa ameongozana na watu wanne wenye silaha

“Edwin umerejea.Mambo yamekwendaje huko?Kuna mafanikio yoyote?akauliza Ruby

“Madam Annabel sijaja hapa kwa ajili ya jambo hilo”

akasema Edwin na Ruby akaonekana kukasirika

“Nini kimekuleta hapa basi?

“Madam naamini umepata taarifa za kifo cha ghafla cha Fidelis mmoja wa wataalamu wetu mahiri kabisa ambaye amekuwa na mchango mkubwa mno katika kufanikisha shughuli zetu mbali mbali”

“Ndiyo nimejulishwa”

“Nimejulishwa kwamba kifo cha Fidelis kimesababishwa na kipigo

ambacho wewe na huyu mtu wako mmempiga” akasema

“Edwin hukuwepo ofisini wakati jambo hilo linatokea hivyo basi unatakiwa utulie uulize na ueleweshwe nini kimetokea?akasema Ruby

“Madam sina muda wa kuuliza wakati kila kitu kiko wazi nimekuja hapa kwa jambo moja tu.Kwa niaba ya wafanyakazi wengine wa idara hii nimetumwa kukujulisha kwamba kwa kitendo hiki ulichokifanya leo umevunja kanuni kwanza kwa kumuingiza ndani ya ofisi hii

nyeti mtu ambaye si mfanyakazi wa idara.Hilo ni moja ya jambo lisiloruhusiwa kabisa kwani ofisi hii ina siri nyingi za nchi.Pili kwa kusababisha kifo cha mfanyakazi wa idara.Kwa mujibu wa kanuni zetu wafanyakazi wanayo madaraka ya kumuondoa mkurugenzi katika ofisi yake kwa siku saba hivyo kwa kutumia kanuni zetu kwa niaba ya wafanyakazi wote ninakuondoa katika nafasi yako na suala lako linapelekwa kwa Rais kwa ajili ya maamuzi.Kuanzia sasa

kabidhi kila kitu cha idara na hutakiwi kuonekana hapa katika idara kwa muda wa siku saba na utarejea hapa pale Rais atakapokwambia hivyo” akasema Edwin na Ruby akacheka kidogo

“You can’t be serious Edwin”

“I’m very serious madam” akasema Edwin

“Aliyeniweka katika nafasi hii ni Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania wewe huna mamlaka yoyote ya kuniondoa mimi katika nafasi yangu ! akasema Ruby

“Ni kweli madam sina uwezo huo lakini kanuni ambazo zimetiwa saini na Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania ndizo zinazokuondoa”

“No I won’t leave ! akasema Ruby kwa ukali

“Madam tafadhali usisababishe nguvu ikatumika kwani kanuni zinaelekeza nguvu inaweza ikatumika vile vile kukuondoa.Tafadhali kabidhi kila kifaa cha idara sasa hivi” akasema Edwin

“Just do it ! Mathew akamwambia Ruby

“No I can’t ! akasema Ruby

“Wape kila kitu chao tuondoke hapa kwa amani” akasema Mathew na Ruby akatoa kadi yake ya ufunguo bastora na vifaa vingine akaviweka mezani

“Ahsante sana madam Annabel” akasema Edwin huku akikusanya vifaa vile.Ruby akaichukua kompyuta yake na kuiweka katika mkoba.

“Madam kopyuta hiyo huwezi ukaichukua hadi ikaguliwe tujiridhishe kama

haina siri za idara” akasema Edwin

“Nimekuwa hapa siku mbili tu sina siri zozote za idara” akasema Ruby kwa ukali

“Huo ni utaratibu madam” akasema Edwin

“Ruby pakia kompyuta yako na vifaa vyako vingine tuondoke ! akasema Mathew

“And you,who are you? Akauliza Edwin huku akimtazama Mathew kwa hasira

“Mimi ni mtu ambaye hupaswi kumfahamu ! akajibu Mathew

“Usijibu kwa dharau ndugu ninao uwezo wa kuamrisha ukawekwa ndani sasa hivi.Wewe si mfanyakazi wa hapa na huruhusiwi kuwepo katika ofisi hii ! akafoka Edwin

“Bwana mdogo usinijaribu.Sipendi kujaribiwa ! akasema Mathew kwa ukali huku akimsogelea Edwin

“Okay guys tusilifanye suala hili likawa kubwa.Edwin the office is yours now.Please

make sure you find Khalid Sultan” akasema Ruby

“Yes madam we will find him” akajibu Edwin

“Thank you for everything.I hope we’ll meet again soon” akasema Ruby na kumshika Mathew mkono wakatoka.Hakumuaga mfanyakazi yoyote wa idara ile wakaelekea hadi katika gari lake wakaingia na kuondoka.

“Mathew mimi sijaelewa hiki kilichotokea ! Bila wewe kunilazimisha nikubali kamwe sikuwa tayari kutoka mle ofisini.Nimepewa ofisi na Rais

wa jamhuri ya muungano wa Tanzania nawezaje kuondolewa kienyeji namna hii na mtu asiye na hadhi yoyote?akauliza Ruby akiwa amekasirika.

“Ruby ni kweli umepewa ofisi na Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania lakini idara hii ya SNSA tayari imekwisha ota mzizi mkubwa wa mabeberu na umeondolewa makusudi kabisa kwani tayari umeanza kuonekana kikwazo kwao.Zoezi la kumfuatilia Khalid limekwamishwa makusudi kabisa na aliyefanya

kitendo kile ameuawa.Pili ni kifo cha Fidelis.Nina mashaka sana kama kipigo kile nilichompiga ndicho kimesababisha kifo chake”

“Unadhani Fideli ameuawa?akauliza Ruby

“Ndiyo.Yeye pia aliufahamu ukweli kuhusiana na kukatika kwa mawasiliano wakati wa lile zoezi la kumfuatiliaKhalid na kama ilivyokuwa kwa Edina naye pia ilibidi aondolewe haraka.Nina uhakika mkubwa ameuawa.Ninayafahamu haya mambo” akasema Mathew

“Wameamua kutumia kanuni ili kukuondoa na mipango yao iendelee.Nilikwisha liona hilo na ndiyo maana nikakutaka ukabidhi kila kitu chao na tuondoke kwani bila kufanya hivyo yangeweza kuibuka mambo mengine makubwa zaidi.SNSA ya sasa si ile ambayo ilianzishwa kwa malengo ya kulinda usalama wa nchi.Imekuwa ni sehemu ya kuhatarisha usalama wa nchi na hilo limedhihirika usiku wa leo.Zoezi muhimu sana la kumfuatilia Khalid

limeshindwa kufanikiwa.Edina na Fidelis hawako peke yao ndani ya SNSA lazima upo mtandao mkubwa”

“Sasa tutafanye nini Mathew? Rais atanielewaje akisikia hiki kilichotokea?

“Rais anakuamini sana lakini kwa misheni hii tutaiendesha sisi wenyewe bila kutegemea SNSA.Tutamsaka Khalid na kuhakikisha tunampata vile vile James Kasai.Nina uhakika mkubwa tutawapata naomba uniamini”

“Mathew ninakuamini sana lakini hapa tulipo

tumekwama.Tutawezaje kujikwamua kutoka katika mkwamo huu?akauliza Ruby

“Ahsante kwa kuniamini.Endelea kuniamini na tutalimaliza suala hili” akasema Mathew

Mara tu baada ya Mathew na Ruby kuondoka,Edwin akampigia simu Dr Fabian Kelelo akamjulisha kile kilichotokea na hatua walizozichukua kuhusu Ruby lakini hakumueleza kitu chochote kuhusu Khalid.

“Edwin kwa nini ukachukua maamuzi kama

hayo bila kunishirikisha kwanza mimi?akauliza kwa ukali Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais nililazimika kufanya vile kwa sababu tayari wafanyakazi walikwisha goma kuendelea kufanya kazi na madam Annabel.Hata kanuni zinaeleza hivyo mheshimiwa rais” akasema Edwin na Dr Fabian akashusha pumzi

“Sawa niachie suala hili nitalishughulikia kama kanuni zinavyoelekeza” akasema Dr Fabian na kukata simu akampigia Ruby

“Rais anapiga simu” Ruby akamwambia Mathew

“Tayari amekwisha elezwa kila kitu na Edwin” akasema Mathew na kumtaka Ruby apokee ile simu

“Mheshimiwa Rais” akasema Ruby

“Ruby nimepokea simu kutoka kwa Edwin muda mfupi uliopta amenipa maelezo ambayo yamenistua sana.Nini hasa kimetokea?

“Mheshimiwa Rais kwa sasa siwezi kukueleza chochote naomba unipe muda ili

nikutane nawe tuzungumze kuhusiana na suala hili”

“Alichokisema Edwin kwamba umesababisha kifo cha mfanyakazi wa SNSA ukishirikiana na mtu ambaye si mfanyakazi wa idara ni kweli?

“Ni kweli mheshimiwa Rais” akasema Ruby

“Kwa nini Ruby?Kwa nini ukafanya hivyo?Alichokifanya Edwin ni kitu sahihi kabisa.Ulivunja kanuni na wakalazimika kukuondoa kwani wafanyakazi wote hawakuwa tayari kuendelea

kufanya kazi nawe.Hata hivyo niachie suala hili nitalishughulikia.Kanuni zinasema ni siku saba utakaa nje ya ofisi na baada ya hapo utarejea kazini”

“Sawa mheshimiwa Rais nitasubiri kwa siku hizo saba”

“Ni nani uliyekuwa naye ofisini ambaye anatajwa kushiriki kumuua mfanyakazi?

“Ni Mathew Mulumbi mheshimiwa Rais?

“Mathew Mulumbi !! Dr Fabian akashangaa

“Ndiyo mheshimiwa Rais nilikuwa na Mathew”

“Huyu mtu ametokea wapi na kuja kuleta matatizo makubwa namna hii?Kila sehemu alipo huyu jamaa ni matatizo matupu ! I’m sorry to say this but I don’t like that guy ! akasema Dr Fabian kwa ukali na ukapita ukimya kisha akasema

“Nenda kapumzike Ruby tutazungumza zaidi kesho.Nitahitaji nisikie pia upande wako kujua nini hasa kilitokea”akasema Dr Fabian na kuagana na Ruby

Mathew na Ruby walifika nyumbani tayari ilikwisha

kuwa usiku mwingi.Wakati Ruby akiwa bafuni anaoga Mathew akaenda ofisini kwake akafungua kasiki akatoa kompyuta yake na kumpigia simu Habiba Jawad

“Mathew habari yako.Unaonekana umechoka sana leo” akasema Habia

“Ni kweli mama siku imekuwa ndefu sana na mambo yaliyojitokeza ni mengi pia”

“Naamini umefanikiwa kumuona Khalid na kumfuatilia” akasema Habiba

“Kuna tatizo limejitokeza mama wakati wa kumfuatilia Khalid” akasema Mathew na kumsimulia Habiba kilichotokea

“Mathew usalama wa nchi yako uko hatarini hivi sasa.IS wanapanga kufanya shambulio kubwa lakini bado sijajua ni shambulio gani na wapi lakini fahamu kuna shambulio kubwa linaandaliwa.Misheni hiyo niliyokutuma ni mtihani kwako kwani ukifaulu basi utakuwa umefuzu kwenda kufanya misheni nyingine kubwa zaidi.Endapo

utashindwa na IS wakishirikiana na James Kasai wakafanikiwa kutekeleza shambulio lao utanipa mashaka kama utaweza misheni nyingine kubwa inayokusubiri.Hawa jamaa wana mtandao mkubwa sana usimuamini mtu yeyoe kuanzia sasa.Fanya wewe mwenyewe kila kitu.Umenielewa Mathew?

“Nimekuelewa mama”

“Vizuri.Nategemea kesho utakaponipigia simu uwe na majibu mazuri ya kunipa.Ninataka uonyeshe

umahiri wako na usitegemee mimi kukupa kila taarifa”

“Nimekuelewa mama” akasema Mathew na kuagana na Habiba

“Habiba Jawad yuko sahihi.Nimetetereka sana.Natakiwa kurudi kuwa Mathew Mulumbi wa kipindi kile.Mambo yaliyotokea leo hayakupaswa kutokea.Nilipaswa hadi muda huu niwe tayari na taarifa za mahala alipoKhalid na kama James Kasai amekwisha ingia nchini lakini mpaka sasa sina taarifa zozote .Sifahamu alipo

Khalid wala James”akawaza Mathew na kugonga meza

“Kuanzia kesho jiji hili halitakalika.Mathew Mulumbi will be back.Siwezi kuchezewa na magaidi kiasi hiki” akawaza Mathew na kurejea chumbani kupumzika

****

Saa kumi na mbili za asubuhi simu ya rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania Dr Fabian Kelelo iliita akaunyoosha mkono na

kuichukua akatazama mpigaji sura ikabadilika

“Jenerali Akiki ! akasema kwa sauti ndogo akiwa amekunja ndita

“Anataka nini huyu jamaa asubuhi yote hii?Huyu ni mtu ambaye sitaki kabisa hata kuisikia sauti yake ! akawaza Dr Fabian akiitazama simu ile ikiita na kukatika ikaanza kuita tena

“Ngoja nimsikilize anachotaka kuniambia.Akiniletea dharau zake leo hii hii nitapelekea majeshi Uganda nikamchakaze

vibaya sana ! akawaza Dr Fabian na kuipokea simu ile ya Jenerali Akiki.

“Mheshimiwa Akiki habari za asubuhi” akasema Dr Fabian

“Dr Fabian samahani sana kwa simu hii ya asubuhi ambayo hukuwa umeitarajia”

“Ni kweli sikutarajia kabisa kupokea simu yako.Unasemaje Jenerali Akiki?

“Dr Fabian nimekupigia tuzungumze kidogo mambo ya msingi.Nafahamu hasira ulizo nazo juu yangu na ndiyo

maana hata mara ya mwisho tulipozungumza simuni mazungumzo yetu hayakuisha vizuri.Dr Fabian Uganda na Tanzania hatupaswi kufikia hatua hii tuliyofika.Sisi si majirani tu bali ni ndugu.Uganda tunapolia wa kwanza kusikia kilio chetu ni Tanzania na Tanzania inapolia wa kwanza kusikia kilio chao ni Uganda.Mheshimiwa rais naomba hiki kilichotokea siku chache zilizopita kisivuruge mahusiano mazuri ya kindugu kati ya nchi zetu hizi mbili”

“Jenerali Akiki sina imani kama hayo unayoyasema yanatoka moyoni.Kama ungetambua Tanzania na Uganda ni ndugu usingethubutu kumuacha James Kasai akaishi Uganda ! Yote haya yanatokea kwa sababu serikali yako inamuhifadhi James Kasai na sasa anajulikana kama gaidi James Kasai ! akasema Dr Fabian kwa sauti ya ukali

“Mheshimiwa Rais ni suala hilo ambalo limenifanya nikupigie simu asubuhi hii”

“Nini unataka kuniambia?akauliza Dr Fabian

“Ninataka suala hili limalizike hivyo nataka tuwe na kikao cha pamoja kati yako na Rais wa jamhuri ya kidemokerasia ya Congo bwana Patrice Eyenga mapema sana ikiwezekana hata kesho .Nataka tukae tuzungumze na tumalize suala hili kindugu.Katika kikao hicho tutazungumza mengi na kubwa ni kuhusu James Kasai” akasema Jenerali Akiki

“Jenerali Akiki kwa muda mrefu umekuwa ukipigiwa

kelele sana na nchi za Rwanda na Congo kuhusu James Kasai lakini wewe na serikali yako mmekuwa mkikana kabisa James kuwepo nchini Uganda na matokeo yake ndiyo haya yaliyotokea hivi majuzi.Unasema unataka kukaa nasi tuzungumze kitu gani kipya unataka kutueleza ambacho hujawahi kutueleza? Akauliza Dr Fabian

“Dr Fabian ninataka tulimalize hili suala ili kuepusha nchi zetu kuingia katika machafuko ambayo

wanayoathiriwa nayo ni raia wetu”

“ Jeneral Akiki kitu pekee ambacho tunakihitaji kwa sasa na ambacho kinaweza kutuleta mezani kwa mazungumzo ni kujua mahala alipo James Kasai” akasema Dr Fabian

“Hicho ndicho kikubwa ambacho ninataka kuzunguza nanyi.Najua James ndiye aliyechafua amani ya Afrika Mashariki na ninataka kumaliza sintofahamu hii.Naomba uandae kikao hicho cha siri baina yetu ili

tuzungumze kama ndugu” akasema Jenerali Akiki

“Umeelekeza kwamba unataka kuzungumza na mimi na Patrice Eyenga,vipi kuhusu Rwanda?Nao pia ni waathirika wa James Kasai” akasema Dr Fabian

“Suala la Uganda na Rwanda halijatokana na James Kasai mheshimiwa Rais.Kuna matatizo yetu ya muda mrefu na sitaki kukaa meza moja na Rwanda”

“Jenerali Akiki nitawasiliana na rais Patrice na kumshawishi akubali tukae na

tuzungumze lakini naomba tafadhali mazugumzo hayo yawe na tija”

“Nakuhakikishia mheshimiwa Rais kwamba sintawapotezea muda wenu nina nia ya dhati ya kulimaliza suala hili.Ninaomba sana iwe mapema zaidi hata kesho kama ikiwezekana”akasema Jenerali Akiki

“Sawa nitawasiliana na Rais Patrice halafu tutaona kama tukutane kesho au siku nyingine.Nitakujulisha”akase ma Dr Fabian

“Nashukuru sana mheshimiwa Rais.Nategemea sana jibu lako” akasema Jenerali Akiki.

Mara tu alipomaliza kuzungumza na Dr Fabian,jenerali Akiki akampigia simu Melanie Davis

“Mheshimiwa rais” akasema Melanie

“Melani habari yako mpenzi wangu”

“Nzuri kabisa mheshimiwa Rais.Nimekuwa nakuwaza sana usiku wa leo.Tayari nimeanza kukumbuka

Uganda” akasema Melanie na wote wakacheka

“Melanie hata mimi nitafurahi sana kama nitakuona tena Uganda.Nategemea utapanga tena safari hivi karibuni” akasema Rais Akiki

“Usihofu mheshmiwa Rais.Nitakuja Uganda tena na tena” akasema Melanie

“Melanie nimekupigia kukujulia hali lakini vile vile kukujulisha kwamba nimetoka kuzungumza na Rais Dr Fabian nimemtaka aandae

kikao cha pamoja na Rais Patrice Eyenga”

“Amekubali?!akauliza Melanie

“Ndiyo amekubali.Nimetaka kikao hicho kiwe kesho lakini amesema atanipa jibu baadae baada ya kuwasiliana kwanza na Rais Patrice na kila mmoja kuangalia ratiba yake.Natumai kwa upande wenu mnaendelea kujiandaa vizuri”

“Ndiyo mzee kwa upande wetu hakuna tatizo,tunasubiri upande wako”

“Msiwe na wasiwasi kila kitu kitakwenda vizuri kama kilivyopangwa ninachowasisitiza ni umakini mkubwa kwani hii ni misheni kubwa.Endapo mtakosea hata kidogo tu basi misheni hii itashindwa kufanikiwa na sisi sote tutakuwa katika matatizo hivyo kumbukeni hakuna kufanya kosa hata dogo.Kila kitu kipangwe kwa umakini mkubwa sana” akasema Jenerali Akiki na kuagana na Melanie.

PARIS – UFARANSA

Kengele ya mlangoni kwa Peniela ikalia akainuka akafikicha macho kisha akachukua kitanza mbali akabonyeza kitufe na mtu aliyekuwa mlangoni akaonekana katika runinga iliyokuwa ukutani

“Maggie unasemaje?akauliza Peniela kwa sauti ya uchovu

“Kuna mgeni wako amefika anasema ana miadi nawe anaitwa Peterson”

“Sawa ninakuja sasa hivi” akasema Peniela akainuka akavaa vizuri kisha akatoka akaelekea sebuleni

“Peterson” akasema Peniela

“Peniela samahani sana kwa kukusumbua lakini nilikuahidi saa kumi na mbili za asubuhi nitafika hapa”

“Karibu sana Peterson.Uliifanya ile kazi niliyokutuma?

“Ndiyo madam.Nimeifanya”akasema Peterson na kufungua mkoba wake akatoa bahasha

akampatia Peniela akaifungua akatoa makaratasi yaliyokuwamo ndani.

“Ni ripoti ndefu hii nitapata muda baadae wa kuipitia naomba unieleze kwa mdomo kile ambacho mmekigundua kuhusu Melanie Davis” akasema Peniela

“Tulichokigundua ni kwamba Melanie Davis ni rais wa Ufaransa lakini hakuna taarifa zake za kueleweka.Watu wanaotajwa kuwa ni wazazi wake na kwamba walifariki dunia hakuna taarifa zozote za

kuwahusu,hakuna mahala wamewahi kusajiliwa kama wafanya biashara na hawajulikani walikuwa wanaishi wapi.Melanie Davis hana makazi hapa Paris wala hakuna biashara yoyote iliyosajiliwa kwa jina lake hapa Ufaransa.Akaunti yake ya benki ina shilingi trilioni tano ambazo hatujui zimetokana na biashara gani.Kwa sasa Melanie anaishi Tanzania ambako amewekeza katika biashara.Ulielekeza tuchunguze pia na watu wake wa karibu tumegundua

kwamba Melanie Davis hana marafiki hapa Paris ila ana mtu mmoja tu ambaye ndiye amekuwa akiwasiliana naye mara kwa mara anayeitwa Devotha Adolph.Tumemchunguza huyo Devotha Adolph tukagundua kwamba huyu Devotha amewahi kuwa wakala wa Mossad”

“Amewahi kuwa wakala wa Mossad?

“Ndiyo.Alikuwa wakala wa Mossad toka akiwa nchini Marekani na hata alipohamia

Tanzania bado aliendelea kuwa wakala wa Mossad”

“Bado anaendelea hadi sasa na kazi hiyo ya uwakala?akauliza Peniela

“Hapana kwa sasa si wakala wa Mossad tena.Ukisoma katika ripoti inaonyesha anaishi kifahari sana hapa Paris anatumia magari ya kifahari ana walinzi wanaomlinda lakini hajulikani anafanya kazi gani ila tumegundua ana ukaribu mkubwa sana na Rais wa Ufaransa ambaye

wanawasiliana karibu kila siku”

“Wana mahusiano gani?

“Uchunguzi unanyesha ukaribu wao ni wa masuala mengine na si mapenzi na tunahisi labda ukaribu huo na Rais ndio unaomfanya aishi maisha ya kifahari” akasema Peterson

“Huyu Devotha ameingia lini Ufaransa?

“Miaka mitatu iliyopita” akajibu Peterson na Peniela akazama mawazoni hakafu akasema.

“Peterson nakushukuru sana kwa kazi hii kubwa mliyoifanya ndani ya kipindi kifupi.Hata hivyo kuna kazi nataka ifanyike leo.Huyu Devotha ninamfahamu na nitahitaji kumfanyia mahojiano leo.Nitampigia simu na kumtaka aje hapa nyumbani kwangu leo hii kwa mazungumzo na atakapotoka

Hapa nataka atekwe apelekwe sehemu mnayotumia kwa mahojiano halafu mtanijulisha” akasema Peniela.

“Sawa madam Peniela.Ahsante kwa kutupa kazi kwani hatukuwa na kazi ya kufanya leo.Utanijulisha mara tu atakapokuwa amefika ili zoezi lifanyike haraka”akasema Peterson

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Mathew na Ruby waliwasili hospitali kuwajulia hali Austin na Gosu Gosu.Siku hii ilianza kwa tabasamu kwani taarifa waliyoipata kutoka kwa daktari ni kwamba

tayari Gosu Gosu alikwisha fumbua macho na hali yake ilikuwa inaendelea vizuri.Hii ilikuwa ni taarifa njema sana kwa akina Mathew.Asubuhi ile hawakuruhusiwa kuingia kumuona ili kumpa nafasi ya kuendelea kupumzika zaidi wakaelekea katika chumba alikolazwa Austin ambaye naye alikuwa anaendelea vizuri.Austin alifurahi sana kusikia kuhusu maendeleo mazuri ya Gosu Gosu.

Baada ya kutoka kumtazama Austin Mathew na

Ruby wakaelekea katika nyumba Fulani.

“Hii ni moja ya nyumba zangu ambazo Peniela haifahamu hivyo nina uhakika haijauzwa.Anayeifahamu ni Gosu Gosu peke yake.Nafikiria kumuhamisha Gosu Gopsu kutoka hospitali na kumleta hapa kwa ajili ya usalama.Pale hospitali hayuko salama hata kidogo” Mathew akamwambia Ruby

“Ni wazo zuri lakini itategemea na madaktari kama watakubali mgonjwa ahame” akasema Ruby

“Watake wasitake lazima Gosu Gosu ahame.Nitaigeuza nyumba hii hospitali kwa ajili ya Gosu Gosu.Kuendelea kuwepo pale hospitali kwa sasa wakati hali yake imenza kuimarika ni kuendelea kuhatarisha maisha yake.Watu wanaotaka kumuua lazima watajaribu tena na tena hadi pale watakapofanikisha lengo lao” akasema Mathew na kushuka garini akaelekea katika geti ambako kulikuwa na kisanduku kidogo cheupe chenye vitufe viwili vya rangi ya kijani na

nyekundu.Akaweka dole gumba katika kitufe cha kijani na mwanga ukatokea halafu zikatokea namba akatabasamu na kubonyeza namba Fulani kisha geti likaanza kufunguka wakaingia ndani.

“Nyumba nzuri lakini inaonekana ina muda mrefu haijakaliwa na mtu yeyote”akasema Ruby

“Ni kweli ina muda mrefu haijakaliwa na mtu.Niliijenga nyumba hii kwa ajili ya kuipangisha lakini baadae niliamua kuifanya kuwa ya mapumziko binafsi.Kila

nilipohitaji kupumzisha akili yangu huja hapa.Nashukuru Gosu Gosu kwa kuendelea kuifanyia usafi na kuiboresha.Naamini hata kama nikifa leo bado watakuwepo watu watakaonienzi na mmoja wao ni Gosu Gosu.Japokuwa iliaminika nimekufa lakini bado vile vitu ambavyo vilinihusu sana amekuwa akivitunza kama vile aliamini siku moja nitarejea" akasema Mathew na kufungua sehemu akatoa funguo akafungua mlango wa sebuleni wakaingia

ndani.Wakazungukia nyumba yote wakaikagua ili kuwa vizuri.

“Nitamleta Lucy kufanya usafi wakati maandalizi mengine ya kuigeuza nyumba hii hospitali kwa ajili ya Gosu Gosu yakiendelea” akasema Mathew kisha wakaondoka kurejea hospitali ambako Mathew alitaka kuzungumza na madaktari kuhusu suala la kumuhamisha Gosu Gosu.

PARIS – UFARANSA

Ni saa tatu za asubuhi jijini Paris gari moja lenye rangi nyeusi liliwasili katika makazi ya bilionea Peniela.Mlango wa mbele ukafunguliwa akashuka jamaa mmoja aliyevaa suti nzuri nyeusi akatazama kila upande kuhakiki usalama halafu akaufungua mlango wa nyuma na mwanadada mmoja akashuka akaelekea katika mlango mkubwa wa kuingilia ndani ambako alipokewa na mwanadada aliyevalia sketi

nyeusi na shati jepesi jeupe akamuongoza kuelekea ndani ya jumba kubwa la Peniela akamkaribisha sebuleni.Baada ya dakika chache akatokea Peniela akiwa amevaa suruali nyeupe,shati jekundu lililokatwa mikono na kofia nyeupe ya mduara.

“Devotha ! akasema Peniela na kukumbatiana na Devotha

“Karibu sana Devotha”akasema Peniela

“Nashukuru sana Peniela kwa kunikaribisha tena katika makazi yako.Nilifurahi sana

uliponipigia simu na kunitaka nifike hapa kwako.Nilikuwa natafuta sana nafasi ya kuja kuonana nawe kuzungumza masuala Fulani muhimu nadhani hii ni fursa nzuri.Ningependa kwanza kusikia kile ulichoniitia kabla sijakueleza ya kwangu” akasema Devotha

“Ahsante sana” akasema Peniela

“Kikubwa nilichokuitia hapa ni masuala ya biashara.Nilitaka kuzungumza na Melanie lakini nikaona nizungumze kwanza

nawe.Kama unavyofahamu mimi ni mfanya biashara mkubwa.Nina makampuni mengi na biashara nyingi.Nilimuuzia Melanie baadhi ya bisahara zangu zilizokoTanzania lakini bado ninazo biashara nyingine barani Afrika.Nina kampuni ziko Afrika Kusini,Misri ,Zimbabwe n.k.Ninataka kuyauza makampuni hayo yote.Sitaki kuendelea na uwekezaji wowote barani Afrika.I'm done with Africa.Ninataka kumpa Melanie nafasi ya kwanza

katika wale ninaofikiria kuwauzia biashara zangu lakini kabla ya kufanya hivyo ninataka kufahamu uwezo wake wa kifedha je unadhani anaweza akamudu gharama za kununua makampuni hayo? Wewe ni mtu wake wa karibu unamfahamu vyema.Naomba uniweke wazi kama anaweza akamudu basi nizungumze naye" akasema Peniela na Devotha akatasamu.

"Melanie ni tajiri sana sidhani kama anaweza akashindwa kununua makampuni hayo.Ana fedha za

kutosha ndiyo maana hata ulipomtajia bei ya makampuni yale ya Dar es salaam hakusita wala hakuomba kupunguziwa.Uwezo anao wa kununua makampuni zaidi kama utapenda kumuuzia” akasema Devotha

“Nimefurahi sana kusikia hivyo.Ninataka kuyaacha makampuni hayo kwa mtu ambaye atakuwa na uwezo wa kuyaendeleza sitaki nimuuzie mtu makampuni halafu nisikie baada ya mwaka mmoja kumebaki magofu”

“Nakuhakikishia Peniela ,Melanie anao uwezo mkubwa wa kununua makampunio hayo” akasema Devotha na Peniela akapokea simu akazungumza kwa muda kisha wakaendelea na maongezi

“Ukiacha biashara zile nilizomuuzia Melanie kule Tanzania,ni biashara zipi nyingine anamiliki?akauliza Peniela na swali lile likaonekana kumbabaisha kidogo Devotha

“Melanie utajiri wake ni wa kurithi.Wazazi wake walikuwa matajiri wakubwa

sana na walipofariki katika ajali ya gari Melanie akaendeleza utajiri wa wazazi wake” akasema Devotha

“Wazazi wake walimiliki biashara zipi hapa Ufaransa?akauliza Melanie

“Sifahamu sana mambo ya Melanie.Nimekutana naye hapa hapa Ufaransa tukawa marafiki hivyo mambo mengi kuhusiana na biashara zake siyajui bado”Devotha akaonekana kukwepa kuzungumzia kuhusu biashara za Melanie

“Peniela kwa nini unataka kuuza mali zako zote Afrika?akauliza Devotha

“Kama nilivyosema I’m done with Afrika.Sitaki tena kuwekeza kule”akasema Peniela

“Ni kwa sababu ya kifo cha mumeo?

“Ndiyo.Hiyo ni sababu kubwa iliyonifanya niichukie Afrika na ndiyo maana nataka kuuza kila kitu sitaki kurejea tena kule”akasema Peniela.Waliendelea na maongezi mengine na baada ya muda Peniela akasema

“Devotha ulisema kuna kitu ulitaka kunieleza tukionana ni kitu gani hicho?

Devotha akavuta pumzi ndefu na kusema

“Nina mpango wa kuwania urais wa Tanzania” akasema Devotha na Peniela akastuka

“Unataka kuwania urais?

“Ndiyo.Ninataka kuingia katika mbio za kuwania urais wa Tanzania”

“Umenistua.Hadi kupata nafasi ya kuingia katika kinyang’anyiro cha kuwania urais si jambo dogo”

“Ni kweli hicho unachokisema Peniela lakini ninao mtandao ambao ndio unaonitengenezea mambo hivyo ninahitaji sana pale muda utakapofika ninyi watanzania wenzangu mniunge mkono ili niweze kufanikisha ndoto yangu hiyo”

“Dah ! hongera sana kwa kuwa na ndoto kubwa namna hiyo.Uongozi wa nchi si jambo dogo Devotha inahitaji uzoefu mkubwa”

“Ninao uzoefu wa kutosha.Ninayafahamu

majukumu ya Rais na ndiyo maana ninaamni nitaweza”

“Umewahi kufanya kazi kulu?

“Nilikuwa mkurugenzi wa SNSA.Secret National security Agency.Hii ni idara nyeti sana ambayo inashughulika na usalama wa ndani ya nchi na kwa kuwa kiongozi wa idara hii ambayo iko chini ya Rais ikulu kulikuwa ni kama nyumbani.Hapo ndipo nilipopata nafasi ya kufahamu mambo mengi kuhusiana na kazi ya urais na ndiyo maana nikasema kwamba ninaweza

kuongoza nchi” akasema Devotha

Mara tu Devotha alipotamka SNSA Peniela akastuka

“Mathew alitamka hii idara wakati ananieleza kile kilichomtokea hadi akapotea.Kumbe huyu amewahi kufanya kazi katika idara hiyo.Vile vile Mathew aliniambia kwamba alitekwa na watu wa Mossad wakati wa operesheni ya kubadilishana mateka kati yao na magaidi wa IS lakini mpaka leo hii hata yeye hajui Mossad

walifahamuje kuhusu mabadilishano yale.Sasa nimepata picha.Huyu alikuwa mkurugenzi wa SNSA na vile vile akawa ni wakala wa Mossad.Kama anamfahamu Mathew basi huyu ndiye atakuwa alimuuza Mathew kwa Mossad.Nitafahamu kila kitu leo mimi na yeye.”akawaza Peniela

“Kwa nini uliacha kazi hiyo ya ukurugenzi katika idara ya SNSA?akauliza Peniela

“Niliacha kazi ili nianze mchakato wa urais”

“Kwani hapa Ufaransa umekaa kwa muda gani?

“Nina miaka mitatu sasa” akajibu Devotha

“Devotha mimi nimefurahi sana kusikia una ndoto kubwa namna hiyo.Nitakuunga mkono lakini pale utakapokuwa umechaguliwa na chama chako kugombea.Gharama zote za kampeni ni juu yangu mimi.Nitatoa ndege,helkopta na magari kwa ajili ya kukusaidia katika kampeni zako” akasema Peniela

“Peniela ninakushukuru mno kwa kunielewa na kuahidi kunisaidia.Sijui nikushukuruje”

“Usijali.Ni lazima nikuunge mkono mwanamke mwenzangu” akasema Peniela akazungumza kidogo na simu halafu akasema

“Samahani Devotha unajua ninapokea simu nyingi za biashara hivyo univumilie”

“Ninaelewa Peniela usijali”

“Ulisema uliongoza idara ya SNSA ulimfahamu mume wangu Mathew Mulumbi?Huyo naye alikuwa

anashughulika na masuala hayo hayo ya usalama”akauliza Peniela na Devotha akaoyesha mstuko kidogo

“Mathew Mulumbi?! Akauliza Devotha

“Ndiyo aliwahi kufanya kazi na idara yenu?

“Hapana hajawahi kufanya kazi na idara yetu” akajibu Devotha.Waliendelea na mazugumzo halafu Peniela akamtaka radhi Devotha akaelekea chumbani kwake akachukua simu na kumpigia Peterson Lebrave mkurugenzi

wa kampuni ya wapelelezi wa kujitegemea

“Madam Peniela” akasema Peterson

“Peterson mtu Yule tayari ninaye hapa ndani vijana wako tayari wamejipanga?akauliza Penila

“Vijana wangu wako tayari.Atakapotoka hapo kwako utanijulisha” akasema Peterson

kisha Peniela akarejea sebuleni alikomuacha Devotha wakaendelea na maongezi kuhusu mambo mbali mbali ya maisha na kubwa likiwa ni

suala la Devotha kuwania urais.Dakika arobaini baada ya Peniela kuzungumza na Peterson simuni Peniela akamuomba radhi Devotha kwamba anahitajika ofisini.Wakaagana kwa miadi ya kukutana tena kwa mazungumzo zaidi.Peniela akamsindikiza Devotha hadi katika gari lake wakaagana akaondoka.Peniela akamtumia ujumbe Peterson kumjulisha kwamba Devotha anatoka getini.

Eneo la makazi ya Peniela lilizungukwa na miti mingi na

kutoka katika makazi hayo hadi kukuta barabara kuu ni umbali wa kilometa moja na nusu ukipita katika msitu.Walipokaribia daraja katika mto unaopita katika msitu ule wakayakuta magari mawili yameegeshwa.Dereva wa gari la Devotha akapunguza mwendo.Alipotazama katika kioo cha pembeni akaona kuna gari nyingine mbili zinakuja nyuma yao pamoja na piki piki mbili.

“Kuna nini kinaendelea pale darajani?akauliza mlinzi

wa Devotha aliyekuwa amekaa kiti cha mbele

“Nashangaa kwa nini zile gari mbili zimeegeshwa pale darajani” akajibu dereva.Waliyakaribia yale magari mawili yaliyokuwa yameegeshwa darajani na kusimama dereva akapiga honi na mara pikipiki mbili zilizokuwa zikija nyuma yao zikafika na wale jamaa wawili wakachomoa silaha na kuanza kumiminia risasi dereva na mlinzi wa Devotha wote wakafa pale pale.Devotha alikuwa anatetemeka mwili

kwa woga.Haraka sana watu wengine sita wakashuka kutoka katika magari mlango gari la Devotha ukafunguliwa akashushwa na kufunikwa mfuko kichwani akaingizwa katika mojawapo ya gari lililokuwa limeegeshwa darajani kisha likaondoka kwa kasi.Maiti za dereva na mlinzi wa Devotha zikaingizwa katika gari lingine na kuondolewa pale kisha usafi ukafanyika eneo lile kuhakikisha kwamba hakuna hata kioo kitakachoonekana.Mkoba wa Devotha ukachukuliwa simu

yake ikazimwa,gari lake likapekuliwa kisha likasukumwa likaangukia mtoni.Baada ya kuhakikisha kila kitu kimekwenda vizuri wale jamaa wakaondoka zao.

****

Peniela akiwa nyumbani kwake akajulishwa kwamba kila kitu kimekwenda vizuri na akaelekezwa mahala alikopelekwa Devotha

“Ni wakati wa kwenda kutafuta majibu.Yule mwanamke anamfahamu

vyema Melanie na leo atanieleza Melanie ni nani hasa? Nilimuahidi Mathew kumtafutia majibu kuhusu Melanie na sasa ninakwenda kuupata ukweli” akawaza Peniela na kuvua mavazi aliyokuwa amevaa akavaa suruali ya jeans na fulana vyote rangi yeusi akavaa na kofia nyeusi akaondoka bila dereva wala mlinzi akaelekea mahala alikoelekezwa na Peterson kwamba ndiko anakoshikiliwa Devotha.

“Kabla ya kukutana na Mathew Mulumbi niliwahi

kufanya kazi na Team SC41.Ni kazi ya hatari sana nilikuwa naifanya lakini ni Mathew ndiye aliyeniondoa katika maisha yale na nikawa hivi nilivyo leo.Kila nikiyakumbuka maneno yale niliyomtakia jana roho yangu inaumia mno.Sikupaswa kumtamkia maneno kama yale.Sijui nitafanya nini kuyafuta maneno yale katika akili yake.Lakini kwa nini niliaamua kuchukua maamuzi kama yale?Je yalikuwa ni maamuzi sahihi?Toka ndani kabisa mwa moyo wangu

ninampenda sana Mathew na hatatokea mwanaume ambaye nitampenda kama yeye” akawaza Peniela

Peniela alifika mahala alikopelekwa Devotha.Ilikuwa ni katika bohari moja kuu kuu lililoonekana kutelekezwa.Aliingiza gari ndani ya bohari lile akashuka na kupokewa na Peterson

“Ahsante sana Peterson kwa kuifanikisha kazi hii kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa” akasema Peniela wakati wakielekea katika ofisi ya Peterson

“Madam Peniela kama nilivyokueleza kwamba vijana wangu hawakuwa na kazi ya kufanya leo ndiyo maana wakaifanya kazi ile kwa haraka sana” akasema Peterson wakaelekea katika ofisi yake akamweleza Peniela namna zoezi la kumteka Devotha lilivyofanyika na kila hatua waliyochukua kuhakikisha wanaondoa kila ambacho kingeweza kuleta matatizo endapo uchunguzi wa kutoweka kwa Devotha ungefanyika.Peniela akafurahi na kuahidi kuwalipa mara

mbili ya kiasi walichokuwa wamehitaji.

“Huyu mtu unataka tumfanye nini?akauliza Peterson

“Huyu nataka mniachie mimi mwenyewe nitashuhulika naye.Kuna taarifa muhimu sana nazihitaji kutoka kwake” akasema Peniela na kupelekwa katika chumba kilichokuwa na kioo kikubwa akamtazama Devotha akiwa ndani ya chumba kingine amefungwa katika kiti.

“Hatujampa mateso yoyote tulikuwa tunakusubiri kwanza ufike” akasema Peterson

“Ahsante Peterson nifungulieni mlango nizungumze naye” akasema Peniela na kufunguliwa mlango akaingizwa ndani ya kile chumba alimo Devotha.

“Hallo Devotha ! akasema Peniela huku akitabasamu akavuta kiti akaketi akatoa kofia na miwani.Mstuko alioupata Devotha ulikuwa mkubwa.Alihisi yuko njozini na si kitu cha kweli anachokishuhudia

“No ! This is not true ! akasema Devotha

“It’s true Devotha.Unachokiona si njozi ni kitu cha kweli kabisa.Aliyeko mbele yako ni mimi Peniela” akasema Peniela na Devotha akamtazama kwa hasira

“Wewe ndiye uliyenifanyia hivi?! Akauliza kwa ukali

“Ndiyo Devotha ni mimi!

“Kwa nini Penielea?Nimekukosea nini hadi unifanyie hivi?akauliza Devotha

“Devotha nimekuleta hapa kwa mahojiano na ninakuomba unijibu kwa ufasaha maswali nitakayokuuliza na endapo utaleta mzaha au kiburi this will be the end of the road for you” akasema Peniela

“Don’t threaten me Peniela.Hunifahamu mimi ni nani na huna uwezo wa kuniamuru chochote.Kwa taarifa yako mambo kama haya nimeyapitia ninafahamu kila kitu na huwezi ukanitishia kunitesa.Peniela nakushauri usitake kungia katika matatizo

makubwa.Mimi si mtu wa kutaka kuingia naye katika matatizo.Nakushauri tulia na maisha yako mazuri haya mengne yaache kabisa! akasema Devotha

“Devotha ninakufahamu vizuri wewe ni nani.Ninaifahamu historia yako umetoka wapi na hadi umefika hapa na ninakuhakikishia kwamba bado hujawahi kupitia mateso.Bado hujawahi kuaona mateso na leo utayashuhudia labda ukubali kutoa ushirikiano ndipo utajiokoa

lakini kama ukiwa kiburi basi utazungumza lugha zote unazozifahamu leo ! akasema Peniela

“Peniela nani wanataka kukuingiza katika matatizo haya makubwa?akauliza Devotha

“Devotha ninataka unieleze kuhusu Melanie Davis.Nimegundua kwamba anashrikiana na kikundi cha kigaidi cha IS na wewe kama mtu wake wa karibu lazima jambo hili unalifahamu vizuri.Nataka unieleze ukweli

Melanie Davis ni nani ?
Akauliza Peniela

“You go to hell shetani wa kike wewe ! akasema Devotha kwa ukali

“Huwezi ukaniweka hapa na kunihoji maswali.Wewe ni mtu mdogo sana wa kunihoji mimi ! akaendelea kufoka

“Devotha nimekuuliza swali naomba unijibu.Melanie Davis ni nani?Peniela akauliza

“Siulizwi maswali na panya mchafu kama wewe ! akasema Devotha.

“Devotha nimekuuliza Melanie Davis ni nani?akauliza Peniela

“We kahaba siwezi kukujibu swali lako lolote.Please go to hell ! akasema Devotha

“Sawa Devotha tutaona mimi na wewe nani atakayetangulia kwenda huko unakosema niende ! akasema Peniela na kubonyeza kitufe na Peterson akaingia

“Naomba niandaliwe vifaa ! akasema Peniela na Peterson akafungua kabati la chuma

akatoa vifaa mbalimbali akaviweka mezani

“Unahitaji msaada wowote Peniela? Akauliza Peterson

“Huyu nitashughulika naye mimi mwenyewe.Ninahitaji watu wawili kwa ajili ya kumshika.Nataka nimuonyeshe kweli mimi ni shetani wa kike ! akasema Peniela.Peterson akawaita jamaa wawili wakaingia mle ndani Peniela akaenda mezani akachukua mkasi wa kukatia vitu vigumu

“Devotha hii ni mara ya mwisho nitakuuliza.Melanie Davis ni nani? Akauliza Peniela

“Peniela narudia kukuonya kwamba usiendelee na mchezo huu utajuta sana baadae” akasema Devotha na Peniela akawaelekeza wale jamaa wawili waliojazia miili wamkamate Devotha wamfunge katika kitanda cha chuma kilichokuwamo mle ndani.Devotha akanyanyuliwa na kufungwa katika kitanda kile

“Melanie Davis ni nani?akauliza Peniela Devotha akamtemea mate usoni.Peniela akakishika kiganja cha mkono mmoja wa Peniela uliokuwa na vidole vitatu na kwa kutumia mkasi akakikata kidole cha mwisho

“Aaaaaaaaghhh !! Devotha akatoa ukelele

“Melanie Davis ni nani?akauliza Peniela

“Nitakuua Peniela ! akasema kwa hasira Devotha .Peniela akakishika kidole kingine na kukikata Devotha akaendelea kupiga kelele.

“Who is Melanie Davis?akauliza Peniela.Devotha aliendelea kupiga kelele kubwa kwa maumivu makali aliyoyapata.

“Devotha nilikutahadharisha toka awali kwamba huu unaweza ukawa ni mwisho wako kama hautakuwa makini na ninarudia tena kukutahadharisha kwamba endapo hautakuwa makini huu utakuwa mwisho wako.Sina utani na Mungu atanisamehe kwani nitakufanyia kitu kibaya

sana ! akasema Peniela kwa ukali lakini bado Devotha alikuwa anatetemeka na kulia kwa maumivu makali.Peterson akamsogelea Peniela akamnong'oneza kitu halafu akafungua droo na kutoa chupa yenye dawa ya chumvi chumvi akaenda kupaka mahala Peniela alipokata vidole.Devotha alitoa kelele kubwa akijaribu kujitoa katika kamba zile lakini alifungwa barabara.Aliweweseka akizungumza maneno kama mwenda wazimu.

“Ulisema huogopi mateso na huu ni mwanzo Devotha.Nitakuharibu haribu leo.Naomba tafadhali unieleze Melanie Davis ni nani? Akauliza Peniela lakini Devotha hakujibu kitu aliendelea kulia huku akiweweseka kwa maumivu makali.

“Devotha nitamaliza vidole vyote vya mikono na utabaki huna hata kidole kimoja.Malengo yako ya kuwa Rais yanakwenda kupotea .Tafadhali nijibu ili tuyamalize haya mambo ! akasema

Peniela ambaye alikuwa na hasira kama Mbogo.Devotha aliendelea kulia Peniela akaushika tena mkasi akakimalizia kidole kilichokuwa kimebakia.Devotha aliendelea kupiga kelele kubwa hadi sauti ikaanza kukwama.

“Devotha nimemaliza kiganja cha kwanza ninahamia kiganja cha pili.Nimekwambia leo nitakufanyia ukatili ambao haujawahi kuushuhudia” akasema Peniela na kukishika kidole cha mwisho cha mkono mwingine akakikata.

“Peniela please !! Niko chini ya miguu yako tafadhali usiendelee kunitesa nama hii.Nimekukosea nini hadi unifanyie hivi?akauliza Devotha akiwa katika maumivu makali

“Melanie Davis ni nani?akauliza Peniela

“Nitakwambia Peniela tafadhali usiendelee kunitesa namna hii ! akasema Devotha

“Nataka unieleze kila kitu kuhusu Melanie Davis! Akasema Peniela

“Melanie Davis….

“Ndiyo nataka unieleze ni nani?Ana mipango gani nchini Tanzania? Akauliza Peniela.Devotha akavuta pumzi ndefu kisha akasema

“Melanie ..aaahg.....ni mfanya biashara....Aaagh Peniela umeniharibu kwa nini lakini? Akaendelea kulia

“Melanie anashirikiana na magaidi wa IS wana mipango gani nchini Tanzania?akauliza Peniela Devotha hakujibu akaendelea kugugumia kwa maumivu

“Devotha naomba jibu haraka sana kabla sijaendelea kukuharibu ! akasema Peniela

“Nitakueleza ukweli Peniela” akasema Devotha na kuvuta pumzi ndefu mara tatu halafu akasema

“Melanie nimekutana naye…aaaghh ! akanyamaza na kufumba macho kwa maumivu makali halafu akaendelea

“Nimekutana naye hapa Paris na tukawa marafiki.Akanieleza anataka kuwekeza Afrika nikamshauri akawekeze Tanzania na ndipo nilipoambatana naye kuja

kwako kutaka kununua makampuni yako.Simfahamu kwa undani na wala sifahamu kama anashirikiana na magaidi ! akasema Devotha

“Devotha unanidanganya ! akasema Peniela na kukibana kidole kwa mkasi

“Peniela usinikate kidole tafadhali ninachokueleza ni kitu cha kweli kabisa.Simfahamu vizuri Melanie ! akalia Devotha.

“Peniela nionee huruma unaniumiza bure sifahamu chochote kuhusu mambo anayoyafanya

Melanie.Nilimsaidia kumleta kwako na sifahamu mambo yake mengine ! akaendelea kuomba Devotha

“Unafanya kazi gani hapa Paris? Akauliza Peniela,Devotha akawa kimya

“Unaishi maisha ya kifahari hapa Ufaransa unafanya kazi gani?akauliza tena Peniela na kukibana kidole

“Usikate Peniela nitakwambia.Nina gharamiwa na Rais wa Ufaransa.Ninamshauri kuhusu

masuala ya Afrika” akasema Devotha

“Ulinieleza kwamba uliwahi kufanya kazi SNSA nikakuuliza kama unamfahamu Mathew Mulumbi ukakana kutomfahamu.Nakuuliza tena kwa mara nyingine tena unamfahamuMathew Mulumbi? Akauliza Peniela

“Devotha nakuuliza kwa mara ya mwisho unamfahamu Mathew Mulumbi? Akauliza Peniela na kuendelea kukibana kidole

“Peniela utaniua jamani usinikate tena vidole vyangu.Nitaishi vipi mimi?akalia Devotha

“Nitakuua kweli kama hautanieleza ukweli”akasema Peniela

“Ninamfahamu Mathew Mulumbi”

“Mathew alishirikiana na idara uliyokuwa unaiongoza kuwakomboa mateka waliotekwa na IS lakini alitekwa na Mossad na hajulikani alipo.Nataka unieleze ukweli nani aliyewapa taarifa Mossad kuhusu

operesheni ile aliyokwenda kuifanya Mathew? Akauliza Peniela

“Sifahamu chochote Peniela” akasema Devotha

“Devotha nafahamu wewe ulikuwa wakala wa Mossad.Niambie ukweli kama ni wewe uliyewapa taarifa za Mathew Mulumbi na wakamteka?akauliza Peniela Devotha alishindwa kujibu.Peniela akakibana kidole na kukikata kikaruka.Devotha akalia kwa uchungu lakini sauti ilikwama kutoka

“Devotha niambie ukweli ama sivyo huu utakuwa ni mwisho wako ! akasema Peniela kwa hasira lakini Devotha hakujibu alifumba macho akigugumia kwa maumivu huku akizungumza maneno yasiyoeleweka.

Peniela akatupa ule mkasi akaenda kuchukua shoka dogo na kuwataka wale jamaa waufungue mkono mmoja wa Devotha na kuuweka katika meza

“Devotha ni wazi wew e ndiye uliyemuuza Mathew kwa Mossad.Ninakusamehe

kwa hilo lakini nataka unieleze nini mipango ya Melanie Davis na IS nchini Tanzania ! akasema Peniela Devotha bado aliendelea kumwaga machozi.Peniela akainua shoka juu kwa ajili ya kukata kiganja cha mkono Devotha akapiga kelele akimtaka asimkate

“Nitakueleza Peniela.Nitakueleza kila kitu tafadhali usinikate mkono” akasema Devotah

“Nieleze haraka sana mipango ya Melanie na IS ! akafoka Peniela

“Sifahamu mpango wowote wa Melanie na IS ! akasema Devotha na bila kuuliza mara ya pili Peniela akainua shoka juu na kulishusha kwa nguvu katika kiganja cha mkono kikaruka chini.Devotha alishindwa kupiga kelele kwani sauti haikutoka tena

“Devotha kinachofuata nitaukata mkono mzima.Leo nitakuondoa kiungo kimoja kimoja kama hautanieleza ukweli.Nataka uniambie mipango ya Melanie na IS ! akasema Peniela Devotha

aliendelea kukoroma sauti haikuwa inatoka.Peniela akakasirika na kuukata mkono katika bega

“Devotha nieleze ukweli! Akasema Peniela.Peterson akamsogelea akamnong’oneza sikioni

“Peniela huyu hataweza kusema chochote tena.Kiwango cha mateso alichokipata ni kikubwa sana! Kwa hatua hii aliyofikia kuna kitu kimoja tu cha kufanya ni kumuua”Akasema Peterson

“Devotha nina hasira sana nawe kwani umeyavuruga

maisha yangu. Kitendo chako cha kumuuza Mathew kwa Mossad kimesababisha hadi sasa maisha yangu yakose furaha kwani siwezi tena kuwa na mtu niliyempenda katika maisha yangu! Mathew ameteswa na kumizwa mno na kwa ajili yako leo nitamlipia kisasi ! akasema Peniela huku akimtazama Devotha kwa hasira

“Naomba u…u.uuusi….niue ! akaomba Devotha macho lakini Peniela aliyekuwa na hasira kama Mbogo akalishusha kwa nguvu

shoka likatua katika goti na kuutenganisha mguu.

“Hii ni kwa ajili ya Mathew na mateso yote aliyoyapitia kwa sababu ya tamaa zako ! akasema kwa hasira na kuukata mguu wa pili.

“Nilikwambia nitakufanyia unyama mkubwa sana leo ! akasema Peniela na kumtazama Devotha

“Kwa heri Devotha ! akasema Peniela na kushusha shoka kwa nguvu katika shingo ya Devotha na kuhitimisha safari yake ya maisha hapa duniani.Peniela akaenda

katika chumba kilichokuwa na tanuru kubwa kwa ajili ya kuchomea miili akavua zile nguo zilizokuwa zimetapakaa damu akavaa nguo nyingine alizokuwa amekwenda nazo halafu akarejea ndani ya kile chumba Peterson akampa karatasi

“Hii ni orodha ya namba za simu ambazo Devotha amekuwa akiwasiliana nazo mara kwa mara” akasema Peterson.Peniela akaipitia ile orodhana kukuta kuna namba nne kutoka Tanzania ambazo

Devotha alikuwa anawasiliana nazo.

“Ahsante Peterson” akasema peniela na kuchukua simu yake akampigia Mathew kwa njia ya video

“Hallow Peniela” akasema Mathew baada ya kupokea simu

“Mathew kabla ya kukueleza chochote kuna kitu nataka ukitazame” akasema Peniela na kuisogeza kamera ya simu karibu na mwili uliokatwa katwa wa Devotha

“Unaweza ukaitambua sura hii” akauliza Peniela

“Oh my God that’s Devotha ! akasema Mathew kwa mshangao

“I killed this devil !

“You what ?! Mathew akauliza

“Nimemuua.Huyu ndiye aliyekuuza kwa Mossad.Alikuwa wakala wa Mossad wakati ule na ndiye aliyewapa taarifa zako wakakuteka”

“Jesus ! akasema Mathew

“Huyu ndiye mshirika mkubwa wa Melanie Davis.Mathew hawa watu watakuwa na mipango

mikubwa sana kwani Devotha amekuwa tayari kufa kuliko kueleza kile ambacho MelanieDavis anapanga kukifanya”

“Melanie na Devotha wanafahamiana?

“Ndiyo wanafahamiana na Devotha ndiye aliyemleta kwangu Melanie” akasema Peniela

“Sijapata kitu chochote cha maana kutoka kwake kuhusu Melanie lakini nimepata namba nne ambazo amekuwa akiwasiliana nazo mara kwa mara nchini

Tanzania.Mtazifuatilia kuwafahamu watu ambao amekuwa akiwasiliana nao.” akasema Peniela

“Peniela sijui nikushukuruje kwa hiki ulichokifanya”

“Mathew hawa ndo waliosababisha mimi nawe tukatengana hivyo nina hasira nao sana.Nimefanya hivi kwa ajili yako.Tafadhali hakikisha unampata Melanie Davis.Nimetumia wapelekezi wa kujitegemea kutafuta taarifa za Melanie lakini walichokipata

kinashangaza.Hakuna biashara zozote zilizosajiliwa kwa jina lake hapa Ufaransa,hajulikani mahala anakoishi hapa Paris,hakuna taarifa zozote za kueleweka kuhusu wazazi wake lakini akaunti yake ina kiasi kikubwa cha fedha karibu trilioni tano.Ninaweza kusema kwamba huyu Melanie Davis amevaa uhusika bandia kwani taarifa zake zote zilizopo zinaonekana ni za kutengenezwa kwa madhumuni Fulani na ninahisi hata wakubwa wa serikalini

hapa Ufaransa wanalifahamu hilo jambo kwani Devotha ambaye nimemuua ana ukarbu mkubwa sana na Rais wa Ufaransa ambaye tunahisi ndiye anayemfanya aishi maisha ya kifahari hapa Paris.Hicho ndicho nilichoweza kukipata Mathew” akasema Peniela

“Peniela nimekosa neno zuri la kukushukuru kwa hiki ulichokifanya” akasema Mathew

“Usinishukuru Mathew.Ni wajibu wangu kukusaidia.Kama kuna kitu

chochote kingine ambacho unataka nikusaidie usisite kuwasiliana nami.Mwisho kabisa Mathew I’m very sorry for what I said yesterday.Sikupaswa kukutamkia maneno kama yale.Ni wewe uliyenifikisha hapa nilipo leo.Nisamehe sana zilikuwa ni hasira tu” akasema Peniela

“Usihofu Peniela yale yamekwisha pita” akasema Mathew na kuagana na Peniela

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Mathew Mulumbi akavuta pumzi ndefu baada kumaliza kuzungumza na Peniela.Kwa sekunde kadhaa alifumba macho yake halafu akayafumbua akamgeukia Devotha aliyekuwa pembeni yake.Walikuwa wameegesha gari pembeni ya barabara wakati Mathew akizungumza na Peniela

“Hatimaye shetani amepatikana na kuuawa ! akasema Mathew na ujumbe

ukaingia katika simu yake ukitoka kwa Peniela.Alikuwa amemtumia namba za simu za watu walioko Tanzania ambao wamekuwa wakiwasiliana na Devotha pamoja na picha za mwili wa Devotha baada ya kuuawa.Mathew akamuonyesha Ruby picha alizotumiwa na Peniela.Ruby alijikuta akibubujikwa machozi

“Nimeshindwa kuvumilia Mathew kwa furaha niliyonayo kwa huyu mwanamke kuuawa.Nilichungulia kaburi kwa sababu yake.Siku nyingine ukiwasiliana na Peniela

naomba umpe shukrani zangu kwa hiki alichokifanya kumuua Devotha” akasema Ruby huku akifuta machozi

“Kwa mujibu wa Peniela huyu ndiye aliyewapa Mossad taarifa za operesheni ile na wakaniteka.Nashukuru Peniela amenilipia kisasi kwa mateso niliyoyapitia”

“Hukuwahi kuniambia kama ulitekwa na Mossad lakini Peniela ulimweleza ! akasema Ruby

“Muda utafika nitakueleza kila kitu.Lakini huyu mwanamke ndiye chanzo cha

mateso yote niliyoyapata. Anastahili kufa kifo cha namna hii” akasema Mathew

“Peniela ametuma namba hizi za watu ambao wamekuwa wakiwasiliana na Devotha,tuanze kuzifuatilia kuwafahamu wenye namba hizi.” akasema Mathew kisha Ruby akaichukua kompyuta yake akaweka sawa program zake na kuanza kupiga zile namba.Namba tatu hazikuwa zinapatikana na alipoingiza namba ya nne kwa ajili ya kupiga akastuka kwani alikuwa nayo ile namba tikana.

“Edwin Mbeko ! akasema Ruby

“Edwin Mbeko?Mathew naye akauliza

“Ndiyo hii ni namba yake” akasema Ruby

“Sasa picha imeanza kujitengeneza Ruby.Hebu tazama huu mtiririko.Devotha ambaye ni mtu wa karibu na Melanie amekuwa na mawasiliano na Edwin Mbeko wa SNSA.Jana tumempoteza Khalid Sultan kwa kitendo kilichofanywa kwa makusudi na watu ndani ya SNSA aliko Edwin.Kwa Edwin kuwa na

mawasiliano na Devotha ambaye ni mtu wa karibu na Melanie nalazimika kuamini kwamba lazima Edwin atakuwa katika mtandao wa akina Melanie na ndiye anayewezesha mambo ya yote ya matandao huo kufanikiwa” akasema Mathew

“Mathew hapa nilipo ninahisi mwili wote unanitetemeka kwa woga.Sikutegemea kabisa kama Edwin angeweza kuwepo katika mtandao huu” akasema Ruby na Mathew akamtaka awashe gari

“Tunaelekea wapi?

“Tunakwenda nyumbani nikachukue silaha kisha tunamfuata Edwin ofisini kwake SNSA”

“Hawataturuhusu kuingia pale kwani mimi si mkurugenzi kwa sasa hadi suala langu litakapotatuliwa”

“Ndiyo maana ninakwenda kuchukua silaha zitakazotuwezesha kungia pale SNSA”

“Mathew huo ni mpango wa hatari kubwa.Ofisi ile ina ulinzi mkali na si rahisi kuivamia” akasema Ruby

“Tutaingia pale ndani na lazima tumpate Edwin.Usihofu Ruby uko na Mathew Mulumbi the unstoppable! akasema Mathew

“Mathew naomba nikushauri mpenzi wangu.Kwa mchana huu tulikuwa na mpango wa kumshughulikia Gosu Gosu.Tumuhamishe Gosu Gosu na kuhakikisha anakuwa sehemu salama halafu usiku wa leo ndipo tukavamie SNSA na kumchukua Edwin.Naamini mpaka muda huo hatakuwa anafahamu kama Devotha

ameuawa na wala hatakuwa akijua kama tumefahamu ana mawasiliano na Devotha” akashauri Ruby.Mathew akafikiri kisha akasema

“Ushauri mzuri.Tumuhamishe kwanza Gosu Gosu na kumpeleka sehemu salama halafu nitamonyesha Yule Edwin na mtandao wake mimi ni nani” akasema Mathew

MPENZI MSOMAJI
TUNAPOKARIBIA
KUMALIZA SIMULIZI HII
YA MAISHA NA KIFO CHA
MELANIE CHUMA KAA
TAYARI KWA AJILI YA
SEHEMU YA TATU NA YA
MWISHO YA SIMULIZI YA
SIRI ITAKAYOJULIKANA
KAMA
JASUSI/GAIDI.
TUKUTANE SEHEMU IJAYO